**p. Lorenzo Sales m.d.c.**

# kifupisho cha maisha

# YOSEF ALLAMANO

**MWANZILISHI WA WAMISIONARI NA MASISTA WAMISIONARI WA CONSOLATA**

*ukurasa 1*

p. Lorenzo sales m.d.c.

# kifupisho cha maisha
# ya Kanoni
# YOSEF ALLAMANO

**MWANZILSISHU WA WAMISSIONARI E MASISTA WAMISIONARI WA CONSOLATA**

**Toleo la pili**

**TORINO**
**ISTITUO MISSIONI CONSOLATA**

**Kimetafsiriwa na P. Livio Ferraroni IMC**

*Ukurasa 2*

*Tupu*

*Ukurasa 3*

ichapwe

Torino, 7 Machi 1938 -

P. Gaudenzio Barlassina. Sup. Gen.

*Ukurasa 4*

*Tupu*

*Ukurasa 5*

*Picha*

KANONI YOSEF ALLAMANO

*Ukurasa 6*

*Tupu*

*Ukurasa 7*

Kwako Msomaji

*KIFUPISHO hiki imetolewa ili kuridhisha maombi mengi ya wapenda Kan. Yosef Allamano na marafiki wa Misioni za Consolata.*

*Ikilinganishwa na kazi kamilifu, inaonekana kama mswada mbele ya utekelezaji wa picha, lakini tunaamini kuwa sura ya mpendwa mwanzilishi wetu ionekane kamilifu, na hai, katika mwanga wa fadhila zake na kazi yake.*

*Lafudhi ya kawaida na kushinda kwa mfumo wa masimulizi zimekusudiwa ili kufanya*

*Ukurasa 8*

*kitabu kisomwe na kila tabaka ya watu, kumbe kasoro la virejeo limekusudiwa kurahisisha usomaji. Msomaji lakini atahakikisha kuwa – na akitaka ataweza kutumia kitabu asilia – kuwa kila tukio na kila wazo yaliyomo hapa, hutegemea ushahidi wa kustahili imani, ambazo kwa wingi hutokana na watu wa Kanisa na walei wa Pidmont.*

*Lengo lililotuongoza katika kazi hii ndogo, na pia tuzo tunaloomba kwa Mungu ni moja tu: ili na KIFUPISHO hicho kitende mema: kuwashia rohoni upendo wa ukarimu zaidi kwa Yesu na ibada ya moyoni zaidi kwa B. Maria Consolata; kuwapelekea kuheshimu zaidi upadre wa Kanisa Katoliki na ari zaidi kuhusu wokovu wa roho za wapagani.*

*Torino, 14 Februari 1938*

*P. Lorenzo Sales I.M.C.*

*Ukurasa 9*

# 1.
# Padre
# na mtume

*Ukurasa 10*

“... Tunashuhudia rasmi shukrani yetu kwako, ambaye tunaona unastahili, kwa namna ya pekee, kwa sababu ya mengi mastahili, ambayo wakati wa huduma yako ndefu ya kipadre, ulijipatia mintarafu Kanisa la Mungu, na pia katika mambo ya kibinadamu na kijamii.

“Naam kwako uliyeteuliwa tangu miaka 43 kuwa Rekta wa Kanisa la Consolata, na kwa ajili ya ibada yenye ari kwa Bikira Maria, wakaaji wa Torino wanakutilia stahili ya kukarabati na kupanua karibu toka msingi jengo hili, sembuse kujitahidi kwa taratibu kulipamba na kazi za sanii na kulifunika na marumaru ya thamani.

“Sifa hiyo yako, ijapo kubwa, inapaswa kuwekwa nyuma, ikilinganishwa na kazi ya kudumu na ya jitihada uliyofanya kwa muda mrefu: kuhusu kutakatifuza roho za watu, na tena kwa kuhifadhi malezi na utakatifu wa mapadre.

“Naam, kwako mara ulipoanza kazi ya huduma takatifu, Mafrateri wa seminari ya Torino walipata mwalimu wa ibada mwenye hekima; na halafu tangu ulipoanza kuwa Rekta wa Kanisa la Consolata ulichukua mwongozo wa Chuo cha Mapadre, hustaajabisha jinsi ulivyoshughulikia kwa ajili ya kuwapa utaaluma na pia fadhila mapadre uliowalea, na hivyo wamehesabiwa mamia na mamia mapadre – na kati yao wengi maaskofu na maaskofu wakuu – ambao wanajivunia kuweza kulelewa nawe kwa maisha yanayostahili watu wa Kanisa... “

Pius XI

*Kwa Jubile ya kipadre*

*Ya Kan. Yosef Allamano*

*Ukurasa 11*

**Baaraka ya Mtakatifu.**

Yosef Allamano alizaliwa Castelnuovo d’Asti (leo Castelnuovo Don Bosco), tarehe 21 Januari 1851: wa nne kati ya watoto watano ambao Mungu aliwapa wanandoa Yosef na Maria Anna Cafasso. Kesho yake kwa njia ya Ubatizo alizaliwa mtoto wa Mungu, wakiwamo baba wa Ubatizo Yosef Ostino, na mama wa Ubatizo Franchiska Cafasso: wote wawili ndugu wa Allamano

Kwa sababu ya kifo cha baba kilichotokea baada ya miaka mitatu, mwongozo wa nyumba na malezi ya watoto yaliangukia mama, dada mstahilivu wa Mt. Yosef Cafasso. “Alikuwa mwenye huruma - wanashuhudia - kwa kila aina ya mahitaji, na mwenye jitihada kwa mema ya wengine” -

“aliwahudumia na kusaidia wagonjwa kwa kila namna” – “alikuwa yeye kutayarisha yaliyohitajika kwa Komunyo pamba katika nyumba ya wagonjwa”. Basi, mwanamke mwenye fadhila kiasi kwamba Paroko mwenyewe, Mtheol. Anton Cinzano, alizoea kuwaambia watoto wake: “Mngepaswa kubusu mahali anapopita mama yenu”.

*Ukurasa 12*

Kwa sababu alipendezwa na Mungu, hakukosa kupata majaribio. Mwaka 1866 ugonjwa wa uti wa mgongo ambao ulianza tangu muda kuashirisha, ulizidi hadi kumzuilia kufanya kazi na hata kumzuilia kujimudu. Kwa muda wa miaka saba , yaani hadi kufa, alibaki katika hali ile, akiketi kwenye kochi, asiyeweza tendo lolote, na kipofu. Walisema: “Hatujawahi kuona kiumbe mwenye magonjwa mengi kiasi hicho”.

Akafa tarehe 15 Desemba 1871. Husimulia, na Allamano mwenyewe alithibitisha, kuwa, saa ya kufa alimwona B. Maria. Naam alijiinua kwa mwamko, na kutabasamu na kutaja jina la B. Maria, na macho yake, vipofu tangu miaka, yalikazia maangavu mahali mbele yake.

Kutoka kwa mama mwenye fadhila kiasi hicho, Yosef alipata malezi ya kwanza. “Aliweza kuwalea wanae vema; – alisisitiza mwenyewe – hakuwa mkali bali mtaratibu kamili, na hasa: utaratibu wa kupanga mambo. Kilichonishitusha daima katika familia ulikuwa mpango uliotawala. Alituvalia mavazi ya wakulima, lakini safi: chakula kilikuwa maskini na isiyozidi. Kaka yake Ottavio kwa upande wake anasimulia kuwa, walipokuwa wadogo, waliwahi kukosa, badala ya kukimbia adhabu ya mama, walimwendea kupiga magoti, kuungama kosa, na kusikiliza makaripio na kulipiza”. Nyongeza nyingine ya udogo wake Yosef ni ushahidi wake wa Placida Gilardi, mpwa wa Mt Cafasso:

*Ukurasa 13*

“Yosef mdogo tangu udogo wake alionyesha tabia tulivu, asiyependa kelele, kama mwanaume mdogo mwenye hekima. Akienda machungani, alichukua kitabu cha shule cha kujisomea”.

Ilikuwa mwaka 1857, akiwa na miaka sita, kwamba alikutana, kwa mara ya kwanza na ya mwisho, na mjomba wake: Padre Yosef Cafasso. Alifika Castelnuovo kwa ajili ya kuwapongeza wanakijiji wenzake kwa kutaka kupinga mafundisho ya Waprotestanti: Maria Anna alimpelekea watoto na kuwaleta mmoja mmoja ili awabariki. Mkutano ule ulitia ishara katika moyo wa Yosef Allamano kama njia mwangavu: ilikuwa kana kwamba alirithi roho yake, utume na fadhila zake.

Miaka sitini baadaye (1925) Cafasso alitangazwa Mwenye Heri. Kanoni Allamano – aliyehimiza mchakato wa kumtangazwa – alipokwenda Castelnuovo, alitaka kurudia kuishi tendo lile la utotoni. Alitaka kiti, na kukiweka mahali pale pale ambapo Padre Cafasso aliketi kupokea heshima ya wapwa wake; kwa sauti ya majonzi alitamka: “Hapa nilipata baraka yake!”.

Halafu mwaka uliofuata, mjomba na mpwa walikutana mbinguni.

*Ukurasa 14*

**Mwalimu na mtume.**

Mtu mwingine alishughulikia kwa dhati katika malezi yake Yosef tangu utotoni: Mwalimu Benedetta Savio, mkuu wa chekechea. Kan. Allamano, jinsi asivyosahau kamwe miaka ile ya utotoni, vile alikumbuka daima na shukrani mema aliyopokea kutoka kwa Mwalimu wake, tena alitaka sana waandike habari za maisha yake. Daima alidumisha uhusiano wa barua naye, na akamtumia kwa ajili ya kufikishia kwake misaada yake kwa maskini wa Castelnuovo.

Katika barua yake kwake, anamwita "mama mlishi wa watoto Yesu wengi". Asingeweza kutoa sifa bora zaidi kwa fadhila na utume wa mama huyo. Don Bosco mwenyewe, alipoanzilisha shirika la Masista wa Maria Msaada wa Wakristo, alimfikiria Benedetta Savio wa kufaa kabisa kama Mama Mkuu wa kwanza. Aliwatuma mapadre wawili Castelnuovo, ili kumhamasisha kuja Torino, lakini hakufaulu. "Mmwambie Don Bosco – akajibu – kuwa ni mapenzi ya Mungu mimi niwe mtawa nyumbani, jinsi alivyonihakikishia mwongozi wangu, Don Cafasso.

Kweli amekuwa mtawa nyumbani. Kama Mkuu wa chekechea, alikuwa mkamilifu kutekeleza wajibu wake;

*Ukurasa 15*

alikuwa na mwendo wa upole na watoto aliwatendea na wema wa kimama. Akijifanya mdogo na wadogo, aliweza kupenyeza mioyoni mwao safi kanuni za msingi za malezi mema, chanzo cha fadhila zile ambazo kwake zilikuwa mwangaza. Aliona shule kama utume, na ya utume alikuwa na ari kuu na roho ya sadaka. "Ni miaka 48 – alimwandikia Allamano karibu na mwisho wa maisha yake – kuwa nafundisha shuleni na kuwamo kati ya watoto, walio marafiki wa Yesu. Sijui nitatoaje hesabu kiasi gani kwa Mungu yule anayeona yote! Sijui kama niliwahi kulima vizuri vichipukizi hivyo, na kama vyote vitapandikizwa katika bustani ya mbinguni! Bora kufa mara elfu kuliko kusababisha upotevu wa kichipukizi hata kimoja kutokana na uzembe na uvivu wangu. Ningegharamia maisha yangu kwa ajili ya roho hizo teule!".

Alikufa mwaka 1896, baada ya miaka hamsini ya utume mtakatifu na wenye matunda, na ukumbusho wake bado leo unabarikiwa na watu wa Castelnuovo.

Familia, shule, kanisa: ndio nyanja tatu za utume, ambazo zinakamilishana kati yao, kwa ajili ya malezi ya watoto na vijana. Na pia, ndio maelezo, tunavyoona, ya mazao ya ajabu ya watakatifu, katika Castelnuovo, katika enzi zile.

*Ukurasa 16*

**Shuleni mwa Mtakatifu mwingine**

Tarehe 17 Oktoba 1860 Yose Allamano alipokea Sakramenti ya Kipa Imara, ya kumfanya kuwa askari hodari wa Kanisa. Bali hatujui tarehe alipokutana na Yesu katika Komunyo ya kwanza; lakini tunajua kuwa yeye alikuwa akisherekea kila mwaka ukumbusho wake na ibada.

Alipomaliza kwa mafanikio shule ya msingi kijijini, kwa muda alisitasita achague lipi. Alipenda masomo, lakini hakutaka kamwe kutengana na mama yake. Alikuwa na upendo sana! Bwana aliingilia kati kwa namna ya pekee.

Siku moja ilitokea kwamba walifika nyumbani mwa Allamano liwali na mwalimu. Katika mazungumzo pamoja na mama, akiwemo Yosef, mmoja wao alitokea kusema:

“Lakini mtoto huyo hammsomeshi?”.

“Kwa upande wangu – alijibu Maria Anna – sina neno, yeye akipenda”.

Kwa maneno hayo Yosef alijikusanya akilia machozi.

“Acha, acha – waliendelea wale wawili – haifai kumwacha kupotea, lazima asome!”

Ndivyo ilivyoamuliwa.

*Ukurasa 17*

Yosef, akiwa na umri ya miaka 11 aliingia katika Oratorio ya Wasalesiani ya Torino kwa masomo ya Middle School. Mwenye akili nyepesi, aliweza kutimiza katika miaka minne masomo ya miaka mitano, akiwa daima wa kwanza wa darasa. Katika mwaka wa tatu alipata mamlaka ya mwangalizi.

Tena hushuhudia bidii yake masomoni, madaftari yake ya miaka ile, kila moja ni kielelezo cha utaratibu na usafi. Aliandika yote na kuyatunza, jambo ambalo kwa mtoto asiyetimiza miaka 15 ni alama ya bidii isiyo ya kawaida. Na kupita wote alimpenda na kumheshimu Don Bosco, mwungamishi wake kwa muda huo wote. Don Bosco, mjuzi wa vijana, angalipenda abaki, na kumhamasisha kujiunga na shirika la Wasalesiani. Lakini haikuwezekana. Kumbe ilitokea kwamba, ili aepe masisitizo zaidi, kijana ameacha Oratorio, bila kuagana.

Muda baadaye, Don Bosco atamkaripia kwa upendo: “Umenikosea sana”... Mbona umeondoka bila hata kunisalimia!”.

Naam, bila kumsalimia Don Bosco, lakini akichukua naye roho yake, na pia shukrani ya kina kwa Mwalimu wake mkuu.

Mungu alikuwa akiongoza matukio kadiri ya malengo yake ya ajabu.

*Ukurasa 18*

**Saa ya Mungu**

Kwa kila roho iliyoteuliwa kuna saa ya uamuzi ambamo kwake hutokea utume wake duniani, na tokea kwake utakatifu wake na basi, utukufu wake baadaye.

Ndivyo ilivyokuwa kwa kijana Allamano.

Bwana, ambaye alitaka kutoka kwake tendo kishujaa la kuitikia kipaji bora cha wito wa upadre, aliruhusu kuwa uzuiliwe kwa muda fulani na kaka zake. Sio kwamba walikataa wito wake, bali wangalipenda Yosef audhurie shule ya sekondari ya serikali, ili, kwa bahati mbaya angepaswa baadaye kuondoka seminarini, asiwe mtu “hohehahe”.

Sababu isiyo na msingi, ya kufaa kwa walio na wasiwasi daima, lakini isiyofaa kamwe hapa, kuhusu wito uliojaribiwa na thabiti. Lazima pia kukubali kuwa shetani, yu daima macho kuzuilia mema, ajaribu kutilia kwatu yake.

Kwa upande mwingine, neema ya Mungu haikubaki tuli, na kwa nguvu yake laini, kijana hakuridhika kamwe kuahirisha kuingia seminarini. La, sivyo, hiyo si namna ya kutumia vipaji vya Mungu! Alitaka kitu kimoja tu: kujua mapenzi ya Mungu ili ayafuate kwa vyovyote.

*Ukurasa 19*

Hali alikuwa akiugua moyoni na kusali.

Na siku moja aliangazwa kutoka juu alivyoomba, na neema ya Mungu ikamwangaza wee! Aliamka ghafla kutoka kwa dawati la kusomea, alitupa mbali vitabu ya masomo ya dunia, akaenda mbele ya kaka zake na: "Bwana ananiita leo... sijui kama ataniita tena baada ya miaka miwili mitatu!"

Mkazo thabiti wa sauti haukuachia nafasi ya kujibu.

Siku ile na mkazo ule zimeamua maisha ya baadaye ya Yosef Allamano katika wakati na hata kwa umilele.

**Mpenzi wa Yesu**

Katika sikukuu ya B. Maria Mzazi wa Mungu – tarehe 11 Oktoba 1866 – Yosef Allamano alipiga hatua ya kwanza katika jeshi la Kanisa, akivaa sare yake; halafu akaingia katika seminari ya Torino.

Alikuwa Rekta mzee kan. Alexander Vogliotti; lakini kwa kweli aliyeongoza seminari alikuwa kan. Yosef Soldati, aliyekuwa Mwongozi wa roho, na ambaye toka mwaka 1875 hadi 1884 alikuwa pia Rekta.

Frateri Allamano hakukawia kushangaza wakubwa na wenzake. "Alikuwa wa kwanza kwa mastahili ya masomo na fadhila" anashuhudia Mons. G. B. Ressia, mwenzie wa masomo, na baadaye askofu wa Mondovì. Na nafasi ya kwanza ya masomo aliishika zaidi kwa nguvu ya utashi, kuliko akili,

*Ukurasa 20*

ijapo ilikuwa ya hali ya juu sana; lakini stahili ilizidi pia kwa sababu ya afya yake isiyo nzuri, na tena kudhoofishwa na ugonjwa aliopata katika mwaka wa kwanza wa seminari.

Jitihada yake ya kwanza: asipoteze nafasi, hata sehemu ndogo, akitumia vema hata dakika zile chache kati ya wakati wa kujisomea na shule darasani, kati ya darasa na darasa. Halafu mwangalifu sana wakati wa mafunzo, ambayo alihudhuria kisha kusoma walau mara moja somo litakalofundishwa; na kutengeneza mafupisho ya masomo muhimu, ambayo yalitunzwa, na kuweka

miniti kwenye vitabu vya masomo. Kati ya makusudi yake, tunapata: "*Nitajifunza na shauku, lakini kwa ajili ya Mungu, ili niokoke na kuziokoa roho za watu*". Programu bora sana toka kwa mseminari: kupenda kusoma kwa nguvu ya shauku, na kuielekeza kwa utukufu wa Mungu peke yake.

Alihifadhi kwa nia kamili nidhamu tokana na tabia na kwa fadhila, asikose sheria yo yote, alizijifunza kwa moyo, akifuata *ad litteram* shauri la Mons. Gastaldi, askofu mkuu wa Torino, aliyeandika sheria zile za seminari. Hatujui kama wengine walifuata mfano wake wakati ule ama hata sasa.

Alikuwa hasa mtu wa maisha ya ndani rohoni, aliyopumua na ilivyoonekana ibada yake. Enzi zile mabaki ya ujansenio, Komunyo ya kila siku ilikuwa nadra hata seminarini. Frat. Allamano alikuwa mmoja kati ya wachache kutekeleza, na kwa sababu ya hofu ya kuonekana angalitaka kuacha, isingekuwa Mwongozi wake wa roho

*Ukurasa 21*

kumtilia moyo:

"Pokea, pokea tu!".

"Lakini wenzangu watasema kuwa nataka kuonekana mwema zaidi...".

"Nawe upokee, ili upate kuwa mwema zaidi".

Na hakubana yote katika dakika zile chache ya Sakramenti ya Komunyo, upendo na umoja na Yesu:

"*Nitagawa siku kati ya shukrani ya Komunyo niliyopokea na matayarisho ya Komunyo inayofuata".*

*"Kila tamaa ya chakula nitaigeuzia kwake Yesu katika Sakramenti, na hivyo kishawishi kitatokeza komunyo ya rohoni".*

*"Mezani nitakazia mawazo kwa mkate wa Ekaristi, nikimwomba Mungu neema ya kwamba chakula cha mwili kisipunguze hamu ya chakula cha roho".*

*"Nitafikiri kula nikishiriki na Familia Takatifu, na kila bonge litagusa kwanza ubavu wa Yesu".*

*"Nataka kutembea mbele ya Mungu, nikitamani kuungana naye, kukimbilia Moyo wa Yesu na hamu, na komunyo za rohoni".*

*"Nitaungana, kadiri iwezekanavyo na Yesu kwa Komunyo, chemchem ya kweli ya utakatifu".*

Makusudi hayo yameandikwa katika kijitabu binafsi, iliyo kama historia ya roho yake.

Akilishwa na chakula hicho cha nguvu, akizima kiu chake kwenye chemchem ya maji ya uzima wa milele, Frat. Allamano alifanya hatua

*Ukurasa 22*

za kupanda mlima wa wateule, na macho kukazia kilele mwangavu ya utakatifu.

*“Padre lazima awe mtakatifu; utakatifu na upadre zinalingana”.*

*“Sitakuwa padre mtakatifu, nisipokuwa mseminari mtakatifu”.*

*“Si kwamba kukaa seminarini kunatufanya watakatifu, bali kufanya mambo yote yapaswayo na jinsi ipasavyo”.*

*“Nataka kushughulikia jambo lililo muhimu: kuwa mtakatifu na sio mwema tu; kufanya sio kungoja”.*

Utashi, basi, kweli thabiti wa kuelekea utakatifu; ukamilifu sio wa maneno, bali wa matendo. Na kwamba imekuwa hivyo, anashuhudia mons. Ressia, tuliyemtaja: “Kila padre ni rafiki wa Yesu. Hakuna shaka kwa upande wa Allamano kuwa hivyo. Tena ningesema kuwa Benyamin wa Yesu (mpenzi wake), yule aliyempenda. Ilikuwa siku chache alivaa vazi la kipadre, na kwa muda wa miaka saba nilishiriki naye na wenzangu wengine wa darasa, shuleni, masomoni, wakati wa kucheza, matembezini, katika ibada ya sala. Yeye alikuwa kielelezo chetu kwa ari katika sala, kwa kupokea mara nyingi, kwa uvumilivu na wema wake nasi, kwa utii, na mwangaza wa fadhila ya kimalaika. Basi, hamna kati yetu aliyeshangaa, kuona kuwa mapema wakubwa walimteua kuhudumia sakristia na altareni; wala kwa kuwa, mwaka wa mwisho wa theolojia, amepewa kazi ya prefekt wa Chapel, yaani kuwa wa kwanza wa waseminari wote. Wote walijua kuwa

*Ukurasa 23*

Allamao alikuwa karibu zaidi na Moyo wa Yesu, na rafiki yake, na hakuna asingeweza kuthubutu kujifananisha naye.

Kiasi hicho cha ari ya fadhila hakikupungua wakati wa likizo, ambalo kwa Allamano lilikuwa kitu kidogo sana. Alikuwa na mama yake mgonjwa na alitumia siku zake karibu naye, kumshughulikia kwa wema na uangalifu, akichukua nafasi ya mtumishi hushika. Hadi mgonjwa aliweza kusikia, alimsomea masomo ya ibada; lakini baadaye, alikuwa yeye kusikiliza mashauri yake ya hekima, akijibu kwa kumgusia mkono. Vile vile alikuwa mkalimani alipokuja paroko kuja kumwungamisha.

Baada ya kifo cha mamake, aliweza kufurahia zaidi, lakini hakuwahi kujitawanya kamwe. Alijiwekea mwongozo, akigawa katika juma masomo ya kujifunza, na pia saa za kusali na kupumzika, na kushika kwa bidii. Watu kadhaa wa Castelnuovo wanakumbuka likizo zake Frat. Allamano: mwenendo wake taratibu, na wa kujikusanya, hadi kuvutia heshima na wema; mwenendo wake kielelezo kanisani na kujikusanya wakati wa ibada. Paroko wake. Theol. G.B. Rossi (atakayekuwa askofu wa Pinerolo, aliyemfuata Cinzano mwaka 1870, alimheshimu sana Frateri na kumpenda kibaba, hata kutaka Jumapili kumwalika mezani naye.

*Ukurasa 24*

**Kilele kuu**

Ikiwa matayarisho kwa Madaraja lazima yaanze mapema tangu miaka ya kwanza ya seminari, hakika yanapaswa kuongezeka yanapokaribia lengo. Frat. Allamano alitambua masharti yake. Miaka baadaye atasema na kurudia bila kuchoka: “*Mjitahidi kujitayarisha mapema. Hakuna*

*matayarisho, hata ya bidii sana, itazidi mno; na wote, kwa kiasi kikubwa au kidogo, siku ya upadirisho watajuta kuwa hawakujitayarisha ya kutosha. Na si shauri la unyenyekevu, lakini, bahati mbaya, ni ukweli*".

Kwamba naye aliona majuto si ya kushangaza; lakini ilikuwa shauri la unyenyekevu. Maana hakuweza kujikaripia. "*Nataka kuwa mtakatifu, sio mwema tu*" aliandika mbele ya makusudi yake alipoingia seminarini. Na alitembea katika njia hiyo bila kusimama, na ari iliyoendelea kuongezeka. Na sasa, alipofikia mwaka wa nne wa Theolojia, tunamwona akielekea kwa nguvu yote ya nia yake.

Utashi, sio dhana tupu. Utashi unaojenga sio kwenye mchanga ya makusudi yasiyo na msingi, bali katika mwamba ya makusudi thabiti, nayo yakilingana na fadhila zilizo za maisha ya upadre. Akijitayarisha kupewa daraja dogo la Kipara na madogo mengine (Mei 21,1872), alikusudia:

*Ukurasa 25*

*Picha*

*Ukurasa 26*

*"Nitajitahidi kuendelea katika roho na hamu ya umaskini".*

*"Nitafanya matendo ya kurudiarudia ya kujitenga na kutoa sadaka ndogo kwa maskini".*

Na akijitayarisha kwa Ushemasi mdogo (Desemba 21,1872):
*"Nataka kutayarisha fadhila safi ya usafi wa moyo kwa ajili ya daraja la Ushemasi mdogo".*

*"Nitafukuza mara, kwa kutaja jina la Yesu na Maria, kila wazo linaloweza kunukia dhidi ya usafi".*

*"Katika matembezi nitafanya matendo mawili ya kunyima macho na tamaa ya chakula".*

*"Kila siku nitantolea usafi wangu B. Maria ili mwenyewe autayarishe. Kila Jumamosi nitaongezea majikatalio mengine zaidi".*

Basi, ni chini ya ulinzi wa B. Maria kuwa Allamano anataka kutembea, ili ajitayarishe kwa Madaraja yajayo. Na tena, kabla ya kupokea Ushemasi mdogo, kana kwamba anataka kuharakisha kujitolea kwake, na ili kuonekana kuwa na tabia ya uhuru zaidi, katika sikukuu ya B. Maria wa Karmeli (Julai 16, 1872) aliweka nadhiri ya usafi wa moyo mikononi na B. Maria, akitumia maneno aliyotunga mwenyewe:
"*Ee Maria, Malkia wa mabikira, mimi, maskini mkosefu, nakutolea kabisa na kuweka wakfu, katika dakika hii, kwa mikono ya Malaika*

*Ukurasa 27*

*na Watakatifu wote, na hasa ya Mt. Yosef mume wako safi kabisa, ya Malaika wangu Mlinzi, na ya*

*Mt. Alois, ubikira wangu, nikikuomba uusafishe na madoa yote niliyoweza kuuchafua; na ukipambwa na weupe wa usafi wako, kumtolea Yesu Mwanao Mungu, ili autunze katika Moyo wake Mtakatifu kabisa.*

*Uniombee neema, ee Maria, ya kuwa jinsi leo unaomtolea Yesu, vivyo, mzima kabisa, kwa mikono yako, niweze kuutolea siku ya hukumu, ili uwe mbinguni nyota katika taji lako...*"

Halafu tena, siku ya kuamkia Ushemasi wake, amejitolea wote kabisa kwa milele kwa Bikira mtakatifu sana: "*Leo, tarehe 25 Machi 1873, sikukuu ya Kupashwa Habari ya Malaika kwa B. Maria Mtakatifu sana, nimemchagua, na natumaini amekubali, kama MAMA YANGU MPENZI SANA. Na ili nipate hasa kushinda kiburi hasa, kwa sababu katika unyenyekevu, kama vile katika usafi wa moyo na upendo wa Mungu, nataka kumwiga. Nitamwita Maria: MAMA YANGU MPENZI SANA katika kila shida na nitakuwa na ibada kwake, kwa kujionyesha mwanae anayestahili, kiasi kinachowezekana zaidi*".

Toka saa hiyo mawazo yake yanaelekea dum daima kilele cha mwisho: na hamu, sala, majikatalio na makusudi, yote anaelekeza kwenye ncha moja: Misa! "*Nataka kushiriki idadi iwezekanayo ya Misa, nikijitahidi kabisa na hamu. Tangu sasa nazishiriki zote kwa nia ya kupata kuziadhimisha kitakatifu*".

*Ukurasa 28*

Wenzake walipata Upadirisho katika sikukuu ya Utatu Mtakatifu (1873). Kumbe yeye, kwa sababu ya umri, alipaswa kukawia hadi tarehe 20 Septemba. Aikingia katika mfungo wa matayarisho, alimwandikia rafiki: "*Najiandalia kujiweka tayari Daraja Takatifu la Upadirisho, sababu ya tamaa nyingi, lengo la miaka mingi ya masomo. Moyo wangu hushikwa na hisia mbili tofauti: hofu ya heshima hiyo kuu ninayojiandaa kupokea, na pia ya kumwamini Mungu kuwa atapenda kutekeleza ndani yangu maajabu aliyotenda katika roho za wengi*".

Alipokea upadirisho katika Kanisa kuu la Torino kwa mkono wa askofu mkuu Gastaldi. Aliimba Misa ya kwanza Castelnuovo, wakati wakiadhimisha sikukuu ya B. Maria wa Mateso

Lakini, tazama, kigezo cha roho ya Allamano. Jinsi matayarisho ya upadirisho yalivyokuwa yote na kiroho pekee, ndivyo na siku ya Misa ya kwanza alivyotaka ipite katika mwungano wa ndani na Mungu wake, asiruhusu kitu kuzuilia. Kwa hiyo: hakuna karamu kuu, hakuna kelele ya kidunia. Mwenyewe aliomba paroko kwamba karamu iwe nyumbani ya paroko, akiwaalika kaka zake tu. Bali alasiri, kisha kumaliza ibada, aliwakusanya mapadre nyumani mwake kwa kinywaji. Hakuna kitu kingine.

*Ukurasa 29*

**Msimamizi wa parokia**

Kisha kuwa Padre, Allamano alishika kwa muda wa miaka mitatu mamlaka ya kuwa Mwangalizi seminarini, akitimisha – full marks na sifa – stashahada ya Theolojia. Wakati huu alizoea kupita kiasi cha likizo Passerano pamoja na mjomba paroko, padre Yohanes Allamano. Agosti 1876, huyo aliugua vibaya sana na mpwa aliitwa haraka sana karibu na mgonjwa. Alifika

wakati wanaposali sala za waazimia. Zaidi, padre aliyehusika, katika bidii yake, alikuwa akisukumana bila kuchoka na sala fupi, na tafakari, ambazo, kwa kuwa mno, ziliishia kumchosha zaidi udhaifu wa mgonjwa mahututi. Basi, huyo alipomwona mpwa wake karibu, alimwambia (kilugha) na sauti hafifu iliyobaki:
"Mwondoe huyo mchokozi!".

Kan. Allamano alikuwa akisimulia mara nyingi kisa hicho, na akitabasamu kwa maneno ya mzimia, alikuwa akifafanua: "*Mnaona?... Haifai kuwachosha wanaokufa na maneno mengi, kwa sababu, mbali ya kuwasaidia, kuna hatari ya kuwahimiza kukosa uvumilivu. Naam, tuseme mara kwa mara sala fupi kwa kumwelekea mgonjwa, lakini halafu tuwaachie kutulia. Bali, tuseme sisi wenyewe sala, hata mgonjwa aweze kusikia, ambaye ataweza kushiriki, bila kuchoka mno*".

*Ukurasa 30*

Padre Yohanes Allamano alikufa tarehe 21 Agosti, akiwa na umri ya miaka 76, baada ya miaka 35 ya kuwa paroko. Katika wasia alimwacha mpwa mrithi wake. "*Ilinishtusha sana* – alikuwa akisema baadaye kan. Allamano – *kwa kuwa sikuambiwa neno hata mara moja kuwa alikuwa na nia hiyo*". Ulikuwa Mwongozo wa Mungu uliotengeneza mambo kuelekea kazi kubwa ambayo Allamano ataanzilisha.

Kisha kufariki mjomba, Allamano alipewa amri ya kubaki Passerano hadi atakapoletwa padri kumbadili. Alibaki miezi mitatu, na wakati huo alipata nafasi ya kuangaza huruma yake kwa kila aina ya wahitaji, licha ya ari yake isiyochoka ya kiuchungaji. "Alikuwa mwembamba kama kijiti – wanasema mashahidi - alionekana asiweze hata kusimama wima, lakini alipatikana kila mahali, na kuwa tayari kwa yote yale". Tunashika bado maandiko ya mafundisho yake aliyofundisha katika vijiji vya kandokando, aliyoandika toka mwanzo mpaka mwisho kwa kilugha. Jiwe la ukumbusho, lililomo pale kanisani, hukumbusha jitihada yake na ukarimu wake mintarafu kushughulikia heshima ya Nyumba ya Mungu.

Basi, aliweza katika muda mfupi hivyo, kujivutia heshima na upendo wa watu, waliotaka awe paroko wao, na amekuwa Msharifu mwenyewe Alois Radicati wa Passerano kuwa mjumbe wao kwa Askofu mkuu, kumpelekea matakwa ya watu. Matakwa ambayo hayakusikilizwa kwa

*Ukurasa 31*

kwa sababu alikwisha kumchagua Allamano kwa wadhifa nyingine.

Onyesho hilo, ijapo fupi sana, ya huduma parokiani, lilikumbukwa daima na Allamano, na hisia ya shukrani sana kwa Bwana, kwa sababu ya faida aliyopata: kwa ajili yake binafsi, na kwa ajili ya malezi ya mapadre vijana.

**Kiongozi wa roho**

Kisha kupita miezi mitatu, mwanzo wa Novemba. Mtheol. Allamano alikwenda seminarini,

alimosikia kuchaguliwa kwake kuwa Baba wa roho. Askofu Gastaldi alipomjulisha , yeye hakuweza kuzuia tamko la mshangao na kushtuka:
“Monsinyori, unasemaje!?”.

“Naam. Nimekuweka kuwa Baba wa roho seminarini Torino; una matatizo?”.

“Lakini, ona... nia yangu ilikuwa kwenda msaidizi, halafu paroko katika kijiji fulani”.

“Unataka kuwa paroko? Basi, nakupa parokia muhimu katika Jimbo”.

“Lakini Monsinyori, mimi ni kijana sana...”.

“Ah! Ujana ni kasoro linalopotea polepole; halafu wanakupenda”.

“Basi, Monsinyori, unibariki”.

Alishika wadhifa siku ile ile, bila sherehe yo yote au

*Ukurasa 32*

malalamiko, ijapo analemewa na uzito wa madaraka. Alifuta kila shughuli, wala kupokea mengine; hivyo tena, katika miaka minne ya kuongoza, hakujiruhusu kuondoka seminarini hata saa moja wakati waseminari wamo chini ya uangalizi wake. Hupaswa kudhihirisha kuwa nyakati zile, Kiongozi wa roho alikuwa akiangalia pia na utekelezaji wa nidhamu.

Mfumo aliotumia na aliofuata baadaye kila wakati katika malezi ya vijana watumishi wa Kanisa, ulikuwa ule wa *fortiter et suaviter*: kamwe kuacha kupita kosa lo lote bila kulisahihisha, walau kadiri unavyoruhusu utaratibu; lakini kusahihisha kwa wema na heshima. Walau alizidi kwa wema. Nalo limekuwa baraka ya Mungu, kwa sababu aliweza kutuliza ari iliyozidi, pamoja na tabia ya mlipuko wa Rekta, kan. Soldati, ambaye kwa upande mwingine alikuwa padre kielelezo na mkubwa bora sana. Huyo alikuwa baba mkali, Allamano alikuwa mama mwenye huruma. Na ulikuwako usemi kati ya waseminari, wakidokeza hawa wawili: “*Justitia et pax osculatae sunt!*” (Haki na amani zimebusiana).

Alikuwa akiwapokea waseminari walipoingia, kwa namna ya kupendeza sana. Akiwa na utaratibu sana kujimudu, lakini alipenda furaha, akishiriki mazungumzo yao. Aliandika katika kijitabu majina yao, na mara kwa mara alikuwa akitafakari juu yao, akiona fulani ambaye hajaongea naye kipekee, alitafuta njia ya kumsogea, hata wakati wa starehe. Aliangalia kuwa mezani kisikose kitu; na kwa wagonjwa

*Ukurasa 33*

alikuwa anawajali namna ya pekee. Alikuwa na heshima kubwa kwa wakubwa chini yake, na hakuwahi kuonyesha chukio kwao mbele ya mafrateri, ijapo waliwahi kukosa wajibu wao.

Toka uso wake mfurahivu huonekana utulivu wa roho usiobadilika kamwe. Hutambulikana kama mtu aliyevuliwa na ubinafsi, ili aishi tu kwa ajili ya mafrateri, kujifanya wote kwa wote. Hakuna alama ya kipolisi, ya kichokozi au kizito katika kiongozi chake. Akidumu daima katika usawa, daima katika amani, alihifadhi daima kandokando yake utaratibu, na nidhamu laini na ya kupendeza.

Sio kwamba hakujali. Bali ilikuwa rahisi kutambua jinsi alivyougua kuona, kwa upande wa wengine kasoro la roho ya kikanisa. Hapo hakuweza kuvumilia, lakini bila kukasirika kamwe; alijiruhusu kumwonya mkosaji kwa nafasi, hata kuahirisha hadi mwezi mmoja, akitarajia nafasi ya kufaa ili kupata matokeo mazuri zaidi. Jinsi alivyoweza, ikitakiwa kubadili huruma na ukali, hadi kufikia kuwafukuza mara moja wakosaji, kama ilivyotokea safari moja kuwa waliondoka watano mpigo mmoja.

Kazi muhimu ya Kiongozi wa roho, lakini ilikuwa malezi ya kiroho ya mafrateri, ambayo Allamano alishughulikia hadharani na faraghani. Aliongea mara nyingi na mafrateri, katika kikanisa, na maonyo ya kifamilia, kwa moyo, yenye mpako wa kiroho yaliyoingia rohoni na kuwa tunda la utakatifu. Naam juu yake wanafunzi wa zamani wanaongea na shangwe inayogusa, wakichora

*Ukurasa 34*

“sura yake ya heshima, na sharifu”, wakikazia “elimu pana ya kitheolojia na mang’amuzi makuu katika mambo ya kiroho”, na kusifu fadhila

“Alikuwa asiweze kukosolewa katika yote”.

“Hakuna kati yetu aliyeweza kukosoa neno”.

“Sura yake tu ilidai heshima na utauwa; ilitosha kuona macho yake kutambua wema wake”.

“Sisi tulidhani kuwa alitunza safi kanzu yake ya ubatizo, kana kwamba hakuwa na habari ya dhambi”.

“Alikuwa na chapa ya ibada ya kweli bila unafiki, ibada ya kudumu bila kuyumbayumba”.

“Utauwa kwake ulikuwa kama vazi, jinsi ilivyokuwa kawaida kwake roho ya sala na mwungano na Mungu”.

“Mons. Gastaldi alirudia mara nyingi kusema usemi: *si sapiens es doce nos, si prudens es rege nos, si sanctus es ora pro nobis* (ukiwa mwenye hekima uufundishe, ukiwa mwenye busara, utuongoze, ukiwa mtakatifu utuombee). Usemi huo Allamano alitekeleza katika sehemu zake zote. Yeye alikuwa *sapiens*, *prudens*, na hasa *sanctus*”.

Haishangazi kuwa wote walimpenda, hadi kupatana wote kumpendeza kwa vyo vyote; na kuwa na imani kubwa kwake. Chumba chake kilikuwa na hadhara daima. Aliwapokea mafrateri kwa uungwana, hata kwa heshima na kuwapa nafasi pana ya kuongea huru. Alikuwa na kutambua ghafla kwa hakika, na kupenya rohoni, kufunua donda, na kutanguliza sababu ya kumwendea.

*Ukurasa 35*

Toka chumba chake kila mmoja aliondoka akiridhika, ametulia, tayari kufuata mashauri yake, ili kushinda matatizo mengi ya miaka ya kwanza ya seminari.

“Ijapo imepita karibu miaka hamsini tangu wakati ule – anaandika kan. Silvio Marchetti – nakumbuka vema sana sura ya kan. Allamano: shwari, tulivu, stahifu. Sura iliyodai heshima, wala haikupunguza imani kwake. Ningesema zaidi kuwa imani hiyo ilikuwa huru, kwa sababu pia ya

tabasamu ya daima usoni mwake wa kibaba. Alijimudu kama mtu mstahifu lakini alipendeza; mwenye heshima katika mwenendo wake, lakini hakuna ukali. Elimu yake ya kitheolojia na, ningesema, mwangaza wa hali ya kiroho uliomdhihirisha, ilisisitiza kumwendea na urafiki wenye heshima, na imani bila mashaka, tukiwa na hakika kabisa kuwa tungepata mashauri ya busara na makomavu...".

Uthibiti maarufu ya hekima ya Allamano tuliona katika hiyo: kwamba mafrateri walioongozwa naye na kufikia Upadirisho, hata mmoja aliweza kumsumbua Askofu wake, bali wote walitekeleza wadhifa zao kwa utukufu, wakiridhisha wakubwa wao na kwa manufaa ya roho za watu.

Jinsi gani yangetokea mema kwa ajili ya ulimwengu, ingekuwa hivyo katika seminari zote!

*Ukurasa 36*

**Dakta Mshiriki**

Katika mwaka wa kwanza wa Mwongozo wake wa kiroho (1876-1877), Allamano alipata kushirikishwa na Fani ya Kipapa ya Theolojia. Lilikuwa Shirika lenyewe kumwalika kushindana kupata nafasi iliyokuwa wazi. Akijua kuwa litampendeza Askofu Mkuu alikubali na kuanza kujitayarisha na bidii ya kawaida, akipunguza saa za usingizi usiku.
Mitihani ilikuwa miwili: mmoja faraghani, na wa pili hadharani.

Mtihani faraghani ulichukua majaribio mawili. La kwanza, kutetea Thesis (tasnifu) aliyojulishwa siku tatu kabla, bila kujua mabishano yatakayomngojea. Utetezi ulidumu saa moja mbele ya Maprofesa na Halmashauri ya Fani. – La pili, kutoa 'lecture' ya nusu saa, kuhusu tasnifu iliyochaguliwa nusu saa kabla. Alipaswa kuongea kuhusu 'pantheismi'.

Bali katika mtihani hadharani mabishano yalidumu saa tatu, kwa lugha ya Kilatini, kutetea tasnifu sita zilizochaguliwa katika Theolojia ya Maadili nzima. Ya nadharia na kibiblia, dhidi ya mabishi kutoka kwa Madakta sita waliochagulia na bahati nasibu, ili kumjaribu. Pamoja nao. Katika mtihani wa Allamano, alijiunga Askofu mkuu mwenyewe.

Aidha, aliyechaguliwa kwa mtihani wa hadhara ya ushirikiano,

Ukurasa 37

alipaswa kutangaza hoja ya kitheolojia kama onyesho la ujuzi wake, akichagua mada kwa hiari yake. Aliyochagua Allamano na kuimudu ilikuwa: De admirabili Filii Incarnatione. (Kuhusu Umwilisho wa ajabu wa Mwana).

Washindani walikuwa wawili: Mtheol. Allamano na Mtheol. Paschetta. "Nina hakika kuwa Paschetta alisema vizuri zaidi kuliko mimi" alikiri Allamano kwa unyenyekevu. Linaliojulikana ni kuwa Mons. Gastaldi, akiwa Chancellor Mkuu wa Fani ya Kitheolojia, aliamua uchaguzi, ambao ulimwangukia Allamano, kwa sababu ya umri.

**Mtengenezaji (Ukarabati) na Rekta wa Chuo cha Mapadre**

*(Chuo cha Mapadre kilikuwa na lengo la kuzoeza mapadre vijana, mara walipotoka seminarini, kwa kazi ya huduma, hasa kwa kitubio, kwa muda ya miaka miwili ya Maadili zoezi)*

Mwezi Septemba 1880 Mtheol. Allamano aliteuliwa kuwa Rekta wa Kanisa la Consolata. Kwa mamlaka aliyopewa kutoka kwa askofu mkuu, alimchagua kumsaidia, kwa jina la Makamu Rekta, Mtheol. Yakobo Camisassa: yule ambaye leo tunayemheshimu kama mwanzilishi msaidizi wa Misioni za Consolata.

Baada ya kufunga Chuo cha mapadre – iliyotokea miaka miwili kabla, kwa amri ya Askofu mkuu Mons. Gastaldi, kwa sababu ya mizozano ya kielimu na za kinidhamu –

*Ukurasa 38*

ilibaki katika konventi ya Consolata, *Nyumba ya mapadre wazee*: taasisi takatifu kinadharia, lakini kwa kweli isiyowezekana kujiendeleza. Alipofika Allamano, ilikuwa karibu kufifia, na mwaka 1982 ilibaki na mtu mmoja, na tena mpungwani. Alidhihirisha kitisho kwa vyembe vya magonjwa. Hakuguza pesa isipokuwa na mguu wa paka, na akiguswa na mtu, alikwenda mara kujisafisha na dawa. Kwa kufa kwake, yote yalikwisha, hasa mahangaiko yaliyodumu miaka miwili kwa Allamano, aliyetumia saburi ya ajabu, na imekuwa basi.

Basi, taasisi hiyo ilipokuwa inakwisha walikuwa wakiona sana umuhimu wa kurudisha Chuo cha mapadre pale Consolata: kwa ajili ya huduma katika Kanisa, ambalo limekwisha kupata uhai mpya, na pia kwa ajili ya malezi ya mapadre vijana wenyewe. Lakini ililazimu kupata mtu aliyeweza kusimama mbele na ushujaa wa kitume, na kama mwombezi kati ya Askofu mkuu na makleri; na alipaswa kuwa mtu aliyeaminika, asiye na matatizo ya mambo yaliyotokea ya kusikitisha, na mwenye uwezo wa kuaminika kwa mambo ya baadaye kuhusu mwendo mzuri wa Chuo.

Mtu wa aina hiyo alikuwa Mtheol. Allamano.

Mwezi Juni 1882, basi, kwa kusudi hilo, alimwandikia barua ndefu Mons. Gastaldi. Naye akiguswa, na akitambua umuhimu wa sababu zilizotolewa, alikubali kufungulia Chuo pale Consolata,

*Ukurasa 39*

kwa sharti moja pekee na ya lazima kabisa: kuwa Allamano mwenyewe achukue madaraka ya kuongoza mazungumzo ya Maadili.

“Ama sharti hilo – alimwambia askofu mkuu – ama tusirudie tena kujadili jambo hilo”.

Kwa upendo wa mapadre vijana, baada ya kusali na kuomba ushauri, Allamano akakubali sharti lile gumu, lililo kinyume na maelekeo yake, na kushinda nguvu yake kiasi kikubwa.

“Monsinyori – alisema na ushujaa wazi kwa Askofu mkuu, akieleza uamuzi wake - napokea shule, lakini sitatumia vitabu vyako”.

“Haidhuru, fanya unavyotaka, nakuamini”.

*(Aliviona vile vitabu vyenye makasoro na visivyokamilika; na kwa sababu mwandishi alikosa muda tosha kwa ajili ya taaluma kama hizo).*

Akashika wadhifa ya kufundisha Maadili hadi, alipochaguliwa kard. Alomonda kuwa Askofu mkuu wa Torino (1883), na kurudishiwa Chuoni mwalimu maarufu na mzee Mons. G. B. Bertagna, mwanakijiji mwenzake na rafiki mkuu wa Allamano.

Hatusemi neno kuhusu maendeleo ya Chuo na kazi aliyotenda Allamano katika miaka 44 ya kuwa Rekta; tungepaswa kurudia kuandika yote yaliyosemwa kuhusu mjomba wake mtakatifu. Lazima kulidokeza jambo moja tu, kwamba: alikipenda Chuo, na alikipenda hadi mwisho, hata kuachia, katika urithi wake, maandiko yote na vitu vitakatifu vya thamani vya Mt. Cafasso.

*Ukurasa 40*

Na jinsi aliyokipenda, ndivyo alivyokishughulikia na uangalifu wa kibaba. Na ikiwa hakuweza kujitolea kwa ajili yake peke yake kwa sababu ya mengine mengi, aliweza kukitilia chapa yake pekee, na matokeo ya kuridhisha sana.

Ilipotokea kuwa kwa sababu ya lundo la kazi na mahangaiko kuhusu kuongoza Chuo na ukarabati wa Kanisa, uliongezeka uzito wa uanzilishi wa Shirika la Misioni, Allamano kwa tendo la busara na kibali ya askofu mkuu, aligawa madaraka akimwita kumsaidia Mkurugenzi mmoja, ambaye alikabidhiwa nidhamu na malezi binafsi ya wanachuo, alishika mwenyewe mwongozo wa jumla wa Chuo. Uchaguzi aliofanya wa kan. Alois Boccardo kama Mkurugenzi wa kwanza, lazima tuihesabu kama sifa kuu ya Allamano kwa manufaa ya mapadre vijana.

*(Kan. Alois Boccardo anajulikana katika Italia nzima kwa vitabu vyake vya Mwongozo wa kiroho. Alikufa na sifa ya mtakatifu tarehe 9 Mei 1936, na umri wa miaka 75. – Alitangazwa Mwenye Heri mwaka 2007)-.*

Alimpa mkurugenzi miongozo ya kufuata, na alitaka mwenyewe amtaarifu kinaganaga kila kitu, akijichukulia mambo yasiyopendeza, kama masahihisho na makaripio mazito zaidi. Akiongea hadharani ila mara chache, akimwachia kazi hiyo Mkurugenzi; lakini mwendo wa jumla wa Chuo alikuwa anauangalia daima kwa bidii. Ni kweli kwamba Allamano, ijapo kando, aliwajua wanachuo kwa kina, hadi kwamba mwisho wa miaka miwili, walipotumwa kazini,

*Ukurasa 41*

*Picha*

*Ukurasa 42*

aliweza bila hofu kushauri mahali pa kufaa kadiri ya tabia yao, uwezo na maarifa; jambo ambalo lilikuwa linaamsha mshangao kati ya wanachuo wenyewe.

Mema aliyotenda Allamano akiwa Rekta wa Chuo cha mapadre, hayawezi kujulikana hapa duniani ila kwa sehemu tu: kwa sababu yameandikwa moyoni mwa mtu na kung’aa katika matendo ya wale waliokuwa na heri ya kulelewa katika roho ya kipadre kwa mfano wa fadhila zake. “Ni

jeshi la mapadre . anaandika Mons. Pella askofu wa Casale – ambao, kisha tawanyika kaitika Pidmont yote wanapeleka popote nuru ya elimu na ari ya upendo"; kwa kudumisha hai mapokeo ya makleri wale wa Pidmont, yaliyolipa Kanisa wengi watakatifu na taasisi takatifu.

Ni wale, ambao leo wanapaza sauti kama kundi la sauti moja ya shukrani na mshangao kwa Mwalimu na Padre wao aliyewaaga:

"Aliheshimiwa na wote".
"Wakisema juu yake, ilikuwa na utauwa".

"Alikuwa mmoja wa watu wale ambao zaidi wanavyojulikana, zaidi wanaheshimiwa".

"Alikuwa wa ajabu hasa kwa maelekeo yake salama katika kuongoza mapadre vijana".

"alikuwa na vipaji vyote vya mlezi bora wa makleri na vipaji hivyo vilivuta mioyo".

"Alikuwa *vir sapiens* (mtu mwenye hekima) katika mantiki halisi; akiwafahamu mapadre vijana *intus et in cute* (ndani kwa kina)"

"Alitambulikana kama mtu wa kupita wengine kwa akili, kwa kuongoza na kwa fadhila".

*Ukurasa 43*

Lakini sifa inayopita kila sifa, ni ile aliyosema juu yake na Baba Mtakatifu Pius XI, katika Breve (barua) aliyotumia kwa Jubile yake ya kipadre, tuliyoandika mwanzoni wa kitabu.

**Rekta wa Kanisa la Consolata**

Allamano alipoingia kama Rekta, Kanisa la Consolata lilichakaa sana hadi kuitwa: *la travà d'la Consolaa* (banda chakavu la Consolata). Na hakuna fedha.
"Nakupelekea Consolata – alimwambia Mons. Gastaldi - lakini ujue kwamba hakuna kitu cha kuwezesha kufikia mwisho wa mwaka".

Na Rekta baada ya siku chache alihakikisha: "Monsinyori, sio kuweza kufikia mwisho wa mwaka, lakini hata ya kuweza kuanza".

Na hayo yote, baada ya miaka mitano tu (1885) aliwahi kutumia katika kukarabati nje ya kanisa zaidi ya Lira 125 elfu! Halafu, mwaka 1899, alianza kazi ya ajabu ya kushangaza, kupanua kanisa lenyewe, halafu kurembesha nje yake. Alipoelezea Count Ceppi dhana yake, yule mkandarasi maarufu akashituka:
"Lakini wewe unataka mwujiza!".

"Basi – akajibu Mtu wa Mungu – mwujiza utatendeka".

*Ukurasa 44*

"Lakini umefikiri kwamba milioni haitoshi?".

"Isipotosha milioni moja, tutatumia mbili na kiasi kinachotakiwa, lakini Mji wa Torino unapaswa

kuwa na Kanisa linalomstahili Msimamizi wake".

Naam, gharama ilipita milioni, na milioni ikafika. Imekuja hivi kwa hiari, kwa njia ya sadaka ya watu wa kawaida. Jinsi zilivyofika, katika mwezi mmoja tu, lulu 759 na mawe ya thamani kuu, ya kweli na ya thamani kuu, kwa ajili ya taji la mtoto Yesu na la B. Maria. Kama vile ilifanikiwa michango kwa ajili ya nguzo za marimari  na ya sakafu mpya, nayo ya marimari. Na leo kanisa la Consolata linang'aa la dhahabu na marimari, ni kumbukumbu ya sanaa na ya imani, inayoustahili mji mkuu wa Pidmont.

Kwa wakati anaorembesha Kanisa la mawe, Allamano alijitahidi kwa kubuni mapya kwa ajili ya kuamsha moyoni mwa watu ibada ya B. Maria Consolata. Tutagusa ibada ya Sabato tisa za matayarisho ya sikukuu ya mwaka, na ibada ya Sabato za Kwaresima, na Majitoleo ya nyumba kwa B. Maria Consolata, kuanzisha sekta mpya ya Jumuia ya Consolata, kuanzisha Kigazeti "La Consolata", kilichoanza kuchapwa mwaka 1899, na kuwa kati ya vya kwanza vya aina hiyyo.

(Baadaye kigazeti kikagawiwa hivyo: "*Il Santuario della Consolata*" (Kanisa la Consolata) kwa niaba ya Kanisa lenyewe; - na "*Le Missioni della Consolata*"  kwa ajili ya shirika la Consolata kwa Misioni ya nje – Corso Ferrucci,  14- 10138 Torino).

*Ukurasa 45*

Lakini hasa ni kwa njia ya mwenendo mwema wa Kanisa na heshima ya ibada ya dini, kwamba ibada kwa B. Maria Consolata ilifikia wakati wa miaka 46 ya Allamano kuwa Rekta, kuwa kipindi cha dhahabu. Na tazama, Misa kila saa, toka asubuhi mapema hadi saa sita; - mapadri waungamishi kwa hesabu ya kutosha ya kuweza kuridhisha watu kila saa ya msongamano kuwa tayari kitubioni kuwasubiri watu; - Komunyo takatifu iligawiwa kwa waamini kila wakati; - matendo ya ibada kutekelezwa kikamilifu; - usafi kutekelezwa hadi kiasi cha kuchukiza; - katika sakristia awemo padre mmoja kwa zamu, toka asubuhi hadi jioni tayari kuwapokea waamini; - halafu kupanga kila kitu vizuri (hakuna ovyo), na kufuata orodha ya wakati kikamilifu bila kuchelewa, kama ilivyopangwa; halafu tena, na hasa, sala na utakatifu wa maisha.

Watu wema wanaofuata harufu ya fadhila kama nyuki wanaotamani maua yenye mnukio, hawakukawia kutambua kuwa mambo Kanisani yalikwenda vema, na kuwa kuongoza alikuwako Mtu wa Mungu kweli, waliongezeka idadi siku hadi siku. Inatosha kukumbusha sherehe za miaka mia mwaka 1904, zilizoonyesha onyesho la kushangaza ya kuchanua kwa ibada ya B. Maria Consolata; - na mfululizo wa ibada za pekee zilizozidi kiasi kikubwa; - na idadi ya Komunyo Takatifu miguuni pa B. Maria zilizofikia kupita 200 elfu kwa mwaka.

Ibada ya B. Maria iliamka kiasi kikubwa ajabu.

*Ukurasa 46*

Kanisa la Consolata limekuwa kiini cha ibada ya kila siku, hazina ya kutamaniwa, utukufu safi zaidi wa watu wote. Ming'ao miwili, ya dhahabu na ya ibada, iliunganika kama wimbo wa kudumu kwa yule anayekaa kukugawia neema kwa ukarimu.

**"La, Sivyo" ya mtu mtakatifu**

Haiwezi kushangaza ikiwa shetani alisogelea mbele kuzuilia mema hayo yote kwa faida ya roho. Ikatokea kwamba kard. Alimonda, kufuatana na taarifa za wongo, huenda kwa nia ya kumwondoa Allamano kutoka katika Kanisa la Consolata, alidai kuona vitabu vya uhasibu aone urari wa hesabu. Kwake mtu wa ukamilifu na haki na hisia kama kan. Allamano, na baada ya yote aliyofanya kwa ajili ya kanisa la B. Maria, limekuwa jambo la kudhuru sana. Aliumia vibaya sana, hadi kutapika damu; lakini alibaki mtulivu na shwari, akiweka matumaini yake yote kwa Mungu na B. Maria.

Alimpelekea Askofu mkuu vitabu, alivyoshika daima taratibu kamili, na kufuatisha barua ya heshima sana. Lakini kard. Alimonda, alibadili mara shauri, na kumrudishia na hakuongeza tena neno.

Lakini Allamano, baada ya tendo hilo la kutoaminika, alionelea vema kujiudhuru kutoka kwa madaraka, na angalifanya hivyo, isingalitokea kujiweka kati kwa B. Maria kuzuilia utekelezaji. Naam, wakati alipokuwa akienda uaskofuni, tazama, anakutana

*Ukurasa 47*

na P. Carpignano, Padre wa Oratorio, mwungamishi wake na mwenye sifa ya utakatifu, ambaye, akitambua usoni mwale mahangaiko, akamwuliza anataka kwenda wapi. Kisha kuambiwa:

“La, sivyo – anatamka kwa amri – usiende, hata!”.

Na akamshika na kwenda pamoja wakizungumza, hadi kufikia kanisa la Mt. Filipo. Walipoachana, Allamano mtulivu akashika njia kwenda Consolata.

Kard. Alimonda, siku alipofariki kan. Soldati, akampa madaraka ya Mkubwa wa Masista wa Mt. Yosef. Akisisitiza akubali, walau kwa mwaka mmoja, Rekta akatii. Lakini, baada ya mwaka kupita, mara alimwendea Askofu kurudisha mamlaka.

“Hapana – alitamka Alimonda – mambo yanakwenda vizuri mno, endelea tu”.

Halafu akimkumbatia:

“Ah, nilidanganywa juu yako!”.

**Nguvu ya baraka ya Allamano**

Mbele ya upendo mkuu kiasi hicho cha mwana, haukukosa ukarimu mkuu wema wa Mama wa faraja. Neema walizopokea wenye ibada kwa Consolata, tukitazama zile ziliopelekwa kwenye sakristia ya Kanisa la Consolata, zilifikia kwa muda mfupi, kiasi cha tano elfu kwa mwaka. Nyingi za neema hizo zilipatikana pia kwa njia ya sala za Rekta, ambaye walimwendea kama mweka hazina ya B. Maria Consolata!

*Ukurasa 48*

Tukumbuke kwa namna ya pekee kuponywa na kifafa kwa kijana, mtoto wa familia sharifu

wa Torino. Mapigo ya ugonjwa zilizidi sana, hadi mtoto alipaswa kubaki nyumbani. Mama yake, na uchungu sana, alifikiri kumwendea Allamano, ambaye alimshauri sala ya siku tatu kwa B. Maria Consolata, na halafu kumpelekea mtoto kwake. Alipopelekewa alisali sala kadhaa, halafu akambariki. Toka saa ile ugonjwa ukatoweka hata haukuonekana alama yake.

Inastahili kukumbukwa kuponwa kwa kijana aliyepokelewa miaka mitatu katika hospitali ya TB. Jambo lilitokea mwaka 1923 na ndivyo anavyosimulia mama yake aliyepewa neema: "Binamu alinishauri nimwendee kan. Allamano. Nikaenda kwa shida, jinsi sikuwa na imani. Mara nilipofika mbele yake, nikaangusha machozi. Aliongea binamu kwa niaba yangu. Mimi nilikuwa nikimtazama Kanoni na kungoja kwa majonzi jibu lake. Sitasahau kamwe uso wake uliojikusanya, macho yaelekea mbinguni kama akisali. Aliniuliza mwana alikuwa katika hospitali gani. Alijikusanya tena kitambo, halafu kwa tamko la furaha na kwa sauti:
"Ah, lakini mwanao amepona, amepona! Umwondoe mara toka hospitalini!"

"Wakati alipoongea, matumaini makubwa yakawaka moyoni mwangu".

"Nendeni – aliongeza - kusikiliza Misa moja ya shukrani altareni ya Consolata, nawe umwombee roho ya mwanao, naam, sali sana!".

*Ukurasa 49*

"Mara nilipofika nyumbani nikamwandikia mwanangu na siku kumi na tano baadaye alikuwa nyumbani mzima kabisa, hata aliweza kuoa na hakupata tena ugonjwa wo wote kamwe".

Hapo mbele yetu tuna historia aliyoandika mwenyewe msichana maskini ambaye, asiye na mazoea ya maisha, na asiyefikiri matokeo ya mwenendo wake, aliishi kinyumba miaka mitatu na yule aliyejidai kuwa mchumba wake, ambaye hakuwa na wazo la kumwoa, hata kwa sababu ya upinzani wa wazazi. Siku moja, akizungukazunguka Torino amekata tamaa, na kufikiria mabaya moyoni mwake, bila kujitambua, na asijue namna gani, alijikuta mbele ya kanisa la Consolata. "Mara – anaandika – nilipata mvuto wa kuingia, halafu nikavutwa kujitupa kwenye kitubio, na baadaye nilikuja kujua kuwa kilikuwa cha kan. Allamano. Nikamfungulia moyo wangu, naye akanifariji, na kunishauri kusali, akasema kuwa atanikumbuka katika Misa ya kesho yake, akanibariki. Nikasimama nimegeuka, na kama kuzaliwa upya kwa maisha mapya. Kesho yake, niliporudi nyumbani pa mchumba, nilimpata yeye na wazazi wake wamebadilika kwangu, kiasi kwamba wenyewe walishauri kurekebisha hali yangu; tukafanya na sasa tunaishi tukiwa na heri".

Katika kumbukumbu ya monasteri ya Maamkio, tunasoma habari za mnovisi ambaye, kabla ya kuweka nadhiri kuu, alikuwa anashikwa daima

*Ukurasa 50*

na maumivu ya kichwa. Kan. Allamano wakati ule alikuwa Mkubwa, baada ya kumtilia moyo, akampa baraka, akaongeza shauri la kunusa tumbako kwa muda fulani, jambo lililomchukiza sana. Lakini akakubali kwa siku kadhaa, na tangu wakati ule maumivu ya kichwa yakatoweka daima.

Padre Sandrone (Mmisionari wa Consolata), alipokuwa tayari kuondoka kwenda misionini, alimwaminisha kan. Allamano mahangaiko yake, kwa sababu ya marudiorudio ya homa ya malaria,

aliyopata akiwa jeshini Albania wakati wa vita kuu ya kwanza.
“Tulia – akamwambia Rekta – nakupa baraka, nitasali kwa ajili yako na utaona kuwa homa zitaondoka”.

Ndivyo ilivyokuwa. Safari ya mwisho ya kuumwa ilikuwa usiku wa kutangulia safari; halafu basi.

Mtu maskini, ambaye waganga walimshauri kuondoka katika familia yake asiwaambukize, kan. Allamano alimwambia: “Umwamini B. Maria Consolata, atakupa neema”. Na hapo akambariki. Siku mbili baadaye, alikuwa amepona; na, baada ya miaka thelathini aliweza kushuhudia kuwa na afya njema muda wote.

Kan. Marchino anakumbuka kuwa, alipokuwa Frateri, akimkabidhi Allamano shangazi mgonjwa, alijibiwa:
“Uwe na imani; kesho nitamwombea na kumbariki katika Misa”.

Kesho yake shangazi alikuwa ametoka hatarini, na siku chache baadaye alipona kabisa.

*Ukurasa 51*

**Kupunga pepo aliyepagawa**

Tukio limetokea miaka ya kwanza Allamano alipokuwa Consolata. Mwanamke kijana aliyedhaniwa kuwa amepagawa na pepo, alipelekwa Torino; na Askofu Gastaldi aliwashauri ndugu zake kumpelekea Consolata, akimpa mamlaka Rekta kufanya ibada ya kupunga, ikiwa ni lazima. Alipotaka kumwingiza kanisani, haikuwezekana, ijapo wanaume wawili walitumia nguvu zao zote. Alionekana kana kwamba amefungwa ardhini; wakapaswa kuacha kujaribu.
Basi, wakamwomba Allamano aje kwenye mgonjwa, katika nyumba alimopokelewa. Na, tazama, Allamano anapokanyaga nyumbani, mwenye pepo, aliyefungwa chumbani ghorofani, alianza kuhangaika, halafu kujitupa kwa nguvu kwenye kuta na kila mara akimwelekea mahali alipokuwa padre, akimwashiria kama angemwona, akimfuata hatua kwa hatua akitapika kila aina ya matusi kwake.

Allamano alitaka kwanza kuhakikisha kama kweli ni shauri la pepo. Aliingia chumbani bila stola au kitu kingine cha ibada; mwanamke akibaki tulivu. Aliingia tena na stola imefunikwa na koti... na mara alianza kupiga kelele na kujikunja. Jaribio jingine: alijaribu kumkaribia na medali, na maskini alikuwa kama mnyama mkali.

*Ukurasa 52*

Aliwakusanya ndugu katika chumba jirani na kusali pamoja, halafu akaamka kiujasiri:

“Imekuaje? – akatamka – kwamba shetani atamweza B. Maria Consolata?”.

Akafungua wazi mlango, akaingia katika chumba cha aliyepagawa na, kama angebebwa naye na nguvu ya juu, akamrukia akamwingiza midomoni medali ya Consolata, na kulia kwa sauti kwa shetani:

“Nakuamuru kumtambua Malkia wako!”.

Nukta tu... yule maskini akaanguka chini kana kwamba amezirai; Allamano akaamuru apewe kinywaji cha nguvu; na maneno ya kwanza ya mwanamke yalikuwa:

“Ahsante, ee Bikira Mtakatifu sana!”.

Kesho yake alikwenda kanisani Consolata kwa ajili ya Misa ya shukrani, na pamoja yule aliyekuwa chombo mikononi mwa B. Maria, kupewa neema kubwa hivi.

**Mkubwa wa Monasteri**

Mwaka 1873, mara alipopata upadirisho, kwa matakwa, na kama amri, ya Mkuu wa Nyumba Ndogo ya Mwongozo wa Mungu (Cottolengo), Allamano alichukua wadhifa ya mwungamishi wa kawaida wa Masista Taidina. Akijitetea kama kawaida kuwa ni kijana wa umri kwa wadhifa nyeti jinsi hii, Padre Anglesio akamjibu: ”Hata don Cafasso alianza akiwa kijana kufanya kazi kwa ajili ya roho za watu!”.

*Ukurasa 53*

Imetosha naye aamue pia, Mpwa, kushika utume huo wa kwanza. Alishika lakini kwa muda mfupi, alipoteuliwa kuwa Kiongozi wa roho seminarini.

Mwaka 1886, tulivyokwishasema kard. Alimonda alimteua kuwa Mkubwa wa Masista wa Mt. Yosef. Jinsi alivyoshika wadhifa hiyo kwa uradhi wa wote, imeandikwa katika habari za shirika, inayosema kuwa “fadhila zake za kipadre”; - “uthabiti wake wa tabia pamoja na wema kweli wa kibaba”; - “hekima yake pekee na upendo”; - “uangalifu wake wa kujadili, wa kupendeza”; - “busara yake isiyopatikana, nadra”; - hadi “roho ya kitawa, kushika sheria kawaida, nidhamu, kutoka kwa mashauri yake zimepata faida na kuongezeka”. Na tena husemwa juu yake kama “Mkubwa mwerevu, wa msaada mkuu kwa Mkubwa, akijali mema ya kila sista na kwa jumuia kwa jumla, mwenye jitihada ya ubora wa kazi kadha wa kadha, akihamasisha masomo kadiri ya mahitaji ya nyakati na ya wadhifa”. Mwaka 1891, kwa sababu ya kazi nyingi, Allamano alijiudhuru, “akiacha jumuia katika uchungu mkubwa”.

Mwaka 1899 tunamwona kan. Allamano kama Mkubwa wa Masista wa Maamkio. “Katika miaka sita ya wadhifa yake – husomeka katika ripoti ya Wakubwa – alijimudu kwa uaminifu mkubwa, akitekeleza kila mwaka Uchunguzi

*Ukurasa 54*

kama alivyohimiza Mwanzilishi wetu Mtakatifu. Katika maonyo yake alikuwa dhahiri, kamilifu, mwenye heshima, mtaratibu katika mwenendo wa kitawa hadi mambo madogo sana. Akidokeza Katiba zetu alikuwa akisema: “Aliongea Mt. Fransisko wa Sales, inatosha!”. - Alitilia maanani kuchagua waungamishi wa kufaa jumuia, wale wa kawaida, na wale wa nyakati za pekee.

“Neno lake, likilowa daima na mambo ya kiroho ya hali ya juu, lilikuwa umeme wa mwanga, ambalo mara lilitokomeza kila shaka na kupendelezea fadhila. Mwongozo wake, ulikuwa wazi, hakika, na kuonekana umevuviwa na kuachia roho katika utulivu daima.

Kama Baba halisi, alichukua moyoni yote yaliyohusu nyumba, kwa mawazo mapana, na moyo mkubwa kushughulikia katika mazingira sugu na magumu.

Tarehe 13 Mei 1906, akizidiwa na kazi kwa sababu ya kuanzisha Shirika la Wamisionari, alichukua nafasi ya kuhamisha Monasteri hadi Pozzo Strada, ili ajiudhuru kama Mkubwa, na walipaswa kuridhika. Aliahidi lakini kuwa daima atawaona kama mabinti yake, na kweli alitekeleza mara nyingi...”.

*Ukurasa 55*

**Mwungamishi mtakatifu**

Licha ya kuongoza kiroho katika Monasteri na katika mashirika mawili aliyoanzisha, vipaji bora vya kan. Allamano kama Kiongozi wa roho viling’arika kwa namna ya pekee katika kitubio.

Akiumbishwa katika shule ya Cafasso, alifanya kitubio kuwa uwanja wake wa utume hali ya juu. Ungeweza kusema kuwa kuungamisha kwake kulikwa kazi aliyopenda zaidi, hata kuonyesha furaha ya kutekeleza huduma hiyo, na kuridhika sana hasa baada ya kumrudisha zake mtu katika amani. Kwa kawaida alikuwa anaungamisha Consolata, nyuma ya sakristia, mahali pembeni na rahisi kupafikia. Alitumia saa nyingi asubuhi, na hata alasiri, na wakati ule, waliomtafuta, walikuwa watu wa uchumi.

Watu wengi maarufu, wa Kanisa na raia walimtumia kama kiongozi wa roho. Lakini yeye hakupambanua kati watu wa aina yo yote; ila akiona watu waliokuwa na haraka, au watoto kucharuka, aliwaita kwake, na kuwahudumia wa kwanza. Upendeleo huo alitumia hasa kuhusu watu ambao walikuwa hawakupata sakramenti toka siku nyingi. Ilipendeza na kugusa moyo kuwaona hawa waliopotea,

*Ukurasa 56*

walipoondoka kitubioni: walidhihirisha usono uradhi wa kiroho, ambao mara nyingine walionyesha kwa maneno, wakiahidi wasiregee tena katika maozea ya Kikristo.

Sehemu ya pekee ya walioungama kwake walikuwa Mapadre. Wangapi walifika kwake! Hata toka nje ya Pidmont, wakiongozwa na neema ya Mungu kwa ajili ya kujifanya upya kiroho kikamilifu. Baba mwema alikuwa akipokea machozi ya mwungamo, na kwa mkono mwororo, lakini thabiti, alikuwa akitibu madonda yao, na kuwarudisha kwao baada ya kubariki makusudi yao.

Tabaka nyingine ya waungamaji ambao Allamano alikuwa akiwashughulikia, ilikuwa ile ya wenye mahangaiko ya rohoni. Imeonekana kana kwamba alipewa kipaji che pekee cha kuwatuliza roho zilizohangaika daima; na imeonekana kwamba Mungu alimpelekea wa kutosha: mapadre, watawa, walei; wakiwa mapadre, aliwasindikiza hadi sakristia, na kuwaona wakati wa maadhimisho ya Misa, na tena baadaye hadi ofisini mwake, na hatimaye kuwaaga na amani akiwaamuru kutii. Na utii ndio dawa peke yake aliyotumia.

Lakini sio watu wenye ibada tu waliomwendea Allamano, lakini hata wakosefu "*quatriduani*" (wa siku nne), waliotoka kutoka kaburini mwa dhambi. Siku moja alifika Kanisani bwana mmoja, ambaye waziwazi alifunulia

*Ukurasa 57*

Picha

*Ukurasa 58*

padre wa kuhudumia: "kwamba hajaungama tangu miaka ishirini. Basi, alitaka kufanya, lakini alitaka padre anayeweza kumwelewa". Wakamfiria mara Rekta. Akaja, akaingia kitubioni. Baada ya roho saa akatoka aking'aa, na kusema: "Nimempata mwugamishi mtakatifu!".

Akiongea hususan nguvu ya neema, Allamano alisimulia habari za mkosefu mmoja maskini, ambaye alipofika kuungama kwake, hakutaka kabisa kuacha nafasi ya dhambi, kana kwamba alidhihaki maonyo aliyopewa, hadi kujibu kwa ufidhuli. "Usipotaka kunipa maondoleo, sina shida nayo!".

Asijue la kusema zaidi kwa kugusa moyo wake, Allamano aliinua macho mbinguni kwa sala toka moyoni kwa mjomba: "Ee Don Cafasso, umwongoe wewe!". Tazama, anamgeukia... anaona yule maskini akidondoa machozi. Neema ya Mungu lilimgusa dakika ile. Akaongoka na kuendelea kuishi kama Mkristo mwema, ijapo alipaswa kupata magumu sana.

Halafu, mara nyingi sana, aliitwa nyumbani kwa wagonjwa mahututi, hasa wakosefu wa wazi na wagumu; na akifaulu kuwajongea, hakika waliongoka, bila shida.

*Ukurasa 59*

**Paradisini kwa utii**

Na hawakuwa pungufu wagonjwa walioomba msaada wa Allamano, asilalamike kana kwamba anasumbuliwa, mchana na usiku. Kuhusu wale waliozidiwa, aliwasaidia hadi kufa kwao, kwa faraja kubwa ya mgonjwa na ya ndugu zake.

Hapo tunakumbushwa tukio moja ambalo Allamano alizoea kusimulia kwetu akifundisha utii. Lilitokea mwaka 1899, na huhusu kifo kitakatifu cha Prof. Ing. Edward Felizzati, ambaye kwa muda wa miaka mingi alikuwa akifundisha kama Msaidizi katika fani ya Jiometria katika Chuo Kikuu chetu; na kufundisha Hisabati katika Sekondari ya Cavour; mwalimu wa somo hilo la Mwana mfalme Ferdinand, mwana wa kwanza wa Duke wa Genova.

Mkatoliki safi sana, alishika dini kwa wazi na heshima, kwa mfano na kwa maneno, akiweza kufunika katika kivuli cha unyenyekevu matendo yake maarufu ya pekee na harufu ya matendo yake matakatifu. Akiwa mwepesi sana wa dhamira, karibu na kuhangaika, alikuwa anahitaji daima neno la mamlaka la kumtuliza moyo na kuhamasisha kupokea kila siku. Neno hilo lilitoka kwa kan.

Allamano, ambaye alikuwa baba yake wa roho mpendelevu sana.

Ghafla, mwezi Novemba 1899, bwana Felizzati anaugua, na hali yake ilionekana kuzidiwa.

*Ukurasa 60*

Jioni ya tarehe 19, Allamano, aliitwa haraka kwenye rafiki mgonjwa. Akabaki usiku kucha, halafu asubuhi, akiona ametulia, akamwambia:

“Sikia, Injinia mpendwa, mimi nakwenda kuadimisha Misa, halafu nitarudi”.

“Hapana – akajibu mgonjwa – usiende... usiniache...”.

“Naona kuwa hali yako ni afadhali, nitarudi mara moja”.

Mgonjwa alikuwa hatulii, na hapo akatokea kusema:

“Basi... niamuru kwa utii niende Paradisini...”.

Allamano, baada ya kitambo kushtuka, akamwambia thabiti: “Basi, naam, nakuamuru kwa utii, uende Paradisini!”.

Punde mgonjwa akainama kichwa, akazimia roho.

**Talanta iliyofanyiwa biashara**

Vipaji vya mshauri, sawa na vile vya kiongozi wa roho, vilionekana katika Allamano kuchukua tabia ya utume halisi aliyokabidhiwa na Mungu. Naam, ilionekana kwamba kwake ilimulika tena nuru ile iliofichwa kwa kifo cha Mt. Cafasso, hata inawezekana kutumia kwake, kwa ukweli kamili, yale yaliyosemwa katika mchakato wa kumtangaza Cafasso Mwenye Heri, yalishuhudiwa na watu: kuwa kwa kutaka ushauri

*Ukurasa 61*

wa mtumishi wa Mungu, walitoka watu kuitoka kwa kila mahali, na watu wa kila yabaka ya watu na hali ya kijamii.

Hatufunulii siri yoyote, tukisema kuwa kwa Allamano walikimbilia Maaskofu makuu wenyewe wa Torino. Kweli alikuwa mshauri wa kwanza wa Askofu mkuu Daudi Riccardi; hali kard. Augustino Richelmy alimwamini sana daima na kumheshimu sana; na kard. Gamba, alipokufa Allamano, alisikiwa kusema: “Sasa hakuna mwingine Torino wa kumwendea kwa shauri!”.

Nayo pia yanafaa kwa Maaskofu wa majimbo mengi ya Pidmont. Kwa nafasi ya Mabaraza ya Maaskofu wa Kanda Subalpino pale Consolata, walionekana kuwa Maaskofu wote walitafuta nafasi ya kuzungumza naye, na wengi walizungumza hususan mwenendo wa majimbo yao ili wapate ushauri.

Hatupitiwi tukisema kuwa kwake walikimbilia makleri wote wa jimbo, maparoko wazee hadi mapadre vijana. “Kila hangaiko binafsi – anaandika mons. Pinardi – au mashaka kuhusu uamuzi wa matendo au wasiwasi wa kuamua, walimwagika kwenye pembe lile la Chuo cha

mapadre, na kurudi wamepokea neno la kukata shauri na la nguvu. Aliongea mara chache na mapadre wa Chuo, lakini Chuoni mapadre walirudi kuomba shauri Mkubwa waliomfahamu toka mbali, walikuwa wanakuja kujifunza miongozo

*Ukurasa 62*

ilioangaza hali ya maisha zilizovurugika, na hasa kusaidia kutegemeza hatua za kwanza katika huduma. Mtu aliyejitenga katika upweke wa ukimya, alisambaza kwa nguvu kazi yake katika Jimbo kuu.

Sawa na makleri, pia walei nao: toka aliye mdogo kabisa wa watu baki, hadi Wana Mfalme wa Nyumba ya kifalme. Alikuwa akipenda kushinda naye katika mazungumzo ya kirafiki Mwana mfalme wa Carignano, katika ziara zake za kila juma Kanisa la Consolata; Binti mfalme Koltilde mara kwa mara alimwita katika Jumba lake Moncalieri, au katika Jumba la kifalme mjini. Kazi nyingi ya kuanzisha asasi za kidini za Binti mfalme takatifu zinatokana na mashauri ya Allamano. Aidha wengi kati ya Washarifu wa Torino, walimwendea kwa ushauri, katika mambo ya binafsi, na pia katika mambo ya kisiasa na kijamii.

Alikuwa amejaliwa vipaji vyote vya mshari mwema. Mwenye adabu sana, na mwema sana, daima mfurahifu na kutabasamu, alimwendea mgeni akiondoa kofia, na kumwingiza, kwa kujali, sebuleni, na kuketi karibu naye na kumsikiliza kwa saburi ya kuvutia, asionyeshe uchovu au haraka.

Tena alikuwa mtu wa busara. Mafanikio ya ajabu ya kazi alizoshughulikia, baada ya Mungu, ni kutokana na busara yake. Hakuwahi kutenda kwa mvuto au bila kufikiri kwanza, katika mambo makubwa na katika madogo. Hakuna sababu ya kushangaa ikiwa mashauri yake yalikuwa na chapa ya fadhila hiyo muhimu.

*Ukurasa 63*

Kwa busara aliunganisha werevu wa kushangaza, ufahamu mkali sana wa moyo wa watu, na vile kutambua mambo ya uchumi na mambo ya dunia. Daima aliyemkaribia alishtushwa na ukali wa mtazamo wa kupenya mambo na watu mintarafu faida ya kibinadamu. Wala hatushangai kusikiliza Profesa wa Chuo kusema: "kuwa mbele ya kan. Allamano walijitambua wadogo hususan dhana ya mazoea ya maisha.

Sifa zaidi ya mashauri ya Allamano, ilikuwa kwa ajili ya uhakika aliowapa. Jinsi alivyokamata kwa urahisi kiini cha shauri, vivyo kwa urahisi bila shida aliwapa jibu, alionyesha njia ya kushika. Hakuwa kama wale ambao wakiombwa, wanabaki wamebaki na wasiwasi ka kuwaachia na wasiwasi kuhusu la kutenda; bali yeye alitoa kila mara hukumu yake, na kwa hakika, na uhakika uliwapa watu moyo.

Tunaruhusiwa kufunga kwa kusema kuwa kan. Allamano alipewa kutoka kwa Mungu kipaji cha kimungu cha shauri: kipaji wasichopewa wote, na wachache wanapewa kwa kiasi alichopewa yeye. Kwa upande wake, hakuifukia talanta hiyo, bali kama mtumishi mwema na mwaminifu aliifanya kazi kwa kiasi kikubwa alichoweza hadi siku ya mwisho wa maisha yake.

*Ukurasa 64*

**Kutazama mbele ya baadaye**

Mang'amuzi licha ya kuonyesha hekima ya mashauri aliyotoa Allamano, pia si mara chache kwamba yalionekana kama unabii.

Kwa padre aliyeomba shauri kama ilifaa ama sivyo, kujionyesha kwa mashindano ya parokia, Allamano alijibu: "Nenda tu, lakini hutapata parokia ile. Mungu anakuita kwa majaribio magumu zaidi". Haukupita muda mrefu kuwa, kinyume cha kila matarajio ya kibinadamu, alijikuta amekabidhiwa kujenga kanisa jipya.

Mtheol. Mascarelli alipoteuliwa kuwa paroko msaidizi wa Mt. Sekundo Torino, Allamano alimwambia: "Furahi kwenda; lakini baada ya miaka miwili mitatu Bwana atataka mengine kwako. Baada ya miaka michache Mascarelli aliteuliwa kuwa Kiongozi wa roho Seminarini.

Kuhusu padre mpya, Allamano alikuwa akisema: "Atawasumbua sana Wakubwa wake, lakini kabla ya kufa atatubu". Baada ya miaka michache sana, yote yakatekelezwa barabara.

Mtheol. Alberione, mwanzilishi wa Jamii ya kidini ya Mt. Paulo, Alba, anaandika: "Nilisikia Allamano kutoa shauri kuhusu wito wa vijana wawili mafrateri. Yeye ambaye alipewa nafasi ya dakika chache

*Ukurasa 65*

ya kuwasikiliza, alionekana kufahamu mara moja hali yao, kwa sababu mara alitoa maono yake. Hayakufuatwa kwa sababu wengine waliamua tofauti. Lakini mambo yalikwenda barabara jinsi Allamano alivyosema.
Walipaswa baadaye, baada ya hasara ya kimaadili, kushika njia iliyoonyeshwa na kan. Allamano. Mmoja wao, mambo yake yalikwenda hivyo, kwamba hata sasa nashangaa kudhani kuwa Allamano huenda alikuwa na mwangaza wa pekee kutoka kwa Mungu.

Nyakati ambamo sheria kinyume na Mashirika ya kitawa, mtu mmoja alikwenda kumfunulia mahangaiko yake kuhusu bahati ya Monasteri ya Maamkio, iliyohamisha siku zile karibuni Pozzo Strada. Naye: "Masista wawe wema na hakuna mabaya yatakayotokea". Jibu lile limetaarifiwa kwa Mkubwa ambaye alishituka sana na akawataarifu masista wanufaike. Monasteri haikushambuliwa, na hadi leo inahifadhika.

Bado tukio moja. Huhusika na yule Bibi Fumagalli, ambaye ukumbusho wake ni wa sikitiko katika historia ya Torino na Italia. Huyo alijitakia kulipa jina la "Consolata" kwa asasi yake fulani. Allamano alipoulizwa kwa shauri hilo, alikataa kibali: "Ni mimi Rekta na ni wajibu wangu kulinda sifa ya Jina la Consolata. Kunyang'anya kwako jina hilo kutakuletea laana". Hakutii na ikatokea, alivyosema, baada ya miaka michache,

Ukurasa 66

kutoka kwa asasi ile ikatoka ishara ya dhoruba kali isiyowahi kutokea Italia, dhidi ya heshima ya mapadre Wakatoliki na dhidi ya asasi katoliki.

## Kazi zote za mema

Kwa kuwa mshauri, kan. Allamano amekuwa chombo mikononi mwa Mungu wa kuinuka au kuimarika kwa asasi za kidini na za matendo mema sio chache mjini. Tunazitaja kadha wa kadha.

Aliwahi kumshauri P. Yosef Giacobbe, wa Dottrinari, kujichukulia kazi ya kujenga *kanisa la kiparokia ya Yesu wa Nazareti*, akimsaidia pia na ufadhili ya fedha.

Kwa shauri lake Bibi Orsola Turchi alianzisha *Shirika la vipofu*, ilianzishwa kwanza katika barabara ya Deposito (sasa road Piave), halafu likahamishwa katika avenue Napoli, ambamo kazi ya huruma ya kan. Boccardo ililistawisha sana.

Kwa shauri lake Dada Franchetti walianzisha *Worshop ya Consolata* na lengo la kutayarisha washonaji wafundi sana katika mazingira safi kimaadili na kidini. Naye amekuwa mfadhili mkuu wa asasi hiyo.

Mons. Edward Bosia anamhesabia yeye mshauri na msaada ya kuanzisha wa Oratori yake ya Mt. Felx.

*Ukurasa 67*

*Shule ya Warosmini* Torino kutoka kwa ushuhuda wa mkuu wa Shirika, iliotokea kutoka kwa ushauri wa kan. Allamano, ambaye pia alitabiri ustawi wake ilivyo leo.

Ni Allamano kuwashauri Mapadre wa Mt. Yosef kuanzisha mchakato wa Murialdo, mwanzilishi wao, aliyemfahamu binafsi. Akawa daima mshauri aliyethaminiwa na shirika hilo.

Kabla ya kuanza *Jamii ya Mt. Paulo* Alba, ambayo unajulikana sana ustawi wake wa ajabu na mema kwa wingi aliyokwishatenda, Theol. Yakobo Alberione alimwendea Allamano kuomba shauri, na akatenda kadiri alivyoelekezwa.

Na hatuwezi kusahau sifa za Allamano kama Mjumbe wa Halmashauri wa *Regia Opera di Mendicità istruita*; - Mjumbe wa Halmashauri wa Uhasibu wa *Hospitali Mkuu* wa mji wetu; - Mjumbe pia wa *Kamati za Kiaskofu* muhimu.

## Uchapaji na Aksyo Katoliki

Na pia kwa yale yanayohusu mwendo Mkatoliki katika njia zake mbalimbali, kan. Allamano amekuwa mkarimu wa dhana na utaratibu kamili.

Yeye anashiriki na walinzi watukufu waliopinga gazeti la Waliberal wakiliona kama dharau na hatari kwa makleri. Kinyume chake gazeti Katoliki

*Ukurasa 68*

limepata kutoka kwake mhamasishaji wa kufanikisha, na pia mdhamini halisi. Alitaka gazeti liwe jepesi na kifundi, akisema kuwa mambo mapya kuhusu muundo na teknika wasiogope kuzitekeleza.

Aliwatilia moyo walioshughulikia utume huo, kwa sababu, mbali na wanavyofikiri watu, maisha ya mwandishi yana uchungu na kugonga mwamba, zake.

Lakini Allamano alitaka kutoa zaidi ya kubembeleza; alitoa fedha. Kwa nafasi aliweza kutumia gazeti kwa ajili ya kazi alizofanya katika amali yake isiyochoka: Kanisa la Consolata na Misioni. Lakini aliifanya kwa utaratibu sana na kwa adabu pia, kwamba waandishi walikuwa wanafurahi kumridhisha, na walijitahidi kwa bidii sana kustahili shukrani yake, isiyokosa hata mara moja, hata kwa huduma ndogo, na iliyostahili wema wake.

Lilipotoka *Italia Reale*, Allamano alikuwa mmoja kati ya wachache asiyeridhika kuwapongeza kwa maneno tu, bali alisaidia na ufadhili mara nyingi. Vile alifanya na magazeti Makatoliki yaliyofuata, kama Conquiste Giovanili, gazeti la juma ya Shirika Katoliki la Torino. Na kuhusu *Voce dell'Operaio* (leo *Voce del Popolo*), tazama, alichosema mtu maarufu wa kikanisa: "Siku moja ya 1889, mwanzilishi wa *Voce*, cav. Giraud,

*Ukurasa 69*

alimwambia kwake Allamano kuwa, mwisho wa mwaka, atafunga kutangaza gazeti, kwa sababu ya shughuli zake kama katibu katika kiwanda cha kutengeneza ngozi Giacomo De Luca. Kan. Allamano alipanga kukutana nao wote wawili Jumamosi iliofuata na, walipokuwa mbele yake akamwambia De Luca: "Bwana huyo - akamwambia akimwashiria Giraud – anataka kufunga gazeti kwa sababu hana nafasi ya kulishughulikia. Haifai kutokea jambo hilo; kwa sababu hiyo, wewe, bwana De Luca, tafuta katibu mshiriki ashike nafasi yake katika kiwanda, ili yeye aweze kuendelea bila taabu kushughulikia gazeti, ambalo tangu sasa litakuwa la kila juma, badala ya kila majuma mawili". – ndivyo ilivyofanyika, kwa sababu watu hawa wawili walithamini sana neno la Allamano kama neno la Mungu"

Tunajua pia kuwa ni kwa sababu ya shauri na hifadhi ya Allamano kuwa lilizaliwa *Risorgimento Cattolico* la Mondovì.

Hata Padre Paul Bailly, maarufu mwanzilishi wa gazeti

"La Croix", alisisitiza kuwa alipata wazo kuanzisha na hata jina ya gazeti hilo tukufu miguuni pa B. Maria Consolata wa Torino, na kushauriana mara nyingi na Allamano.

Sawa na magazeti, alipenda Aksyo katoliki, na kwa ajili yake aliingiza katika Chuo cha mapadre kozi ya masomo ya kila juma. Daima aliwaruhusu mapadre wanachuo kushiriki makongamano na mazungumzo ambamo waliweza kujifunza kwa faida ya huduma ya kipadre.

*Ukurasa 70*

"Aliwapenda Wafanyakazi Wakatoliki – aliandika juu yake mons. Pinardi – waanzilishi ambao, kwa kuitikia mahitaji mapya ya wakati waliingia halafu kwa mpango kamili zaidi katika mistari ya Aksyo Katoliki.

"Na Wanawake Wakatoliki walitambua roho yake kuu, ambao katika kipindi cha maafa ya nchi na ulimwengu, walirusha jambo la ujasiri la saa moja ya kuabudu kila juma ili kuuombea ulimwengu mzima huruma ya Mungu. Imekuwa Kanisani Consolata walioweza kutekeleza

matakwa yao.

"Na tena Allamano, wengi wanamkumbuka kwenye baraza mlangoni mwa kanisa, wakati wa kumalizika majira ya baridi mwaka 1921, karibu na marehemu kard. Richelmy, kutazama maandamano maarufu ya vijana. Ilikuwa siku ya furaha na ari: na Kanoni mzee, aliyedhoofika kwa ajili ya umri, alikuwa kama anaingiliwa na uhai mpya. Ilikuwa roho iliyoshinda juu ya udhaifu wa nguvu inayofifia, na kutambua katika wale vijana Wakatoliki ushindi safi ya mapadre wake na ahadi zenye faraja za baadaye".

**Amali ya kijamii**

Hata katika tawi la amali ya kijamii kan. Allamano alitaka mapadre vijana wapate malezi ya kufaa kadiri ya mahitaji ya nyakati, kwamba wasidharau cho chote kinachoweza kunufaisha huduma ya kipadre. Kwa lengo hilo alimkabidhi kan. Dakt. Anton Cantono, mtaalamu

Ukurasa 71

katika somo hilo kozi ya masomo ya kijamii, kwa ajili ya mapadre wanachuo.

Lakini alitaka, kwa haki, kwamba washughulikie kwanza elimu na malezi yao ya kipadre kimsingi hasa. Naam, alitambua hatari: kuwa bidii ya ziada kwa ajili ya utume wa nje ilikuwa hasara, kwa ajili ya mapadre vijana, kuliko malezi ya kiasketiki-moyoni yanayosaidia padre kijana kushinda mapambano magumu ya binafsi dhidi ya ulimwengu na wafuasi wake.

Alidhamini umuhimu wa jambo kwamba Wakatoliki wawe na umoja kamili na wajasiri kudhihirisha upenyezi wao kiroho katika maisha ya hadhara. Alisisitiza kwa lengo hilo kufanya kazi kati wa watu duni, na kuchunguza mahitaji yao, ili kuwathibitisha katika imani.

Kuhusu siasa halisi, hakujiruhusu wala kuruhusu wanachuo na wanafunzi alioongoza. Kama alivyokuwa Mtakatifu Cafasso, vivyo hivyo Allamano alizoea kusema kuwa padre anapaswa kujua siasa ya roho peke yake. Lakini Wakatoliki walipoitwa kupinga kwa silaha ya kura nguvu ya maadui wa mapinduzi, Allamano hakusita hata nukta kurusha katika mapambano jeshi lake kwa umoja wa mapadre wanachuo na wanafunzi wamisionari, akitungulia kwa mfano wake.

*Ukurasa 72*

**Mazoezi ya roho ya makleri na walei**

Kazi nyingine ya ari ambayo Allamano alishughulikia na moyo wa kitume, zaidi ya miaka arobaini, ilikuwa ile ya mazoezi ya roho kwa makleri na walei, Sant'Ignazio, mlimani pa Lanzo Torinese, akifuata pia katika hayo nyayo za Mt. Cafasso.

Aliyatilia maanani sana. Shughuli yake ya kwanza kutafuta wahubiri wa kufaa, waliojaa ari, na wenye maisha safi, wahubiri zaidi kwa maisha kuliko kwa neno. Halafu alitaka kuhudumia wanamazoezi kwa dhati na kinaganaga, ili kuondoa usumbufu wo wote: kwa sababu hiyo alipanda Sant'Ignazio siku kadhaa kabla, ili kuhakikisha kuwa yote yawe tayari.

Walipofika wanamazoezi, alipatikana kwenye kiwanja cha kanisa, na kuwapokea wote akiondoa kofia, kana kwamba ni mtumishi wa wote, na kila mmoja kumpa neno la kumfaa heshima

yao na mahitaji yao kiroho. Alitenda hayo kwa wema wa pekee wale waliotumwa na wakubwa wao wa kanisa. Hao aliwafuata hatua kwa hatua, akijitahidi kukutana nao wakati wa mapumziko, ili kusema yale yaliyoweza kufungulia moyo wao kujiaminisha wazi kabisa.

*Ukurasa 73*

*Picha*

*Ukurasa 74*

Tunajua kuwa kuna mapadre ambao wanahesabu mabadiliko yao au kukaza maisha yao ya kiroho, tokana na mazoezi waliyofanya Sant'Iganzio, na hasa katika mazungumzo ya kimoyomoyo na kan. Allamano.  Pia tunajua kuhusu walei ambao pale chumbani mwake miguuni pake, walipata mwanga na nguvu ya kusema: "*Surgam et ibo ad patrem meum*" (nitaondoka, nitakwenda wa baba yangu).

Kati ya yote kuna simulio la kijana mmoja aliyekuja Sant'Ignazio katika hali mbaya ya kuonewa huruma. Ameugua nevrastenia kali, akiwa na matukio ya nguvu sana, ambayo yalipomwangusha kimwili, yalikuwa kitisho kwa ndugu, ambao hawakujua la kufanya nini tena. Alikwenda Sant'Ignazio, akipelekwa na rafiki. Allamano, akiangazwa kutoka juu, hakukawia kuona moyoni mwake. Siku moja alipomwita kwake, baada ya maneno mema kadhaa, akamwuliza:

"Uniambie, rafiki yangu, lakini sema wazi, ugonjwa huo ni wa kimwili tu, ama...".

Hakumaliza maneno.

"Wewe umegundua" – akalia yule maskini - .

Halafu akamfungulia yote aliyokuwa anayo moyoni katika moyo wa yule baba mwema; akarudi nyumbani amegeuka katika mwili na roho.

Basi, mbinguni tu tutaweza kujua mema yote aliyotenda Allamano hata katika uwanja huo.

*Ukurasa 75*

**Kumtangaza Mwenye Heri Mjomba Don Yosef Cafasso**

Tunapaswa kudokeza walau kidogo hususan mchakato wa kumtangaza Mwenye Heri Don Yosef Cafasso, ulioanzishwa kwa matakwa ya kan. Allamano. Hatutasema kuhusu awamu zote ulizopitia,, ila tu kwamba ulidumu miaka thelathini na kumtegemea kan. Allamano peke yake. Aliutayarisha kwa bidii yote hadi mambo madogo sana, kuangalia, na tunaweza kusema kuongoza, kwa sababu Mwombaji, kwa kweli, alikuwa yeye. Ama, tukiingilia kidogo mambo hayo ni rahisi kufahamu jinsi mchakato huo ulimgharamia Allamano taabu na sadaka za kila aina.

Safari moja, baada ya siku ya maumivu ya kichwa makali sana (hemicrania), tulimkuta Baba mwema mezani kushughulikia mchakato wa miujiza wa mjomba, tumeshindwa kujizuilia kumkaripia kwa upendo:

"Lakini, Padre, unachoka mno!".

Naye akionyesha sura ya kuteseka, lakini shwari:

"Ah, kwa ajili ya watakatifu tunafanya hayo na tena mengine zaidi".

Naye kweli hakuchukua taabu hiyo ila kwa sababu za kimungu. Alikuwa akisema: "*Ingalikuwa kwa sababu Cafasso alikuwa ndugu yangu, nisingalifanya hayo yote, ni kwa sababu ya kumtukuza Mungu*". Na mara nyingine: "*Kweli sadaka zilizofanyika ni nyingi sana!". Lakini naweza kusema kuwa, nilianza kutekeleza*

*Ukurasa 76*

*mchakato huo si kwa sababu ya udugu, bali kwa ajili ya mema yatokanao kwa kumtukuza padre huyo mtakatifu*". Siku moja, walipomtakia heri ya kumaliza haraka mchakato, na matokeo yake mazuri, akajibu: "*Ah, aidha mimi sipotezi amani na utulivu. Najali zaidi kuokoa roho moja, kuliko kufaulu katika mchakato huo wa kutangaza Mwenye Heri, kwa sababu nadhani kuwa Mungu anatukuzwa zaidi*".

Hasa ni kwa sababu ya utakatifu wa makleri, kwamba alikusudia. Kuwapa mapadre Msimamizi mwenye uwezo mbinguni na kielelezo kamili wa fadhila zote za kipadre. Tena kwa kipindi fulani alibembeleza dhana, ambayo hakutekeleza, ya kutayarisha na kuomba Baba Mtakatifu mswada wa Ensiklika ya kuwaonya Maaskofu ya kuanzisha katika majimbo yao Chuo kama kile cha Torino, na Mwenye Heri Yosef Cafasso kuwa Msimamizi wa wote.

Kumtangaza Cafasso Mwenye Heri kukatokea tarehe 3 Mei 1925. Allamano ijapo mdhaifu aliweza kushiriki. Alikuwa anang'aa. Sanamu ya Mjomba ilipoonekana katika 'utukufu' kati ya makofi ya hadhara, macho yake yakamkazia punde tu, na mara kuinama. Alibaki hivi hivi, akijikusanya, asijali yote yaliyomzunguka, kama amekandamizwa na shangwe kuu hiyo ya kiroho. Katika ibada ya alasiri alipotoa baraka ya Ekaristi, Baba Mtakatifu Pius XI alipopokea zawadi zilizo za desturi, alimpokea kwa ishara ya upendo kan. Allamano, ambaye kwa majonzi na machozi

*Ukurasa 77*

alijaribu kumshukuru, na akawaambia akidokeza zawadi zile za kushangaza:

"Ninyi mmetutajirisha kweli!".

Katika upokezi uliofuata wa wahujaji wa Pidmont, Baba Mtakatifu, mara alipokutana na kan. Allamano, aliyemwonyesha Askofu mkuu wa Torino, kard. Gamba, alisema kwa mshangao:

"Ni nani asiyemfahamu kan. Allamano? Ni muda mrefu tunayemfahamu, hasa kwa njia ya sifa ya Shirika la Msioni!".

Na sasa tunapaswa kuongelea kazi hiyo, muhimu sana katika ya muhimu aliyoshughulikia kan. Allamano.

*Ukurasa 78*

Tupu

*Ukurasa 79*

# 2.
# Mtume
# wa mitume

*Ukurasa 80*

"... Hayo yote lakini tuliyosema kwa sifa, hayatoshea upendo mkuu ambao nao wewe unawaka kwa ajili ya roho za watu: na tazama, katika mwaka 1901 ulianzisha Shirika la Wamisionari, na mwaka 1910 la Masista Wamisionari, yote mawili kwa jina la "Consolata" kwa ajili ya Misioni za Nje. Na kiasi cha Wamisionari na Masista waliokwenda katika nchi za wapagani, ni kikubwa, na wanatekeleza wajibu mgumu wa utume wanatekeleza kwa ari, ijapo walifika wa mwisho shambani, hawaonekani kuwa nyuma ya mashirika mengine yaliotangulia zamani...".

Pius XI

*Kwa Jubile ya Kipadre*

*ya Kan. Yosef Allamano*

"...Itawezekanaje kusahau kuwa miaka iliyo bora ya upadirisho wako uliitolea kwa Misioni? Shirika la Wamisionari wa Consolata litabaki kama kumbukumbu ya daima ya ari yako ya kipadre, ya nguvu, jitihada na vifaa zilizotolewa kwa ukarimu kwa Misioni takatifu za Kanisa. Kwake litatekelezwa neno: *Defunctus adhuc loquitur (marehemu bado anaongea)*; kwa sababu litaendelea katika roho ya mwanzilishi wake kuwa kikundi kilichochaguliwa cha wamisionari na waokozi wa roho za watu..."

Kard. G. M. Van Rossum

Prefekt wa Propaganda Fide

*Ukurasa 81*

## Mwali unaolipuka

Shirika la Consolata kwa ajili ya Misioni za Nje lilikuwa kama mwali unaolipuka uliokuwa

moyoni mwa Allamano: Upendo kwa Mungu; ambao unafurika katika upendo wa majirani; nao katika ari; na ari hukumbatia viumbe vyote na sadaka yote.

Asili ya Shirika iko hapo, na amekiri wazi Pius XI katika maneno tuliyorejea.

Na haiwezekani kueleza, pasipo kanuni hii ya kimsingi ya kimungu, jinsi mtu daima mdhaifu, na mwenye mzigo wa mwongozo wa Chuo cha mapadre, na Kanisa la Consolata, na wakati kazi ya gharama sana ya kukarabati kanisa zilikuwa zinatekelezwa, kwamba alithubutu kujitupa katika shughuli sugu kiasi hicho, lenye magumu na lisilokosa yasiyotarajiwa ya kuogofya, jinsi ulivyo uanzilishi wa Shirika la Misioni ya Nje!

**Baada ya kushindwa ushindi maarufu**

Kati ya matukio ya kibinadamu ambayo Mungu anatumia ili kumtayarishia mtumishi wake kwa kazi hii kubwa lazima kuhesabu jambo la kudumu daima katika Jimbo la Torino roho ya kimmisionari, hasa kutokana na ari au Wakurugenzi kadhaa ya Kazi ya Enezo la Imani.

*Ukurasa 82*

Enzi Allamano alipokuwa mseminari, alishika madaraka hiyo kan. Yohanes Ortalda ambaye, licha ya kujitahidi na mifumo ya kusaidia misioni, alianzisha Mashule fulani ya Kitume yenye malengo mawili: kupatia Mafrateri kwa Majimbo Subalpino na wamisionari kwa nchi za nje. Asisi ilidumu muda mfupi, lakini haikukosa matunda: kama kuamsha ari ya miito ya kimisioni katika seminari, na baadhi yao walisafiri kwenda Misionini, bali wengine, waliokuwa na nia, walizuiliwa na sababu mbalimbali.

Kati yao alikuwamo Frateri Allamano. Tangu mwaka wa kwanza wa seminari aliamua, pamoja na wenzake wawili kuingia katika Shule ya Kitume ya Brugnole Sale, na aliwahi kuagana na mama yake. Lakini kwa sababu ya afya yake hafifu alishauriwa na wakubwa wake kuahirisha kujiunga nao, hivyo mwaka hadi mwaka, mwaka nenda mwaka rudi, hadi... alibaki jimboni tu.

Lakini alitunza hai moyoni upendo wa Misioni, akiulisha na masomo ya maandiko ya Massaia, ambamo alichukua mvuto wa uinjilishaji wa Galla; na ibada ya pekee sana ya Mt. Fidelis wa Sigmaringen, mfiadini wa kwanza wa *Propaganda Fide*, na wakati wa likizo kutembelea mara nyingi kanisa la Monte au lile la Madonna di Campagna, ambamo kuna sanamu yake.

Tena alipokuwa Kiongozi wa roho seminarini hakuacha kusisitiza waseminari ari ya Misioni

*Ukurasa 83*

na kuhifadhi sadaka ya Kazi za Kimisioni. Aliweza pia kutumia kwa maarifa kwa lengo hilo, kila nafasi. Siku moja, wakati wa kupumzika, frateri mmoja alitokeza senti hamsini ya fedha ili kuionyesha wenzake (wakati ule walitumia manoti tu, na ilikuwa shida kuona pesa ya fedha), na mmoja wao, kwa kugonga mkono aliiangusha chini, mara akisikia mlio wa fedha, Kiongozi alisogelea kikundi:

“Hapa hucheza bahati nasibu?”.

“La, sivyo – akajibu mwenyewe – nilikuwa nikionyesha pesa hiyo tu, ukumbusho wa mpenzi wangu”.

Naye kwa sauti ya kupendeza, akichukua pesa:

“Ajabu! Ninavyojua, hadi sasa ukumbusho ulikuwa moyoni, kumbe sasa ungekuwa katika pesa!... tufanye hivi: tutalipeleka kwa Kazi ya Enezo la Imani, hivyo atakuwa Bwana kumkumbuka”.

Hadithi ndogo, inayoonyesha lakini jinsi alivyojali Misioni.

Toka seminarini ari ya kitume ya Allamano ilipitia Chuoni cha mapadre ambamo, kati ya mengi, alihifadhi bahati nasibu ya kila mwaka kwa ajili ya Misioni, akishiriki na zawadi za binafsi.

Na kwa wakati huu aliendelea kustawisha moyoni mfumo wa asasi hiyo, ambayo kwayo jina lake limeungana katika karne. Itakuwa ushindi wake wa kitume dhidi ya kushindwa. Akizuiliwa kwenda Misionini, lakini atakuwamo, na kwa karne zote, katika nafsi ya Wamisionari wake na Masista Wamisionari wake!

*Ukurasa 84*

**Mifumo na vizuizi**

Mfumo wa kwanza wa uanzilishaji ni wa mwaka 1885-86. wakati ule Allamano alifikiri kuanzisha kazi iliyofanana na ile ya kan. Ortalda – liliyokwisha feli - akiipa chapa ya Misioni peke yake: kuwakusanya vijana wanaotaka kuwa mapadre wanaotamani Misioni, kuwatayarisha ya kufaa na halafu kuwaweka mikononi mwa Propaganda Fide, chini ya mashirika ya kimisioni yaliyomo. Ijapo kutokana na upinzani wa maaskofu kadhaa waliolalamikia upungufu wa mapadre, alipashwa kuhamisha mpango wake. Yalikuwa matatizo ya kwanza, yaani ishara hakika kuwa ilikuwa kazi ya Mungu.

Katizo hili la kwanza lilikuwa la kufaa kwa upande wa Mungu; kwa sababu, katika wakati huu, mfumo wa Allamano ulipanuka na kukamilika; sio tu kutegemea mashirika mengine, bali shirika lenyewe, likiwa na wakubwa wake na Misioni zake.

Kubadilika hivyo na kuchunguzwa katika vipengele vyake, mpango ulichukuliwa tena mwaka 1891. Hatua ya kwanza ya Allamano ilikuwa kutaka kujua Propaganda Fide ina mtazamo gani, na jibu likafika kutoka Roma la kibali ya hali ya juu na kutilia moyo.

*Ukurasa 85*

Lakini kutokana na mauti ya Askofu wa Torino, Kard. Gaetan Alimonda (Mei 30, 1891), na halafu mauti ya Kard. Simeoni, Prefekt wa Propaganda Fide (Januari 14, 1892) ililazimika kuacha yote.

Machi iliyofuata (1892), alisimikwa Askofu mkuu mpya wa kiti cha Mt. Maximo, mons. Daudi Riccardi. Hatuna habari kuwa Allamano aliwahi kuongea naye kuhusu mradi maadam popote yalikuwako malalamiko kuhusu ukosefu wa mapadre.

Ndivyo ilivyomalizia katika kushindwa hata majaribio hayo ya pili, bila kuachia nafasi kwa

matumaini ya kuridhisha kwa baadaye.

**Njia za Mungu**

Lakini Mungu, aliyesisitiza kazi na kutaka itekelezwe, alikuwa akitayarisha matukio yatakayopeleka utekelezaji.

Kwanza aliteuliwa kard. Augustino Richelmy askofu mkuu wa Torino mwandamizi wa Mons. Daudi Rikardi aliyefariki tarehe 20 Mei 1897.. Basi, Richelmy alikuwa mwenzi wa seminari wa Allamano, na kusifu fadhila zake; tena alikuwa mwenye ibada ya kumheshimu sana B. Maria Consolata, alitamani sana kuwa utukufu wake utangazwe kwa mataifa yote.

*Ukurasa 86*

Halafu tendo jingine la Mwongozo wa Mungu, liliyopaswa kuhakikisha mwanzilishi wa Shirika, limekuwa kupata nyumba asili ya kwanza. Karibu na katikati ya Mei 1897, Allamano alikutana njiani na mons. Angelo Demichelis, jamii mkuu katika kanisa la Torino, aliyeanzisha "shirika la B. Maria Aliyepaswa habari" kwa ajili ya wanafunzi wasichana wa chuo cha walimu. Kabla ya siku ile haukuwako ushirikiano wa pekee kati yao, na Allamano alikuwa akimsalimia tu. Lakini yule akasimama na kuanza kuzungumza husisan shirika lake, na kuwa alikuwa na nia ya kulifunga kwa sababu ya matokeo hakuna; na alikuwa akiomba shauri lake.

"Kwa sasa – akamwambia Allamano – endelea bado. Halafu utakapoamua kabisa kulifunga, nitaweza kukushauri la kufanya".

Mwenzake akitaka kujua mara moja, Allamano alimwambia kwa siri mradi wake.

Mwaka mmoja na nusu baadaye, tarehe 23 Oktoba, Allamano aliitwa haraka nyumbani wa Mons. Demichelis ambaye alikuwa mahututi kwa sababu ya kiharusi, na alitaka kumwona. Akaenda, akamfariji, akambariki, halafu alitaka kukaa kando. Lakini mgonjwa, asiyeweza kuongea, alimshika mkono. "Unataka nibaki?".

Akaashiria ndiyo. Akaketi karibu na kitanda; na tazama, mtumishi, akidaka nafasi ya kufaa, akamwekea mikononi fulusi:

"Nina amri ya kukutolea wewe".

*Ukurasa 87*

Wakati ule akaingia mganga na Allamano akaondoka kwenda katika chumba jirani; hapo akafungua fulusi.,. na akaona wasia, naye amekuwa mrithi wa yote. Akishituka sana akarudi kwa mgonjwa:

"Lakini umefanya nini!... mimi siwezi kushughulikia Shirika lako...".

Naye akamshika mkono. Wakamletea karatasi na kalamu ya risasi ili aandike. Mgonjwa akaandika: "Vumilia". Kesho yake, akiendelea kuangaliwa na kan. Allamano, Mons. Demichelis

akaenda mbinguni.

Hatua ya kwanza ya Allamano ilikuwa kumwendea kard. Richelmy kusimulia yaliyotokea: “Amefanya vema! – akajibu Askofu mkuu mtakatifu -. Wangefanya hivi mapadre wote!”.

“Lakini mimi siwezi kuchukua madaraka ya Shirika la Mt. Annunziata...”.

“Kwa sasa kubali, halafu tutaona tufanye nini”.

Kati ya mali aliyorithi ilikuwako nyumba, tuliyosema, ya Avenue Duca di Genova 49 -: itakayokuwa nyumba ya asili ya Wamisionari wa Consolata.

**Mkutano mwingine wa baraka ya Mungu**

Hapo tulipofika katika Allamano huonekana kiasi cha wasiwasi kuhusu sura ya mwisho ya kazi aliyoshika mkononi: ama kuanzisha Shirika jipya – dhana hiyo ya kuanzisha ilimshtusha hasa – ama kurudia dhana ya kwanza ya kuwa kituo

*Ukurasa 88*

kwa ajili ya shirika lililomo tayari. Kama ni hivyo pendekezo lake lilikuwa kwa ajili ya Shirika la Watakatifu Petro na Paulo huko Roma. *(Shirika la Watakatifu Petro na Paulo, Roma, lilijiunga baadaye na lile la Milan, na kuchukua jina la Seminari ya Kipapa kwa ajili ya Misioni za Nje)*

Basi, alipokwenda Roma mwezi wa Aprili 1899 kwa ajili ya mchakato wa kumtangaza Mwenye Heri Cafasso, alikwenda kubisha hodi mlangoni mwa Shirika hilo, akitaka kuongea na Mkuu wao. Lakini hakuwamo, wala mkubwa mwingine ye yote. “Yuko padre mmoja tu aliyerudi toka Uchina ni muda kidogo” – akajibu mgoja mlango.
“Vema, nitaongea naye”.

Alikuwa P. Yohane Bonzano. Allamano akamwelezea mradi wake, naye:

“Hata, la, sivyo. Fanya wewe huko Torino”.

“Shirika jipya, basi?”. “Ndiyo, shirika jingine, binafsi”.

Kwake Allamano ilikuwa sauti ya Mungu, na hapo hakuwa na mashaka mengine tena

Maajabu ya njia za Mwongozo wa Mungu! Miaka kadhaa baadaye Bonzano amekuwa askofu na tena Kardinali wa kwanza msimamizi wa Shirika la Consolata kwa Misioni za Nje!

*Ukurasa 89*

Picha

*Ukurasa 90*

**Kuponya kwa mwujiza**

Kisha kushinda vizuio, na kutoweka mashaka, na kuwa nafasi ya kujikabidhi kutekeleza mradi, tazama, ameugua, na kiasi kwamba amekuwa mahututi.

Ulikuwa mwaka 1900 Januari na ililipuka flu. Tarehe 18 ya mwezi kan. Allamano aliitwa usiku kuangalia mgonjwa mahututi, halafu tena saa za asubuhi mapema alikwenda kumfariji mama mgonjwa, kwenye ghorofa ya darini maskini. Ilikuwa baridi barafu na Allamano alikuwa akisikia dalili ya ugonjwa: kwa taabu alirudi hadi nyumbani.

Ugonjwa mwanzoni ulikuwa laini, na baada ya siku chache imeonekana kwisha. Lakini, tazama, jioni ya tarehe 24, homa ilirudi, na mara hii kwa nguvu sana, hadi kesho yake ilidhaniwa na mara kuonekana wazi kukuzwa kuwa kichomi kikali sana. Madakta waliamua majadiliano ya waganga, na matokeo yalikuwa kutambua kuwa kichomi chenye maji (pleuro-polmonite) pafu la kulia na alama ya kuingilia hata pafu la kushoto. Mara pumzi ilikuwa ya taabu na homa kupanda hadi kupita 40° nyuzi.

Kwa kuongezeka ugonjwa na dalili ya kupata kurukwa akili, waganga walishauri apewe sakramenti za mwisho, zilizotolewa usiku wa tarehe 26. Shughuli za utaratibu na za upendo za waganga, hazikuweza kuzuilia maendeleo

*Ukurasa 91*

ya hatari ya ugonjwa, na baada ya kupishana nyongeza za homa, waganga walimaliza kusema: “Kazi bure! Ugonjwa unaendelea na dalili za hatari zaidi, na hali ya mwili wake hauna nguvu ya kushinda.

Habari ya kusikitisha, iliyotangazwa na magazeti, ilileta karibu na mgonjwa watu wastahifu wa makleri na walei. Wa kwanza wa wote kard. Askofu mkuu, ambaye, akimwelekeza mgonjwa maneno ya faraja, akamwambia:

“Basi, tunafanya nini”.

“Tunakwenda mbinguni...”.

“Na kuanzisha Shirika?”.

“Atashughulikia mwingine...”.

“La. Sivyo, wewe hutakufa. Lazima kuanzisha shirika, na utalianzisha wewe!”.

Kwa wakati huo katika Kanisa la Consolata walianza siku tatu za sala, ili kuomba kutoka kwa B. Maria kisichoweza kupatikana kutoka kwa watu. Ushirikiano wa watu kwa wingi unavutia sana. Waonekana akina mama wakileta watoto wao wadogo, na kuinua mikono isiyo na hatia, kumsihi B. Maria; wazee bado wenye homa kuondoka nyumbani na kuja Kanisani na kushirikiana na umati unaosali; wanaomba katika asasi na mashirika ya watawa mjini, na katika maparokia mengi ya Jimbo kuu.

Sala hizo nyingi na za ari, na baraka ya pekee ya baba Mtakatifu, hazikuweza kuishia bure. Na tazama, kama usiku manane kati ya tarehe 28 na 29 (sikukuu ya Mt. Fransisko wa Sales) homa

*Ukurasa 92*

iliyobaki daima juu ya nyuzi 40°, hushuka haraka chini ya 38° na kubaki pale. Asubuhi, wakati gazeti katoliki lilipotangaza habari fupi ya maafa inayokaribia, kan. Allamano aliondoka salama katika hatari.

Waganga hawakujua la kusema. Kichomi na maji cha mapafu mawili, iliyoanza na kuendelea kwa nguvu sana, na kukatika ghafla siku ya nne, ni jambo la ajabu katika habari za uganga. Na hapo, ikitazamiwa udhaifu wa afya ya mgonjwa, ilipaswa kutambua neema ya pekee kabisa ya B. Maria Consolata.

**“Kwa jina lako nitatupa nyavu”**

Akidokeza ugonjwa huo, kan. Allamano alizoea kusema: “*Msifikiri kuwa kuna ufunuo; wala mimi siutafuti wala siutaki. Nilipokuwa karibu na kufa niliahidi, ikiwa nitapona, sitakawia kuanzisha shirika. Nilipona, na nikashika ahadi*”.

Alikwenda kupumzika Rivoli, ambamo alimwandikia barua ndefu sana kwa kard. Richelmy, na kuuliza: ama kuendeleza Shirika la Mtakatifu Annunziata, namna ilivyo sasa, ama kubadili maelekeo, ama kutumia urithi kwa namna nyingine ya kufaa. Na alirudia kutoa sababu zilizomfanya kuelekea kuanzisha Shirika la Misioni.

*Ukurasa 93*

Kwa upande mwingine hakukosa kueleza, akizipanua, sababu zilizoonekana kumzuilia kuuanza kazi hiyo. Halafu alimaliza: “*Tazama, Mwadhamu, nilichofikiri kukuambia kwa utulivu wa dhamira yangu na kwa utukufu mkuu wa Mungu, tena safari moja. Tafakari jambo mbele ya Bwana na, nitakaporudi Torino, utanipa jibu*”.

Tarehe 24 Aprili, sikukuu ya Mt. Fidelis wa Sigmaringen, aliweka barua altareni wakati wa Misa, halafu akaisafirisha. Inavyoonekana, baada ya ishara nyingi alizopata kutoka kwa Mungu, kan. Allamano, anapoamua kufanya hatua kuu, alitaka kibali wazi ya Mkubwa wake.

Nayo imekuja:

“Eh, - alimwambia Askofu mkuu Allamano alipokuja mbele yake - katika barua uliweka zaidi sababu dhidi kuliko kwa faida ya uanzilishi. Lakini lazima ufanye, kwa sababu Mungu anautaka”.

“Basi, Mwadhamu, kwa jina lako nitatupa nyavu!”.

**Uanzilishi**

Tarehe 12 Desemba 1900 kan. Allamano alipelekea Baraza la maaskofu Subalpino, lililokutana katika mkutano wa Kanda kule Consolata, mradi ya uanzilishaji, pamoja na mwongozo wake, akipata kibali ya wote na sifa ya maaskofu kumi na saba.

*Ukurasa 94*

Tarehe 29 Januari, mwaka kamili baada ya kuponywa kwa mwujiza tulikosema, kard. Richelmy aliyekwisha andika hati muhimu ya baraka kwa shirika linaloanzishwa, alitoa Hati za kulisimika kisheria, na kumweka Mkubwa wa Shirika kan. Allamano mwenyewe.

Kisha kupata kibali, mara wakaifikiria nyumba asili, na kuanza kazi ya kukarabati nyumba ya avenue Duca di Genova. Ilikuwa kazi ya miezi michache. Tarehe 18 Juni ya mwaka huo huo (1901) kard. Askofu mkuu, akisaidiwa na kanoni Allamano na Camisassa, mbele ya watu wengi, aliadhimisha ibada kuu ya kubariki kikanisa na nyumba.

Katika kiota hicho kitakatifu kilikusanyika mapema kikundi cha kwanza cha mapadre wenye nia, ili kupata malezi ya matayarisho yanayotakiwa ya utume, hali Allamano akisaidiwa kwa mafanikio na kan. Camisassa, aliharakisha shughuli kuhusu uwanja wa Misioni wa kuwakabidhi Wamisionari wa Consolata.

Tulisema kuwa lengo la Allamano walikuwa watu wa Galla, alimofanya kazi ya uinjilishaji kard. Massaia. Kwa kusudi hilo yakafanyika mashauri mengi na magumu, lakini yote yamefeli katika bahari ya matatizo kisiasa.

Ulikuwa Mwongozo wa Mungu ambaye akiongoza

*Ukurasa 95*

kwa namna ya ajabu matukio, na kuahirisha kwa nyakati zinazofaa zaidi kiingilio cha Wamisionari wa Consolata kati ya Galla, kwa sasa uliwataka katika nchi iliyo kati ya zilizo bora katika Afrika Mashariki, na yenye utajiri wa matumaini ya kitume, ambamo kazi yao ilihitajika kwa haraka zaidi: Kenya.

Kisha kuamua eneo gani ambapo kuanzisha shughuli yao, walitayarisha safari ya Wamisionari, ambayo ilipaswa kuwa wa watu wachache, kwa sababu ya matatizo ya kuanzisha kazi mahali pasipojulikana na bado wazi kwa ustaarabu. Msafara ulichukua watu wanne. Wawili mapadre: P. Tomaso Gays na P. Filipo Perlo; na mabradha wawili: Cheleste Lusso na Alois Falda.

Ibada ya kuagana ilifanyika mwanzo wa Mei 1902, katika kikanisa cha Shirika, akiongoza kard. Askofu mkuu; halafu tarehe 8 ya mwezi, wenye bahati ya kuchaguliwa waliaga Torino. Alamano alitaka kuwemo wanapoondola. Kuachana kulikuwa uchungu kwa wote. Walilia machozi ndugu wa Wamisionari, na kuliko wote alikuwa akilia na kitefutefu kijana mpenzi, Benedetto Falda, kaka yake Bro. Alois. Allamano alimjongea na kumbembeleza, halafu akimwekea mkono kichwani na kumkazia macho kwa upendo:
“Sasa unalia – akamwambia – lakini baada ya muda si mrefu nawe utaondoka kwenda Misionini”.

Tabiri ikatendeka baada ya mwaka mmoja tu baadaye.

*Ukurasa 96*

**Tukio, huenda pekee...**

Ikiwa Wamisionari wa kwanza waliondoka wengi wakistaajabia, wengine si wachache walijionyesha na kuendelea kutoamini mafanikio ya Kazi; wakamshtaki ya kujaribu yasiyowezekana, na hata kukosa busara kuchagua nchi ambayo watu wake ni wakatili na wa kumwaga damu.
Kwa kuhifadhi zaidi mashtaka hayo na matarajio ya kutisha, Bwana aliruhusu jambo ambalo limekuwa huenda la pekee katika historia ya mashirika ya watawa: tunataka kusema ulegevu uliotokea karibu mara moja na wa pamoja, wa wanaushirika waliobaki katika nyumba asili: ikabaki ukiwa, na Allamano alipaswa kuifunga, kuweka funguo mfukoni na kurudi Consolata. Hapo alijitupa miguuni pa Consolata na kusali kwa moyo:

"B. Maria Consolata, Kazi ni yako, uishughulikie mwenyewe!"

B. Maria akashughulikia. Mwezi mmoja baadaye, nyumba ilifunguliwa kupokea kikundi cha mafrateri wanane, waliofuatwa mara na wengine, na mapadre vijana kadhaa, hata katika muda mfupi ilionekana kama jumuia kamili.

Ili kuvutia zaidi baraka ya Bwana juu ya asasi iliyozaliwa, kan. Allamano siku ya Ijumaa ya kwanza 1902 alifanya rasmi

*Ukurasa 97*

Majitoleo kwa Moyo Mtakatifu wa Yesu, akikiri katika maneno ya kufaa nafasi ile: "*kutoka kwake natarajia kila mema kwa ajili ya shirika, kuja kwa wanaushurika wanaostahili, utakatifu wao, na ari ya kitume katika Misioni*". Moyo wa Yesu aliitika kama kawaida yake, kwa ukarimu wa kifalme. Baada ya mwezi mmoja, waliweza kuandalia msafara wa pili wa Wamisionari kwa Afrika: halafu misafara miwili katika mwaka uliofuata 1903; hali nyumba asili iliweza licha ya kuziba pengo, kuongeza idadi ya wanaushirika wake.

**... na majikatalio nadra sana**

Ili kuvutia kibali ya sifa ya wengi mintarafu Shirika ilifaa sana tukio moja, ambalo, kati ya mengine, linaonyesha roho ya Allamano.
Tarehe 12 Februari 1903 alifariki Torino Abate Alois Nikola di Robilant, baada ya miaka tisa ya ugonjwa wa kuteseka, ambamo wakati wake Allamano alimsaidia kiroho na kufariji kwa huruma yote ya moyo wake.

Alipokwenda kusali Misa katika nyumba ya marehemu, ndugu walimtaarifu kuwa alitajwa kurithi mali zake kadhaa.

"Ah – alitamka Allamano – sikutarajia hayo kamwe!"

Halafu, baada ya dakika ya kufikiri:

*Ukurasa 98*

"Mimi nakataa urithi huo. Msichukie, nimekuja kila mara kwa ajili ya huduma na sitaki waweze kusema kuwa nilifanya kwa faida ya mapato. Misioni zinahitaji zaidi sifa ya jina kuliko fedha".

Akaenda moja kwa moja kwa mwanasheria kuandika hati ya kukataa.

"Safi kweli – alikuwa akirudiarudia kusema mwanasheria – sijawahi kusikia jambo kama hilo!"

Na Allamano akitabasamu:

"Basi, mara nyingine hutaweza tena kusema hivyo".

Hata kard. Richelmy alishituka:

"Imekuwaje, umefanya vile?... Lakini haukuwa kwa ajili yako, bali kwa ajili ya Misioni".

"Ndiyo, Mwadhamu, lakini mimi napaswa kulinda sifa ya Shirika".

Habari ya makatalio hayo – yaliyofanyika wakati shirika lilipokuwa linahitaji zaidi msaada – ilitawanyika haraka, hasa katika makleri, na ni rahisi kuelewa jinsi ilivyosaidia kuongeza heshima kwa Allamano, na pia kwa shirika lake aliloanzisha.

**Unabii wa kard. Cagliero**

Kisha kushinda hivyo matatizo ya kwanza, na kushinda visingizio vingi, shirika limeweza kutembea haraka katika njia ya maendeleo yake.

Tayari mwaka 1905, kwa kusimika kanda ya Kenya kama misioni huru, shirika limepita

*Ukurasa 99*

maisha machanga hadi uhai wa amali wazi, ambayo kibali ya Roma ililipa haki.

Mwaka 1908 uliona kusimika karibu na kazi muhimu, nyingine ya maana sana ya Seminari Ndogo Mt. Paulo, kwa kuwapokea mitume wadogo saba wa kwanza. Mbegu ndogo, iliyomea na kukua haraka, hadi kufikia ukuu usiotarajiwa.

Mwaka 1909 Misioni ya Kenya imekuwa Vikarieti ya Kitume, na P. Filipo Perlo Vikar wa Kitume. Kuwekwa wakfu Askofu ya kwanza wa Shirika – katika Kanisa la Consolata, tarehe 23 Februari 1909, kuliandamana na kuzindua nyumba asili mpya katika avenue Ferrucci: jumba kuu lililojengwa katika eneo la mita mraba 8.000.

Gharama ya jengo ilikuwa kubwa sana na Allamano alitumia yote yake. Lakini haikuwa shauri la fedha kumhangaisha. Alikuwa na shaka moja tu kwa muda fulani, kutokana na unyenyekevu wake mkuu: na alimwambia kardinali Prefekt ya Propaganda Fide, ambaye alimwuliza habari hususan nyumba mpya:

"Naogopa kuwa injinia alifanya ramani kubwa mno... sijui kama tutaijaza".

"Naam, mwachie tu – akajibu kard. Gotti – tusifungie mikono Mwongozo wa Mungu!"

*Ukurasa 100*

Vile alikuwa akimtilia moyo kard. Cagliero, mwanakijiji mwenzake na rafiki sana wa Allamano:

“Kanoni, uipanue zaidi nyumba!”

“Lakini nakuambia kuwa naogopa kuwa ni kubwa mno..”

“Panua zaidi, panua zaidi!”

Na kard. Cagliero alikuwa nabii. Nyumba asili mpya baada ya muda mfupi haikutosha, hata kupaswa kuondoa Seminari Ndogo, na halafu hata Novisiati, na tena baadaye kuongeza maghorofa, na tena haikutosha kwa mahitaji.

Tutaongeza kuwa Desemba 28 mwaka ule ule (1909) Kiti Kitakatifu kimetia muhuri msimamo wa Shirika kwa njia ya Hati ya *Decretum Laudis*.

**Masista Wamisonari wa Consolata**

Toka mwanzoni mwa utume, Wamisionari wa Consolata walisisitiza sana mbele ya Mkubwa wao kuwa ilidaiwa sana kupata msaada wa kazi ya Masista: kwa ajili ya kazi nyumbani vituoni mbalimbali; na kwa ajili ya matibabu hasa kwa wanawake; na pia kwa ajili ya vituo vya watoto yatima, chekechea, bweni za wasichana, shule, katekisimu na kazi nyingine ndogo ndogo.

Allamano alimwendea Mkuu wa Nyumba Ndogo ya Mwongozo wa Mungu, P. Ferrero,

*Ukurasa 101*

ambaye kwa hiari alikubali kutoa msaada kwa wana wa Consolata Mabinti ya Mt. Vinsent de Paul. Mwezi wa Aprili 1903 waliondoka Torino kikundi cha kwanza cha Masista wanane wa Mt. Vinsent, waliofuatwa baada ya miezi michache na wengine kumi na mbili, na wengine tena baadaye kufuatana hadi kufikia idadi ya hamsini.

Lakini kwa sababu ya kuhitaji daima idadi kubwa zaidi kutokana na maendeleo ya Misioni, wala isiweze Nyumba Ndogo kuvumilia ziada ya sadaka ya watu, Allamano alijikuta mbele ya suala la kuamulia haraka. Katika mkutano na Baba Mtakatifu Pius X, mwaka 1909, alimwelezea jinsi ilivyokuwa hali ya mambo, na shida ya kupata masista kutoka kwa Mashirika kiasi cha kutosha kwa mahitaji ya Misioni.

“Lazima –akamjibu Baba Mtakatifu – wewe mwenyewe uanzishe shirika la Masista Wamisionari, jinsi ulivyoanzisha la wamisionari”.

“Baba Mtakatifu, kuna tayari mashirika mengi ya masista”.

“Naam, lakini siyo ya Misioni pekee”.

“Lakini, Baba Mtakatifu mimi sina wito wa kuanzisha masista”.

“Kama huna, nakupa mimi”.

Matakwa ya Baba Mtakatifu kwa Allamano yalikuwa mapenzi ya Mungu, na akaanza kwa nia thabiti taabu mkuu mpya. Akikumbuka mazungumzo hayo na Baba Mtakatifu, alikuwa anawaambia masista:

*Ukurasa 102*

“Mnaona? Si mimi niliyewataka, bali Baba Mtakatifu. Lazima ninyi mwe wa “Kipapa” zaidi kuliko masista wengine”.

Tarehe 29 Januari, 1910, nyumba ya Avenue Duca di Genova, iliyokuwa zamani nyumba asili ya Wamisionari, ilifunguliwa tena na kuwa nyumba asili ya Masista Wamisionari wa Consolata. Tarehe 5 Aprili waliingia wapostulanti sita wa kwanza, ambao nao yalianza maisha ya Shirika. Mwishoni mwa mwaka ule walikuwa yapata ishirini. Tarehe 21 Novemba ya mwaka ule 1910 ilifanyika ibada ya kupata mavazi watawa wa kwanza; Aprili 5, 1913 nadhiri za kwanza; na Novemba 3, 1913 msafara wa kwanza wa Masista wa Consolata Misionini.

Mwaka wa 25 tangu kuanzishwa Shirika, idadi ya Masista Wamisionari wa Consolata ilizidi 500, ambao 300 Misionini.

**Kutanguliza nyakati**

Inawezekana kusema kweli kuwa Allamano kwa kuanzisha Mashirika mawili ya Wamisionari alipenyeza macho yake katika nyakati za baadaye: yaani alitangulia kuona mwendo ule wa Kimisioni uliopaswa kuamka Italia baadaye, na kutoka Italia kuenea hadi ulimwengu mzima Mkatoliki.

Tunaongeza kuwa Allamano alitoa mchango wake, kwa njia ya utangulizi wa kuthubutu:

*Ukurasa 103*

kuyakusanya Mashirika ya Kimmisionari ya Italia kwa ajili ya tendo la pamoja la kujieleza kwa njia ya ombi kwa Baba Mtakatifu, ili kuomba aandike Waraka Ensiklika kuhusu Misioni: iwe wito kwa Wakatoliki kupata ufahamu zaidi ya suala la Misioni, na wajibu wa kushirikiana.

Mwezi Agosti 1012 Allamano kwa kusudi hilo aliwaandikia waraka Wakuu wa Mashirika mbalimbali, na wote walionelea muhimu tendo hilo, na kwa umoja kumwamisha Allamano mwenyewe jukumu ya kuandika ombi. Barua hiyo alipewa Baba Mtakatifu mwezi Desemba mwaka ule.

Pius X, katika tarehe 31 Januari 1913, alijibu kwa wema kwa njia ya hati ya hadhara, ambayo isipotekeleza kikamilifu matakwa ya waombaji, lakini ilikuwa sauti ya kwanza ya mlio, ambao baada ya miaka michache, kwa njia ya Benedikti XV na Pius XI, ilipaswa kupiga mbiu kwa nguvu toka ncha hii ya dunia hadi ncha hii.

Mintarafu mtazamo huu wa kutangulia wa Allamano, tuna ishara nyingine katika jambo la Prefecture Apostolic ya Kaffa (leo [1938] Vikarieti ya Gimma), ilioongezeka baada ya ile ya Kenya. Kwamba hii ilikuwa ndoto ya Allamano toka mwanzoni, tulisema mara kadhaa. Kwamba yaliongezeka matatizo mbalimbali daima, Allamano hakupoteza matumaini au kuacha mradi wa

*Ukurasa 104*

kutuma Wamisionari wake kwenye nyayo za Massaia. Na tazama, baada ya miaka 12, kutekelezwa tamaa yake kali.

Historia ya Prefeture ya Kaffa, inayohesabu matendo ya ushujaa yasiyojulikana, itabaki kuwa ukurasa ulio mzuri sana katika habari za enezo la imani.

**Mkuu wa Shirika**

Kan. Allamano, wakati wa maisha yake, alikuwa pia Mkuu wa mashirika mawili aliyoanzisha, ijapo ukuu huo ulikuwa mzigo mzito kwake, aliyetaka na kuomba mara nyingi, kuondolewa nao. Hisia hiyo ya wajibu, licha ya kutaka kuuacha mzigo, ilimfanya kujitahidi zaidi kutekeleza kwa makini wajibu wake wa Mkuu, aliofupisha katika maneno matatu: kusali, kuangalia, kuonya.

*Ukurasa 105*

Picha

*Ukurasa 106*

Kwa sababu ya wadhifa wake wa Rekta wa Kanisa na wa Chuo wa Consolata – asiweze kukaa katika nyumba asili, alimweka wakili wake Kiongozi. Kwa kweli, lakini, kazi yake Kiongozi ilikuwa kuangalia nidhamu, hali uongozi wa kweli na malezi ya wanafunzi zilikuwa kazi za Allamano. Naam, hakuacha kitu kwa ajili ya kuwalea wanafunzi katika roho ya Shirika, ambayo ilikuwa roho yake mwenyewe.

Ili kugusa kanuni kadhaa ya msingi ya jumla, tutasema kuwa yeye alikuwa anakwenda polepole kupokea maaspiranti. Aliogopa idadi, kwa hofu ya kuwa hasara ya malezi ya wanafunzi binafsi. Alipokea na kurudia kusema fasuli ya kard. Vives, Prefekt wa *Propaganga Fide*: "Hutakiwa mlango mwembamba na mlango mpana". Mlango mwembamba wa kupokea, na mlango mpana kwa kuwarejesha.

Kwa askofu, aliyewahi kuwa mwanafunzi wake, aliyemwandikia ili apokee frateri mmoja, Allamano akamjibu: "*Ukisikitika kumwacha, mlete; la sivyo, msike mwenyewe*".

Toka kwa wanafunzi alidai kwanza: nia njema. Aliyewahi kuingia katika shirika na lengo tofauti la kutaka kuwa Mmisionari wa Consolata, ajue wazi "*kuwa mzushi na kupaswa kutoa hesabu kwa Mungu, kwa Nyumba na kwa wafadhili*".

Basi, heshima kuu kwa wito – tusidhani tumemfadhili Mungu kufuata

*Ukurasa 107*

wito wa Mungu, bali ni kipaji cha upendeleo upande wa Mungu –; na kwa hiyo: kuitika kikamilifu, ukarimu na kwa moyo. Kuitika wito, maana yake kuitikia lengo la Shirika, lililo "*kwa wanaushirika kuwa watakatifu na uongofu wa wapagani*". Basi, kwanza kuwa watakatifu wenyewe, halafu roho za watu. Aidha, "*utakatifu, unaozidi ule wa Wakristo wa kawaida, unaozidi ule wa watawa, bora zaidi ya ule wa mapadre wa jimbo; na utakatifu, ikitakiwa, shujaa hata kutenda miujiza"*. Ndiyo dhana kimsingi wa mafundisho yote kiini cha kiasketi ambayo Allamano aliwapa wanafunzi wake wamisionari.

Njia ya kwanza na muhimu ya lazima isiyoepukika ili kutekeleze lengo hilo kuu: ibada. Tutaongea baadaye. Hapa tunakumbusha tu kuwa kanuni Allamano aliyowapa wakubwa wasaidizi wake, kuwa: "*usikate tamaa kuhusu kijana, hata akielekea makosa mara nyingi, bora awe na ibada; lakini kutilia mashaka kuhusu yule asiyependa ibada, ijapo ana vipaji bora vyo vyote vile*". Mang'amuzi yake marefu ya mlezi wa mapadre vijana yalimhakikishia kuwa "*wanaofeli, wengi wao ni kwa sababu hawaitikii neema, na hiyo kwa sababu ya kukosa ibada*". Alilalamikia kuwa hata seminarini mara nyingine kuna "*kizuio kati ya shule na kanisa, kumbe somo, mbali ya kukausha ibada, lazima iihifadhi*".

*Ukurasa 108*

Kwa upande mwingine, somo linalotakaswa hivyo na ibada, aliliweka karibu nayo na katika mstari ule wa kuhitajika katika malezi ya mwanafunzi mmisionari. Alitumia maneno makali na karibu kukasirika kwa upande wa wale waliokiri: kutosha kwa mmisionari elimu hafifu na vipaji visivyo bora. "*La. Sivyo* – alikuwa akitamka – *sivyo. Mmisionari lazima awe namba wani katika*

*fadhila na elimu*". Zaidi alikuwa na hakika ya kuwa mmisionari alihitaji elimu pana na ya kina zaidi kuliko mapadre wa kawaida, kwa sababu mmisionari akipatikana katika matatizo makubwa zaidi, mara nyingi hana nafasi na muda wa kupekua vitabu au kuomba ushauri. Kwa hiyo alikuwa mkali kuwafukuza wanafunzi wale, waliojionyesha hawana uwezo tosha au wavivu katika masomo.

Sehemu ya kukamilisha malezi ya mtume ilikuwa, kadiri ya mafundisho ya Allamano, kazi ya mikono. Naam aliweka namba katika Katiba: "*Kwa kufuata mfano wa Mtume Mt. Paulo aliyejipatia riziki kwa njia ya kazi ya mikono, wamisionari watajitahidi hata katika kazi ya mikono, na ili wafanikiwe, watajitahidi kujizoeza katika ufundi na maarifa zinazofaa mahali pa Misioni*". Basi, katika nia ya mwanzilishi, kazi ya mikono ilipaswa kuwa mazoezi ya umaskini na pia njia ya utume.

Kati ya fadhila zake mwanafunzi mmisionari alisisitiza hasa mbili: kujitenga na utashi wake mwenyewe

*Ukurasa 109*

kutoka kwa raha, kutoka kwa ndugu; na kwa nguvu: "kwao utashi nusunusu, ambao leo ni motomoto, na kesho hakuna kitu, kwa wazembe ambao huenda hawasumbui wakubwa lakini hata hakuna faraja, kwa waoga na wadhaifu, kwa wasioridhika kamwe daima, kwa wasingiziaji wasiojisahihisha, kwa hawa wote hakuna uwezekano kwa kupata malezi ya kufaa, hakuna matumaini ya kazi ya mafanikio misionini. Basi kwao mlango ule mpana akiwa bado wanovisi, au kama walikwisha weka nadhiri, kuwaweka kando, kama zana zinazosumbua.

Katika kazi hii ya malezi yanachukua nafasi muhimu mazungumzo ya kiroho ya Allamano. Ilikuwa siku ya Jumapili alasiri na sikukuu nyingine. Zungumzo la kwanza lilikuwa kwa ajili ya Masista, halafu alipita kwa Wamisionari. Hata iwepo mvua, upepo au theluji, alikuja tu, asijali afya yake hafifu.

Mada ya mazungumzo yake zilikuwa fadhila zote hasa kwa namna ya pekee yahusuyo padre, mtawa na mmisionari; halafu pia liturjia, sikukuu za Kanisa, Injili au Waraka wa siku. Hayakuwa mambo ya ajabu aliyosema, na aliyasema kwa urahisi wa mazungumzo, lakini mafundisho makubwa, kwa hakika, na kukolezwa na Roho hasa! Alikuwa hachoshi kamwe, hata ikiwa mazungumzo yalidumu zaidi ya saa, jinsi alivyoweza kukoleza na mifano au kugusa matukio au makumbusho ya binafsi. Tutaongeza tu kuwa miniti za mazungumzo yake zinachukua madaftari kumi na sita ya maandiko membamba sana yamejaa.

*Ukurasa 110*

Malezi ya wanafunzi yaliongezewa na mazungumzo binafsi. Kila mara alipokuja nyumba asili, Rekta alikuwa tayari daima kupokea ye yote aliyetaka. Lakini hata pale Consolata chumba chake kilikuwa wazi kwetu sisi kila saa. Haikutokea kuwa amekataa kupokea, au kuonyesha ishara yo yote ya usumbufu. Kutoka kila mkutano naye mtu alitoka na furaha moyoni, na moyoni kitu kilichomsukuma kwa upendeleo, lakini kwa nguvu isiyozuilika, kwa ukamilifu.

Isipowezekana kumwendea mara nyingi mmoja alivyotaka, mazungumzo binafsi yalibadilishwa na maandiko. Kila mwanafunzi alikuwa huru kabisa kumwandikia na kutuma

maandiko kadiri alivyotaka. Halafu yeye alikuwa akijibu kwa sauti, au mara nyingi zaidi akiandika chini ya barua aliyopata. Hata mistari michache, lakini ya kufikia lengo daima.

Imani yetu kwake ilikuwa kamili, lakini huru kabisa; hakuidai, wala amekubali wengine kufanya hivyo. Alivutia kwa utakatifu wa maisha yake, kwa upendo wa kibaba, kwa upendo mkuu alivyotupenda. Hayo yamejulikana kutoka kwa macho yake mema, tabasamu laini ya daima, sauti ya kupendeza, na kumwona kufurahi kuwa kati yetu. Lakini hasa ilionekana katika matukio ya uchungu: kifo cha mwanaushirika, kama vile kwa kuondoka kwenda Misionini. Huwezekanaje kusahau tamasha ya kuagana kati ya Baba na wana,

*Ukurasa 111*

steshenini, dakika chache kabla ya kuondoka? Kukumbatiana mara ya mwisho na busu ya kibaba kwa kila mmoja walioondoka? Halafu baraka ya mwisho kwa kikundi hicho pamoja na wanaushirika na ndugu waliopiga magoti miguuni pake? Uso uliopayuka, majonzi ya sauti yake, macho yenye machozi yanayoelekea mbinguni, jinsi tulivyotambua kuwa wana wamisionari walikuwa kweli wapenzi wake pekee, jinsi Shirika lilivyokuwa mboni ya jicho kwake! Jinsi tulivyohisi ukweli wa maneno alivyosema: "*Kila mara kuna safari hizo, moyo huteseka, hasa moyo wangu. Ni kama kujitenga na sehemu ya nafsi yangu mwenyewe. Ikiwa ni majonzi kwa wote, kwangu mimi, nakiri wazi, ni maumivu na maumivu!*". Na pia ukweli wa maneno mengine aliyotamka: "*Bwana angaliweza kumchagua mwingine kuanzisha shirika: mtu mwenye uwezo zaidi, mwenye afya zaidi, mwenye vipaji zaidi, lakini mmoja wa kuwapenda zidi, sidhani!*". Ama: "*Ijapo ndugu wanawapenda kwa upendo unaoonekana kubwa zaidi ya mimi kwenu, lakini kwa kweli sivyo, hata kidogo*!".

Ni wazi kuwa kwa upendo mkuu wake wa kibaba ulilingana na upendo wetu wa wana. Daima tulimpenda kwa uwazi wa mshangao. Na licha ya kutopunguka kwa kuondoka kwake na kwa miaka kupita, daima unaongezeka katika heshima yetu kwa sura ya Mwanzilishi mtakatifu.

*Ukurasa 112*

**Ndugu wa wamisionari**

Upendo ule wenye uangalifu, namna ile ya kujali kwa wema, alitumia kwa ndugu wa wamisionari, aliyewaita "wafadhili wa kwanza". Aliwapokea kwa wema mno na kuwatendea heshima kubwa, mtu asiweze kufanya zaidi.

Siku moja mwanafunzi fulani, kwa aibu kidogo, aliomba kumjulisha kaka yake na mke wake ili awabariki, Baba mwema licha ya kukubali, alijitahidi kuongeza zawadi kwa ajili yao, na kuchagua medali mbili za fedha, za kisanaa, za B. Maria Consolata, na nyuma yake alichapisha tarehe ya ndoa yao. Kwa mwingine aliyekuwa anakwenda nyumbani kwa ajili ya sherehe ya familia, alimpa chupa ya divai bora ya kuwapelekea zawadi. Matendo hayo ya heshima na wema yalikuwa wa daima.

Kwa kifo cha wazazi wa mmisionari, Allamano alijichukulia kazi nyeti ya kutaarifu kwa kumwambia mwenyewe, au kwa maandishi, habari ya uchungu kwa mwanao, na maneno yake yalikuwa daima ya faraja ya kulainisha donda lililotoka damu. Aidha, hakuacha kuwapelekea

rambirambi yake binafsi kwa familia yenye msiba. Hata katika Katiba aliingiza sehemu kuhusu kuombea rehema kwa ajili ya wazazi wa wamisionari, katika jumuia.

*Ukurasa 113*

**Kichwa ngumu wa namna yake**

Iliwahi kutokea kuwa hata wazazi walipinga wito wa mwana, na baada ya mazungumzo naye walitoka wametulia na hata kubadilika. Hapo hupendeza anachoandika P. Gallea, leo (1938) Mhasibu mkuu wa Shirika:

"Nilikuwa nimepeleka ombi la kupokelewa na nikapokelewa. Mama yangu, alipojulishwa hakutaka kabisa kwa vyo vyote, na alipoona kuwa ameshindwa kunishtusha, alijaribu njia ya mwisho. Siku iliyopangwa nijionyeshe kwa kan. Allamano, alitaka kunisindikiza. Tuliingizwa katika sebule mojawapo ya wageni ya Chuo cha mapadre, na baada ya dakika chache za kungoja, tazama, kuonekana, akitabasamu, kanoni Allamano. Alitustarehesha na kuanza mazungumzo. Sikuongea sana siku ile; aliongea mama, ambaye alianza porojo ya hoja zote alizokuwa nazo moyoni alizotayarisha. Kan. Allamano alimwachia kusema, halafu kwa maneno machache alijibu kiasi kwamba mama alipaswa kutafuta hoja nyingine. Ila aliponiuliza ikiwa mimi naingia kwa hiari na kuweka bidii, nikajibu kwa silabi moja tu.

Nakumbuka kuwa, kati ya hoja nyingine, mama alieleza mahangaiko ya nyumbani (yalikuwa ya kweli) na aliomba ikiwa, kwa kunipokea, angaliweza kuahidi msaada kwa familia. Kanoni alijibu

*Ukurasa 114*

"Nyumba yetu haiwezi kujichukulia masharti kwa familia, anayejichukulia ni B. Maria Consolata".

Karibu na mwisho wa mazungumzo, mama, akiona uhafifu wa hoja zake, alinielekea mimi akikasirika na kusema:

"Lakini, basi, kama ilikuwa nia yako, ungaliweza kutuambia kabla ya kufanya madeni!".

Nikainama kichwa kwa aibu. Kanoni akaingilia mara:

"Mlifanya madeni? Kiasi gani?"

"Nadhani zimebaki Lira mia mbili ya karo ya kulipia seminarini".

"Nitashughulikia mimi" – akasema Allamano.

Mama hakujua la kusema tena, akaanza kulia machozi.

"Haya, haya... jipe moyo... utaona kuwa utafurahi. Tena mwana hajajaribu maisha ya Shirika na atakuwa huru wa kurudi nyumbani.

"Eh! – alikatisha mama kwa nguvu – huyu, shingo ngumu?! Hawezi kubadili, hawezi kubadili kamwe!".

Kwa porojo hilo Allamano akacheka kwa moyo, halafu baada ya maneno mengine mazuri, alikubali anipe karo kiasi alichoweza kutumia.

Kisha kufika nyumbani, baba akamwuliza, yamekwendaje. Naye akajibu:

“Kazi bure!... alijibu jinsi usiyeweza kujibu neno. Kati ya mapadre wetu na yule kuna tofauti ajabu!...”.

*Ukurasa 115*

**Mwongozo wa utume**

Ni jambo la ajabu jinsi kan. Allamano, bila hata kuona nchi ya Misioni, lakini alijionyesha kuwa na mang’amuzi ya hali ya juu kuongoza kazi ya uinjilishaji katika nchi za kiupagani, hata kuhusu vifaa, mfumo na kupanga. Miongozo ya utume ilitolewa katika Nyaraka kwa wote kwa Wamisionari Afrika. Tunatoa vichwa vyake.

Kama msingi wa utume, jinsi tulivyosema kuhusu malezi ya utume, Allamano aliweka utakatifu wa wamisionari: “*Mnapaswa kufikiria utakatifu wenu. Sio kwa sababu ya kidunia mmekuja Afrika, bali kwa ajili ya kuwa watakatifu zaidi tu, na hivyo kuokoa roho nyingi”. Akawaangalisha dhidi ya “uzushi wa utendaji*”: kusadiki kuwa utume unakaa hasa, au vibaya zaidi utimishwe katika kufanya mambo makubwa kwa hasara ya utakatifu wenu. Kati ya vifaa vya utakatifu, anashauri: mazoezi ya roho ya mwaka, mfungo wa mwezi, na uaminifu mkali wa mazoezi ya ibada, kupenda kuvaa vazi la kitawa.

Ili kutokeza matunda makuu iwezekanavyo, anahimiza kwanza umoja wa maelekeo: “*Kazi yenu lazima iangazwe kuhusu mfumo wa kufuata*”. Nalo kwa sababu utume ni mapambano, na kwa kushinda haitoshi ujasiri, wala kuwa na vifaa na watu, huhitajika mfumo na mpango.

*Ukurasa 116*

Basi anaamuru mikutano ya mwaka, wakati wa mazoezi ya roho, “*ili kutafuta na kupanga kwa nia ya pamoja kanuni za maisha na ya utendaji wa kitume, ambazo mang’amuzi yalishauri yanayofaa zaidi kutekeleza lengo la wote*”.

Kwa umoja wa maelekeo lazima huafikiane umoja wa utendaji kwa upande wa walio chini: “*Asiyeweza kujikana kuhusu maoni yake binafsi na kukubali ya wengi, na zaidi yale ya wakubwa, anafanya kazi bure, na huenda ataharibu mema waliyotenda wengine*”. Kwa hiyo sharti ya lazima kabisa kwa ajili ya kazi linganifu ni utii. Ndiyo fadhila *magna* (kuu) katika roho na mafundisho ya Allamano. Katika barua zake zote hakosi kuitaja; na baada ya kuitangaza katika Katiba “*fadhila ya kimsingi ya Shirika*”, anaitangaza pia “*ya kimsingi kwa kazi yoyote ya faida na ya kudumu ya kitume*”; akikiri: “*Mabadiliko ya kiraia na kiroho ya watu hawa yatatokea, mniamini, polepole au haraka, zaidi au pungufu kwa upana na kwa kina, kiasi kadiri kila mmoja katika wadhifa yake atakuwa mfano wa utii*”.

Ijapo utii hautoshi kuufikia umoja mkamilifu wa utendaji katika utume. Ni lazima pia kuwa wamisionari wategemeane. Wakiunganika na wakubwa kwa njia ya utii, lazima waunganike kati yao kwa njia ya upendo wa kidugu. Wasia Allamano aliyowachia wanae waliosafiri ilikuwa sawa, na ile ile kwa wote: wapendane kati yao. Kama wasia ya Yesu.

*Ukurasa 117*

Akawaonya: “*Angalieni, kwa sababu siku, yataanzapo masengenyo ya ninyi kwa ninyi, itadhihirisha utasa wa kazi yenu, na kuwa mwanzo wa uharibifu wa Shirika*”.

Akiandika hivyo miongozo ya kazi ya umoja na ya mpango, Allamano aliwapa nafasi wamisionari wake kukamilika katika roho ya kitume, iliyo hasa roho ya sadaka. Naam, ari haimaliziki katika sala na utendaji. Maneno yake kamili zaidi kuhusu kuongoa roho za watu, ni sadaka. Allamano alihamasisha na kutegemeza wanae katika njia hii ya sadaka: katika majikatalio yanayodaiwa na maisha ya kitume, na pia katika majaribio yanayodhihirisha kazi za Mungu. Lakini aliongeza: “*Ikiwa mateso yanafaa kwa ajili ya utukufu wa Mungu na faida yetu, mimi naomba kuwa mateso hayo yatoke kutoka katika ulimwengu, toka nje ya Shirika, sio ndani na wanaushirika wake, kwa kukosa fadhila za pekee za hali yetu*”.

Kati ya majaribio, moja lililo kali zaidi na la hatari ni kukata tamaa mbele ya utasa wa kweli au wa kusingizia tu, wa taabu za kitume, unaotokea daima mwanzoni mwa Misioni. Alikuwa akitangulia kuwaangalisha kwa neno lake jema na lenye madaraka: “*Awali ya yote, si kweli kwamba matunda yaliyotokea ni haba sana. Shukrani kwa Mungu, mapato ni makubwa na, nasema ukweli,*

*Ukurasa 118*

*zaidi kuliko nilivyotarajia. Matunda hayo hayaonekani yote kwenu, kama vile mama aliye na mtoto daima mbele ya macho yake, hatambui kukua kwake kwa kimo; lakini yamo tayari... Halafu mnasahau kuwa kila mmoja atapewa tuzo* secundum proprium laborem (*kadiri ya kazi yake*) *wala sio kadiri ya matokeo aliyopata*”. Allamano alikuwa akiona ukweli. Utasa wa miaka ile ya mwanzoni ilikuwa kisingizio tu: iliyoukuza machoni mwao wamisionari, ilikuwa ari yao yenyewe. Lakini mbegu ya Mungu ilimea *tempore opportuno* (*wakati wake*), na leo ni mti unaositawi.

Kuhusu mahusiano kati ya wamisionari na wenyeji, miongozo ya Allamano inaweza kujumlishwa katika neno moja: upole. Maonyo yake yahusu yanadhihirisha upendo wake mwororo wa kibaba kwa wana wale maskini. “*Wapendeni, watendeeni kwa adabu, bila kupoteza uvumilivu wasipoitikia matakwa yenu*”. Safari moja tu tangu mwanzo wa Shirika hadi kufa kwake, tunaambiwa kuwa kan. Allamano alitumia hati ya kuamuru kwa madaraka ya utii takatifu, na imekuwa katika jambo hilo; kuwakataza wamisionari kuwatendea vibaya wenyeji.

Kwa njia ya miongozo hiyo, na neema ya Mungu, wamisionari wa Consolata walivuna mapato makubwa. Kwa kutii kiaminifu miongozo hiyo mavuno yatakuwa daima maridhawa.

*Ukurasa 119*

# 3.
# Roho
# ya mtume

*Ukurasa 120*

“... Kwako, ambaye huonekana kuwa Mjomba wako stahiki Yosef Cafasso amekuachia mrithi wa roho yake heri na matakwa Yetu, pamoja na kukutakia kuwa yanayobaki ya maisha yako yatumike kupatia Kanisa mafanikio makubwa, kwa njia ya ari uliyo nayo.

Pius Papa XI

*(katika Jubile ya*

*kan. Y. Allamano)*

“...Neema ngapi umepewa, lakini bado tena jinsi uliyotolea wakati huu kwa kazi na mastahili!”

Card. Gaetano De Lay

“... Daima nilishikwa na hisia za heshima ya kina na adabu kwa mpwa wa M. Heri Cafasso”.

Kard. Andon Vico

“... Fadhila, ari na Bwana zimekuweka juu ya kinara cha Kanisa la Torino”.

Kard. Yohane Cagliero

“...Ni wengi wanaokufahamu, kuheshimu na wanapaswa shukrani kwake, ambaye katika maisha yake ya kiupadre anatukumbusha Mjomba wake M. Heri”.

Kard. Gaetan Bisleti

“.. Padre stahifu, ambaye curriculum vitae (*mwendo mzima wa maisha*) inadhihirishwa kutokana na tabia iliyo pekee ya kazi zilizoongozwa na Mungu, yaani mapato na ukuaji”.

Kard. Mikael Lega

*Ukurasa 121*

Picha

*Ukurasa 122*

**Mtu mkamilifu**

Kan Allamano alifanana na Mjomba Mt. Yosef Cafasso, hata kwenye kilema la bega la kushoto kushuka mbele ya la kulia, lakini bila kuharibu sura. Tulidokeza tabia ile nyingine ya wote wawili: usafi wa macho, na mwangaza wa mtazamo, uliopenya kuchunguza siri za ndani.

Ni kweli kwamba Allamano aliweza kushika ustahi uliompasa. Alijali utaratibu wa nafsi "toka ncha ya viatu hadi ncha ya nywele" alivyozoea kusema Cafasso. Alipenda sana usafi, kama vile alichukia fahari. Kamwe aliacha vazi kwa sababu limechakaa au kuchafuka: kwa kawaida alibadili ili kupata nafasi ya kumfadhili mtu. Saa ile moja, aliitumia maisha yake yote: rozari alitumia zaidi ya miaka thelathini, bila kuhitaji matengenezo: madaftari na vitabu – kuanzia madaftari ya Middle school aliyotunza sana – ni ishara ya bidii nadra kabisa.

Aliorodhesha kabisa maisha yake binafsi aliyoshika kwa uaminifu wa dhati.

*Ukurasa 123*

*Age quod agis* (fanya vema unachofanya) ilikuwa kanuni aliyopenda zaidi; na hivyo alipata nafasi kwa yote.

Katika mahusiano wa majirani alikuwa na heshima kamili. Mwenendo wake ulikuwa wa adabu na stahifu. Ijapo alizaliwa na wakulima wa kawaida, hakupata shida kujimudu – na imekuwa mara nyingi – na Wafalme, Wana Mfalme, na Mabinti Mfalme, na watu Makabaila wa Torino.

Aliona fahari kuwa Jumuiya alizoongoza, zijulikane kwa njia ya kushika sheria za maisha ya kiraia. Ilipotokea kuchagua masista kwa ajili ya Chuo cha mapadre, aliwakataa aliopendekeza kard. Alimonda, kwa sababu alitambua alipowatembelea nyumba asili kwa muda mfupi, makasoro fulani kuhusu jambo hilo. Hakuvumilia chochote kilichokuwa kinyume cha adabu, hadi kufukukuza shirikani wasiojisahihisha: alikuwa akisema:

*"Kutokuwa na adabu njema maana yake kutarajia yaliyo mabaya zaidi".*

*"Ninyi mnakuwa na mnapaswa kuonekana hata katika mambo hayo wajumbe wa kweli wa Yesu".*

*"Mnapoanzia na neno lisilo la adabu njema, mnaishia kukosa upendano".*

*Jumuiya zilizo na adabu njema, wanaweza kupenda zaidi".*

*"Hata, haitoshi kuwa na fadhila, lazima kuionyesha kwa adabu njema. Sio porojo, bali kujimudu vema".*

*Ukurasa 124*

Mwendo wake haukuwa na makasoro na wenye heshima, hata mbele yake mtu asiweze kujiruhusu yasiyo ya adabu hata kidogo. Mazungumzo yake hayakuwa na ulaghai. Hakutumia maburudisho, wala mialiko karamuni. Isipokuwa kwa ajili ya huduma, hakutembelea nyumba za familia binafsi: akiendea kwa wajibu, alibaki muda wa huduma, bila kukubali kupokea kitu

chochote.

Aliishi upweke. Aliishi zatika ukimya na utaratibu, zaidi ya miaka arobaini, kati ya Kanisa la Consolata, Kanisa Kuu la Jimbo na Shirika la Misioni. Na hakuwahi kutangua kanuni hizo hata wakati wa likizo ya wakati wa joto.

Unyeti wa hisia yake ya kiroho ilimfanya awe na shukrani sana. Alishika moyoni kwa muda mrefu sikitiko, kwa sababu hakuweza kumshukuru kwa sauti mtu aliyemtolea msaada, ijapo alimpa malipo. Wafadhili wa maisha yake hakuwasahau kamwe, akianzia wazazi, baba na mama wa ubatizo, n. k.; aliwaombea wote kila siku.

Wafadhili wa Shirika aliwatendea kiupendeleo. Alikuwa akisema: "*Mwe na shukrani kwa wafadhili wote, wa zamani na wa sasa. Kumbukeni kuwa tuliyo nayo hutokana na sadaka zao, na za wengi ni sadaka zisizosemeka*". Na akidokeza orodha ya fadhili zilizotangawa kwenye gazeti la Misioni: "*Mimi nasoma kabla na baada ya kuzitangaza, na natumia kwa kutafakari. Sadaka zile ni machozi, ni damu iliyomwagika! Mara kwa mara*

*Ukurasa 125*

*naelekeza dua kwa Mungu na kuwaombea watoleaji*".

Akisema hususan ishara za shukrani, alikuwa akisema: "*Ni wajibu tusioweza kusahau, ni heshima tunayopaswa sisi kwa sisi, ni wema unaoonyesha ilivyo tabia ya mtu.* Oportet impleri omnem justitiam *(lazima kutimiza kila haki), hata katika mambo hayo*".

"Nakumbuka – anasema kan. Dalpozzo, pro-vicar, na aliyekuwa mwungamishi wa Masista wa Consolata – kuwa Allamano aliweza – jambo lililo la wachache – kuoanisha kosa au upungufu wa malipo aliyojiamrisha mwanzoni mwa jumuiya ya kiutawa, na ishara malidadi za shukrani. Mara nyingine ilikuwa sanamu ndogo, kahawa toka Misioni; mara nyingine ilikuwa ishara ya moyoni zaidi. Katika sikukuu muhimu Kanisani Consolata, niliuliza kama angaliweza kupata nafasi kwa ajili ya mama yangu.
"Ndiyo – alijibu – kwa mama yako, naam, hakika!"

Na kwa tabasamu alinipa kadi. Ajabu gani nilipogundua, kesho yake, kumwona mama yangu katika nafasi za heshima, katika mstari wa pili, nyuma ya Wana Mfalme!... ni wema usiosahaulika na ambao mtu wa Mungu tu, mwenye moyo unaoongozwa na upendo wa Bwana Wetu!".

*Ukurasa 126*

**Padre asiye na dosari**

Utume wa Allamano ulikuwa kulipa Kanisa mapadre watakatifu na wamisionari watakatifu. Alifurahia kila Upadirisho, kama ni kufungulia chemchem mpya ya neema kwa Kanisa, Misioni, ulimwengu wote.

Kwa mapadre wote alionyesha heshima wa kina: "*Kwa sababu* – alisema – *asiyeheshimu ustahi wake mwenyewe katika wengine, hawezi kuiheshimu kwake mwenyewe*". Mapadre wahitaji walishika nafasi ya kwanza katika ufadhili wake. Mmoja wa hawa aliyekufa katika hali ya umaskini

wa hiari, na ndugu walipotaka kumpa mazishi ya kimaskini, Allamano mara aliingia kati : "Hata kidogo! Ni padre na anastahili fahari yote ya upadre. Apate mazishi namba wani, nagharamia mimi!".

Shughuli zaidi sana alionyesha kwa wahitaji wa msaada wa kiroho. Katika shukrani ya Misa, kama kawadia alikuwa akisali kwa ajili ya utakatifu wa mapadre, vivyo pia hakuacha kumwomba Mungu kwa mapadre waliopotea. "*Mnajua nawaombea nani zaidi? Kwa waliotengwa na Kanisa* speciali modo" (kwa namna ya peke). Akiwa amejaa roho ya Yesu Mwalimu, alitaka wawatendee kwa huruma na upendo mkuu. Alikuwa akisema: "*Tungeweza kumchubulia fulani*

*Ukurasa 127*

*chapa ya upadre, ingekuwa basi. Lakini kwa sababu haiwezekani, basi, tujitahidi kuwategemeza na kuwasaidia kufufulia* gratiam quam accepertunt per impositione manuum Presbiteri (*neema waliyopokea kwa kuwekewa mikono ya Askofu*). *Tujaribu kuhuisha mwali uliofunikwa na majivu, kuhuisha utambi unaozimika, kabla ya kuzimika kabisa*". Ndivyo alivyofanya, na alifaulu kumrudishia zaidi ya mmoja kwenye kilele na heshima ya wito wake.

Lakini kuliko kwa maneno, alionya na kufundisha kwa mfano wake. Alikuwa padre asiye na dosari. Kutokana na ushuhuda wa waliomfahamu, Allamano alitunza safi kabisa neema ya ubatizo. "Fadhila iliyo bora – wanaandika – ilikuwa inagandamana naye". Na wanamtambulisha: "wa kimalaika". Mwangaza wa roho uliangaza toka kwa nafsi yake, na kuangaza utakatifu wa kiroho wa hali ya juu uliovuta na kuleta mema. Ilitosha kumkaribia, na hivyo kuvutwa kutamani fadhila.

Kuhusu wanawake alikuwa na utaratibu sana; alikuwa akiongea na sauti ndogo, macho chini, na hakutoa mkono wa kubusu; hakuwapokea chumbani, bali sebuleni chini, hata kurudia kutelemka ngazini mara nyingi mfululizo. Wakati wa ugonjwa alitaka daima awemo mmoja wa mapadre wa Kanisani, isipokuwa ugonjwa wa mwisho, ambapo alipaswa kupokea dawa kila muda mfupi, akaruhusu masista wamisionari wawili kumhudumia. Mganga alitumia utaratibu sana kwake, akitumia ya lazima tu

*Ukurasa 127*

kucheki moyo na mapafu, ijapo yeye angalipenda kuacha hata hayo, lakini aliruhusu akiashiriwa na padre aliyemhudumu.

Hufahamika jinsi maonyo yake kuhusu hayo yalivyokuwa ya kufaa sana. Alichota na kutoa toka ya kwake. Fadhila safi, katika mafundisho yake ilikuwa ishara ya kwanza ya wito, na alikuwa mkali kumwondoa katika njia ya upadre walioyumbayumba katika hilo.

"*Tafadhali, naomba, ondoka! Katika hali nyingine huenda utapata wokovu, ambao hakika utapoteza katika hali ya upadre*".

"*Fadhila zote ni za lazima, lakini nawaambia kuwa hiyo ni ya lazima ya pekee".*

*"Usafi pekee unamhalalisha padre na mmisionari kutekeleza huduma yake, na usafi pekee unafanya huduma hiyo kutoa matunda".*

*"Mkiwa safi, daima safi, nina hakika kuwa mtafanikiwa. Bwana wetu anajidhihirisha kwa roho safi*

*na mtatenda maajabu*".

*"Mwe safi! Ndilo onyo linalorudia kila siku Kanisa na Katiba".*

*"Kila siku mnapovaa kanzu, kumbukeni wajibu wa dhati mliojichukulia mbele ya Mungu, na Kanisa na Shirika".*

*"Mkiwa mapadre safi, mtakuwa mapadre watakatifu, kwa sababu ni kweli daima kuwa padre safi kamili ni padre mtakatifu kweli".*

*Ukurasa 129*

Frateri mmoja aliyechora msichana mchungaji katika picha ya shambani, alimwuliza:

"Kwa nini hukuchora mchungaji mvulana?".

Na katika swali hilo nyepesi, sawa na katika mtindo wa sauti na katika macho yake, mafundisho makuu.

Alipomwonya padre kijana kuhusu kuwabembeleza watoto kwa kuwagusa, naye akijitetea kwa kusema kuwa na Bwana Yesu alifanya hivyo:

"Ni kweli – akajibu Allamano – lakini wewe si Bwana wetu".

Jinsi alivyoona wazi alipotoa mashauri, kutokana na usafi wa maisha yake. Kwake ukadhihirishwa usemi: Heri walio na moyo safi, kwa maana watamwona Mungu. Kwa haki, basi, kard. Salotti katika barua ya rambirambi kwa kifo cha Allamano aliweza kuandika juu yake: "Alilinda rohoni usafi wa mtoto, na aliweza kuonja furaha za utotoni safi usiokufa kamwe!".

**Siri kuu**

Ili kulinda usafi uliokuwa kamili vile, na pia fadhila zote za kipadre, Allamano aliweka ibada. Hakukubali njia ya kati: ibada thabiti au uharibifu wa padre, roho ya sala au roho ya ulimwengu. Vipaji vyote vya akili na ya lugha, utendaji wote wa nje alizihesabu si kitu, zisiposhirikiana na maisha ya kina ya ndani:

*Ukurasa 130*

*"Kufanya kazi katika kitubio, kufanya kazi kwa kuhubiri na shuleni, naam, zote sawa, lakini kwanza unatakiwa muda kwa ajili ya roho yake mwenyewe".*

*"Kuna watu ambao kwa kuwashughulikia mno wengine, hawajijali wenyewe; na wamekuwa batili kwao na kwa wengine".*

*"Anayefanya kazi kwa utii au kwa lazima, huyo anasali. Lakini hamaanishi kuwa asipaswe kutekeleza ibada zake, kwa kunyima muda kutoka kwa kazi za huduma".*

*"Angekosa yule anayejitolea mzima kwa kazi za misioni na kuzembea sala, mazoea ya fadhila na kushika nadhiri".*

*“Ijapo Mungu aliahidi kuwa na mitume wake siku zote hata mwisho wa dahari, lakini anajalia msaada wa pekee wale tu wanaoungana naye kwa akili na moyo”.*

“*Yule tu anayeishi, kama Mt. Paulo, katika B. W. Yesu Kristo, ataweza kusema:* omnia possum in eo qui me confortat (naweza yote katika yule anaynipa nguvu)”.

*“Maskini mapadre wale na wamisionari wale ambao wanadhani kutekeleza wadhifa yao kwa wingi wa matembezi, kufanya kelele, wakiacha au kupunguza mazoezi ya ibada! Wanasahau kuwa ni vyombo tu wa neema Mungu, na kuwa hiyo neema kwa kawaida inapatikana kwa sala na mwungano na Mungu”.*

*“Hutendeka zaidi baada ya robo saa ya sala, kuliko saa mbili bila kusali”.*

*Ukurasa 131*

Mara nyingi alishurutishwa kujifunga chumbani asiwapokee watu, na kuepa mialiko kwa kazi njema ili atumie muda katika sala. Haikutokea kamwe aache sala ya kutafakari, kujitafiti mara nne, somo la kiroho. Alikiri kuwa hakuwahi kupata nafasi ya kusoma hadithi za kubuniwa au vitabu vya aina hiyo, na mara nyingine hata kupata nafasi ya kutazama gazeti katoliki. Alifanya bila kukosa mfungo wa mwezi kila Jumapili ya kwanza ya mwezi. Alijiandikia *“Mwongozo wa maisha ya kipadre”*, wenye mazoezi ya ibada ya kila siku, ya mwezi, alioshika hadi kufa. Alipanga, kila siku ya juma, moja ya ibada muhimu ya Mkristo: Utatu Mtakatifu, Roho Mtakatifu, Malaika Mlinzi, Roho za Toharani. Alijiandikisha katika Vyama vingi vya kidini, alivaa skapulari na kusali sala zilizopangwa. “*Lazima kuthamini yote* – alikuwa akisema – *watakatifu hawakudharau kitu. Mt. Alfons alijiandikisha katika Vyama vyote, na kuvaa skapulari zote. Alikuwa Mwali mkuu wa maadili, na wa Theolojia!*”. Alifanya kwa kawaida Saa ya Ulinzi kwa Moyo Mt. wa Yesu, na kuwa na ibada kuu kwake. Katika kusali Rozari alitumia zaidi ya robo saa, kutamka vizuri maneno na kutafakari matendo.

Alikuwa mwangalifu kusikiliza uvuvio, aliishi maisha ya mwungano mkuu na Mungu. Hakuwahi kuonekana katika mambo ya upuzi, mahali popote pale na katika nafasi yo yote;

*Ukurasa 132*

na katika nafasi yo yote; wala hakuzungumza bila kukoleza na maneno ya kiroho; wala hakuwahi kujitolea kabisa kwa mambo ya nje;

“*Mara nyingine kichwa kimevimba hivi... lakini najitahidi kujikusanya. Nashika mkononi msalaba na kusali*”.

Aliweza kutoka kila kitu kuelekea ibada. Alitakasa safari zake, wa kila kijiji alichopitia, alimsalimia Yesu Ekaristi, Malaika na Wasimamizi Watakatifu wa mahali. Na kusali kwa ajili ya roho za marehemu. Wala magonjwa yaliweza kuvunja maelekeo ya roho kwa Mungu. Wakati wa maumivu makali ya kichwa (*migraine*), alitaka kukaa peke yake na kusali zaidi. “*Nina mengi ya kujadili na Bwana, hata wakati unapita haraka zaidi nikiwa peke yangu*”. Usiku, kila alipoamka, alikuwa kufanya Komunyo ya rohoni.

Hapo tunapata maelezo ya kazi nyingi za kan. Yosef Allamano, hapo tunapata siri ya

mafanikio yaliyotokea daima. Ni katika sala kwamba alipatana na Mungu na B. Maria; sala ya daima. Kwake unafaa usemi wa Zaburi: "*Heri mtu ambaye sheria ya Bwana huitafakari mchana na usiku. Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake, wala jani lake halinyauki; na kila alitendalo litafanikiwa*". (Zaburi 1).

*Ukurasa 133*

**"Laus perennis" ya Kanisa**

Umuhimu wa pekee, na kwa haki, Allamano alitilia kusali Sala za Kanisa "Laus perennis (*sifa ya daima*) *ambayo Kanisa la duniani linaunganisha na sifa ya daima ya Kanisa la Mbinguni*". Ikiwa akifurahia kila upadirisho kwa kuweko Misa zaidi duniani, zaidi sana alifurahia kusimikwa Shemasi mdogo, kwa kuweko: "*mmoja zaidi kusali Sala za Kanisa, maana yake kusema kupata neema nyingi zaidi juu ya Kanisa, juu ya Shirika, juu ya Misioni*".

Aliwakemea kwa nguvu wale wanaopuuza wajibu huo muhimu kwa kujitetea kuwa na kazi nyingi: "*Inawezekana mara nyingine kukata sala ya breviari, kwa mfano kwa kwenda kwenye kitubio, lakini baadaye kuendelea mara. Hapo ni kumwacha Mungu kwa ajili ya Mungu na sio Mungu kwa ajili ya kazi*". Safari moja, kwa kusahau tu, aliacha *Kompleto*, na akikumbuka alipoamka baada ya usingizi wa kwanza, mara aliondoka kitandani na kusali aliyosahau. Wakati wa vita kuu ya kwanza, mapadre wengine walifasiri mwongozo wa Kiti Kitakatifu wa kufikiri kusamehewa kusali Breviari kwa sababu waliingia jeshini tu, Allamano alisikitika, na hakuweza kuficha kukataa kwake. Alifurahi sana halafu Roma ilipotoa maelezo kinyume chake. Hivyo pia alifurahi walipohisia

*Ukurasa 134*

wazo la kukusanya sahihi la kuomba Kiti Kitakatifu kupata ruhusa ya kuacha Breviari kwa mapadre wote jeshini, hawa kwa wingi sana walikataa kukubali. "*Hupendeza* – alisema Allamano – *kuonekana kuwa makleri wetu wana roho njema*".

Alikuwa na maoni kuwa wanafunzi wa seminari wanapaswa mapema kujizoeza kusali Sala za Kanisa. Kwa lengo hilo alichukua nafasi ya pekee ili kueleza sehemu mbalimbali ya Breviari, maana yake kiliturjia, miongozo yake, na kufafanua tenzi muhimu, zaburi na sala. Tazama, mashauri yake kadhaa ili kusali vema Sala za Kanisa:

*"Kusali wakati wake. Kwa kusali wakati wake, kadiri ya roho ya Kanisa, si nzito".*

*"Kusali daima na vema yote, bila kuogopa kuiba muda kwa masomo au shughuli nyingine",*

*"Kabla ya kuanza, licha ya kujiwekea mbele ya Mungu kwa kusali kwa ibada sala ya mwanzo, kufanya Komunyo ya rohoni, ili kuunganika mwili, akili na moyo na Yesu".*

*"Katika kusali Zaburi kujitahidi kuingilia hisia ya Nabii, kama ni yetu".*

Alitaka kuupa Sala ya Kanisa wakati ulio bora ya siku, na kusisitiza sana kusali kanisani, iliyo Nyumba ya sala, hali kuna fursa ya kumwamkia zaidi Yesu katika Sakramenti,

*Ukurasa 135*

na kuwapa waumini mfano mwema. Kila mwaka alisambaza sanamu iliyojulikana sana – walivyoiita – ya shetani anayekusanya silabi zinazoanguka kutoka kwa mapadre wanaosali breviari, na anatembea akilemewa na mzigo wa kikapo kilichojaa hata kumwagika.

"*Eh* – alisema kwa kucheka - *inaonekana imezidiwa, lakini kwa kweli ndivyo ilivyo. Itawasaidia kuwa waangalifu katika kutamka vema maneno*". Siku moja, katika Kanisa kuu, aliwapa hata Wakanoni, baadhi yao walimshukuru kwa "onyo!".

Aliangalisha kuhusu mahangaiko, na wenye kuhangaika aliwapa kanuni hizo:
*"Usihangaike hasa kuhusu nia. Kwa sababu ya nini umeshika Breviari mkononi, usipokuwa kwa ajili ya kusali. Basi, nia iko na inatosha hivyo".*

*"Si lazima kukamilisha maneno. Kusema kwa utulivu, kama tunaposali sala huru".*

*"Hasa usirudie kitu. Acha shetani aseme, wewe endelea tulivu. Lazima baada ya miaka kumi, ishirini ya padre, uweze kusema: Sikurudia kitu!".*

*"Hata ikiwa umekosa Breviari yote, usirudie. Hivyo, kama kwa bahati mbaya umesali Zaburi fupi zaidi, hakuna shida ya kulipia. Inatosha hivi, endelea tu!".*

*"Unapokata zaburi katikati, weka alama, halafu endelea toka pale ulipoacha.*

*Ukurasa 136*

*Ole wako ukianza kurudia kitu!. Tena tunaweza kusema kuwa zaburi zote zimevunjika na kila mstari umekamilika wenyewe. Halafu Bwana hana shida kwamba wewe urudie tena zaburi kwa sababu umeikata. Yeye anajua vema tulipofika".*

*"Usihangaike kwa ajili ya mawazo yanayokuja, bora usiyatake".*

*"Hata ingetokea kwamba mwisho wa zaburi una shaka ya kama ulisali vema kwa sababu ya mawazo, kama hatuna hakika kabisa kwamba tumeiacha, kaa tulivu, kuwa umeisali".*

Alimaliza fundisho kwa kusema maneno ya Mt. Yosef wa Kupertino kwa askofu fulani: "Jitahidi kuwa mapadre wako wasali vema Misa na kusali kwa ibada Breviari, na utakuwa na mapadre watakatifu".

**Mwana wa Kanisa**

Akiwa na ujuzi kabisa wa Masomo Matakatifu, kiasi kwamba maneno yake yaliweza kufuatwa na hakika, kan. Allamano lakini alikuwa mtu mwenye imani rahisi: anayekataa mkwaruzo wa kubishi yote, kudadisi yote, kupinga yote; - na mwenye imani nyenyekevu: asiyetaka kujua zaidi ya lazima, kuliko wengine na hasa zaidi ya Kanisa.
Alikuwa na maneno makali kwa wale, hasa mapadre, ambao kila mara wanamsemea Baba Mtakatifu au Kanisa: "

*Ukurasa 137*

Picha

*Ukurasa 138*

alikuwa akisema kwa nguvu – " *Mnawatambua mara; ni watupu wa ibada na wamejaa ya 'ajuaje!*'". Akiongea kuhusu modernismi, alichukua sura ya masikitiko ya kushtusha::

"*Siku hizi zetu kimeinuka na kuenea kikundi kilicho kibaya kushinda ujansenio, uzushi kweli na uasi wa imani. Wengine, kwa ajili ya mambo mapya, wakisukumwa na kiburi, wanajidai kuwa na haki ya kuhukumu yote katika Kanisa: kuanzia Baba Mtakatifu, hadi kweli za dini na maadili*".

"*Sisi tunakiri kuwa pamoja na Baba Mtakatifu. Ikiwa kitabu kinafikia mikononi mwenu, au padre fulani awakaribie ameambukizwa na moderns imi, mwambieni: Vade retro satana!* (Shetani, nena nyuma)".

"*Tusali ili Bwana alinde imani yetu nyenyekevu na nyepesi, akifukuza mbali nasi tabia mbaya ya kuchunguza na kutilia mashaka juu ya yote*".

"*Naomba kwa dhati Bwana shirika letu lisihusike, afadhali aliteketeze!*"

Alisikitika sana kwa ajili ya matangazo ya Waprotestanti katika Italia. "*Sisi tumelala* – alionya – *bali mbwa mwitu wanaua. Eh, hutakiwa ari zaidi, ari zaidi, ari zaidi!* Omnia facio propter evangelium (nafanya yote kwa ajili ya Injili). *Yote tuwezayo: kusali, kufanya kazi, kutolea sadaka chochote na kujitolea*". Kijana aliyetoka gerezani karibuni, alikuja kumwambia kwamba Wavaldo waliahidi kumpa mamia ya Lira, akikubali kujiunga nao. Allamano alitaka kadi ya mlungula, akaipasua, halafu mara akashughulikia kumtafutia kazi. "*Kweli,* akaongeza – *huyu amekuja mara nyingine kunidanganya...*

*Ukurasa 139*

*Lakini nifanyeje? Afadhali kutapeliwa kuliko kuacha kupotea imani ya roho moja*".

Alifundisha kuwa tunapaswa kumtii Baba Mtakatifu, sio katika mambo ya imani tu, bali hata matakwa yake.

"*Sisi tunaona mambo toka chini, Baba Mt. anaona toka juu. Sisi tunaona mambo kama viumbe vinavyokufa, bali yeye anayaona kama Wakili wa B. W. Yesu Kristo*". Kwa sikukuu ya Baba Mt. alitaka tuadhimishe kwa shangwe kuu, na kumwombea sana Baba Mt.: "*Msali ili Baba Mt. aweze kutenda mema yote anayotaka. Tuahidi kwake, kama Wakili wa B. W. Yesu Kristo, utii wa akili na wa moyo, na tumfariji kwa kuongeza idadi ya Wakristo, kwa kulipiza kwa Wakatoliki wengi ambao uzushi na maadili maovu huwapokonya katika Kanisa*".

Katika Katiba ya Shirika aliingiza kiri hilo la imani: "*Wamisionari wako chini, kama kwa*

*Mkubwa wao, ya Baba Mtakatifu wa Roma, na wanapaswa kumtii hata kwa amri ya utii mtakatifu; wanakiri utiifu kamili kwa Idara takatifu ya Propaganda Fide; kwa hiyo itakuwa daima wajibu wao kwa dhati, licha ya kufuata miongozo, pia kulingana katika yote kwa roho na maelekeo yaliyoidhihirishwa kwa namna yo yote ile*". Na alikuwa akieleza: "*Haikuwezekana kusema zaidi ili kuonyesha insi Shirika na kila mwanaushirika anavyopaswa kuambatana na Kanisa na Baba Mtakatifu*".

Kila safari yake Roma ilichukua tabia ya hija. Maamkio ya kwanza yalikuwa Kanisa la Mt. Petro

*Ukurasa 140*

Mara alipoona Kanisa aliondoa kofia, na kusali Kanuni ya Imani, halafu sala nyingine kwa ajili aya Marehemu Mababa Watakatifu na wafadhili wa Kanisa.

Kisha kuingia, baada ya kuabudu Ekaristi, aliendea kaburi la Mkuu wa Mitume, haafu aliendea sanamu ya shaba, na hapo aliweka kuchwa chake chini ya mguu uliotoka nje wa sanamu, alishika kwa muda kana kwamba anataka kudhihirisha kwa tendo lile la nje, matoleo kamilifu yake na ya Shirika kwa ajili ya Kanisa.

**Katika nyayo za Mjomba**

Kutoka kwa imani hiyo hai ya Allamano ilitokea imani thabiti kwa Mwongozo wa Mungu. Ndio uliomhamasisha kukabidhi gharama kubwa sana kwa ajili ya Kanisa la Consolata na Misioni. Kweli, aliwahi kupita vipindi vigumu, hasa mwanzoni, lakini matumaini yake yalikuwa makubwa kiasi kwamba hakuonekana kuhangaika, na hakuwahi kuhitaji mikopo. Mwongozo wa Mungu ulionekana wazi kwa macho, na msaada ulikuwa ukifika wakati wake na kiwango alichohitaji, hata "kusadiki" kulikuwa shida, hasa kwa sababu aliugusa kwa mkono katika miujiza yake mingi. Mara ngapi msaada – na kilikuwa kiasi kikubwa cha fedha - ulifika wakati wa kufaa na kiwango alichoomba cha mahitaji.

*Ukurasa 141*

Kwetu alituambia:

*"Shida yangu, si kuhusu kuingia fedha, bali kwamba mstahili maingilio yake".*

*"Nafurahia idadi wala siogopi gharama".*

*"Mhasibu ananionyesha tarakimu za ajabu, lakini sitishwi. Shirika limeanzwa kwa mapenzi ya Mungu, naye anajua".*

*"Tukiitikia, Bwana atatokeza na kuingiza, la sivyo, kutoka tu".*

*"Bora mshike roho njema, na hamtakosa kitu".*

*"Ikiwa siku moja tutakosa mahitaji ya lazima, itakuwa kwa sababu kati yetu kuna Mwamaleki; na basi, nitakuja na kumfukuza".*

Kwa upande mwingine alituonya tusikae bila kushughulikia, tukingoja miujiza tu.

"*Tegemeo la Mwongozo wa Mungu haikatalii kufikiria na kushughulikia ya baadaye. Yesu anakatalia kuhangaika mno kunakotokana na kukosa imani kwa Mungu na kutamani mno mambo ya dunia. Katika jumuia nadhani kuwa, kwa kumla, tunaelekea kwenye kasoro kinyume chake. Tukiona kuwa mezani hatukosi kitu, na kutayarishwa na gharama kubwa za Wakubwa, karibu hatufikirii Mwongozo wa Mungu na kuushukuru, lakini tunadhani kuwa kimedaiwa! Katika ulimwengu si hivyo! Bali kila mmoja anajitahidi kusogeza mbele. Basi iwe jitihada ya kila mmoja kushiriki kwa mema ya jumuia*".

*Ukurasa 142*

Ikiwa imani ya Allamano kwa mambo ya dunia ilikuwa kubwa hivyo, ni rahisi kufikiri jinsi ilivyokuwa kubwa zaidi sana matumaini yake kwa kudaka Mema Makuu: Mungu. Naam alilalamikia kuwa fadhila hiyo isithaminiwe ya kutosha: "*Tunatambua sharti la kusadiki na kupenda, na tusingekubali mawazo kinyume chake, bali sio watu wa ulimwengu tu, bali hata watu wenye utauwa, na zaidi hawa kuliko wale, hawajali kupokea dhana za kukata tamaa dhidi ya matumaini ya Kikristo, kwa singizio la mema, yaani uchaji wa Mungu*".

Usemi: "*Sijui kama nitaokoka?*" hakutaka kuusikia: "*Ya nini hiyo 'sijui'? lazima kwenda mbele na hakika kuwa Bwana anatujia katika umaskini wetu, bora tutekeleze ulio upande wetu, kiasi cha nia njema*". Alikuwa akisema tena: "*Fadhila ya pekee ya Mt. Cafasso ilikuwa matumaini. Nilishuhudia katika Mchakato wa kutangazwa Mwenye Heri. Hususan fadhila hiyo alikuwa anayo kwa ajili yake mwenyewe, na kwa ajili ya wengine, hata kuwatilia waliokata tamaa na kuwapeleka wima mbinguni. Dhambi kinyume ya matumaini aliita dhambi ya wapumbavu, na ndivyo ilivyo kweli*".

Naye pia Allamano alikuwa anayo fadhila hiyo kiasi kwamba aliweza kuwashirikisha wengine kwa kufanikiwa kabisa, wanavyoshuhudia kwa umoja walioungama kwake. Hakutaka hata mtu mmoja kukata tamaa: "*Bwana, katika dakika za mwisho anaangazia roho na kanuni za Kikristo, na malezi bora waliopokea, na kwa neema yake anasaidia kuweka matendo ya majuto na upendo. Haifai kabisa kuwa na mashaka kwa mtu yeyote,*

*Ukurasa 143*

*kwa sababu huruma ya Mungu haina mipaka, na kupita kazi nyingine zake zote".* Basi, alikuwa na dhana kuwa: *"haiwezekani kuzidiwa upande wa kumwamini Mungu".*

**Miali ya upendo wa Mungu**

Miali hii katika moyo wake ilikuwa inawaka. Kwa kuweza kutambua, ilitosha kumsikiliza kuongea juu ya Mungu, kueleza kunadai nini kumpenda Mungu kwa moyo wote, kwa akili yote, kwa roho yote, kwa nguvu zote. Kila neno limebeba kama chapa ya moto, moto wa upendo wa Mungu.

Mtu mmoja aliyemfunulia kuwa alikuwa na ugonjwa wa moyo na alikuwa akishtuka,

Allamano alimjibu:

“Fikiri kuwa sote tunapaswa kufa kwa ugonjwa wa moyo, sisi tunaompenda Mungu! Tunapaswa kutaka kuwa moyo wetu uchakae na upendo”.

Sista mmisionari ambaye kwa sababu ya kazi yake, alipaswa kumkaribia kila siku Rekta pale Consolata, anaporudi shirikani, alikuwa akiulizwa na masista wenzake awaambie maneno ya Baba. Siku moja alimwambia jambo, akamwuliza alipaswa kwajibia nini.

“Uwaambie kuwa nataka wote wawe wenda wazimu wa upendo wa Mungu!”.

Mara nyingine alipokuja kuongea juu ya upendo wa Mungu, aliwaka kiasi kwamba hata uso uliwaka, na walipaswa kubadili hoja, kwa kuogopa kuwa itamdhuru afya.

Mwanzoni mwa kila mwaka aliweka nia:

*Ukurasa 144*

kuwa hatua zote na kila pigo la pumzi ziwe zote vitendo vya upendo wa Mungu. Alitaka tujizoeze kwa vitendo hivyo, ili viwe rahisi saa ya kufa. Na alipinga kabisa wanaofundisha: kuwa ni vigumu kufanya tendo la upendo kamili wa Mungu: “*Sivyo*, - alisema – *la, sivyo. Maneno ya Baba yetu, hasa sehemu ya kwanza, yote ni vitendo vya upendo wa Mungu.; na vikitoka moyoni, ni upendo kamili*”.

Ulikuwa upendo wa Mungu kumsukuma kwenye kazi nyingi na muhimu za ari. Jinsi ulivyo upendo huo huo uliomfanya kuhisi kwa undani matusi kwa Mungu, na kwa hiyo, kuona wajibu wa kuyazuia au kulipiza. Akipita mjini na kujikuta katika mazingira ya kutarajia kutokwa kukufuru jina la Mungu, alijitahidi kutanguliza maovu na matendo ya malipizi. “*Ikiwa siwezi kuzuilia –* alitufunulia - *walau nataka Bwana apate sifa kabla ya kufuru*”. Kwa sababu hiyo hiyo hakuruhusu kwetu kusema kuhusu ‘karnival’ (sherehe ovyo kabla ya Kwaresima), ila kwa ajili ya kufanya malipizi mbele ya Yesu Ekaristi. “*Nawaambia na nitawaachia kimaandiko: katika Shirika, hakuna karnival. Karnival yetu itakuwa siku ya Pasaka pamoja na Yesu Mshindi*”. Walipomwambia kuwaachia walau wadogo kufanya burudani kidogo, alijibu: “*Hata, nao pia hakuna. Nawaheshimu mno kwa fadhila ya na busara yao*”.

*Ukurasa 145*

Alikuwa na shukrani mno kwa Mungu kwa ajili ya fadhili zote alizopewa. Alihimiza daima fadhila hiyo kwa roho. Ibada ya kufunga mwaka katika Kanisa la Consolata ilifikia, wakati wa Allamano kuwa Rekta, kilele cha utukufu na sherehe. Kwa kila tukio muhimu au fadhili toka kwa Mungu, aliamuru sala za shukrani. Alishauri kutumia neno *Deo gratias* na kumwelekea mara Mungu kwa mema tuliyofanya au kutendewa. Si mara chache, kwa maskini waliojibu “ahsante!” sadaka yake, alifundisha kusema: *Deo gratias!* Alitumia na kuhimiza, adhimisho ya kumbukumbu za matukio muhimu ya maisha, kama ubatizo, komunyo ya kwanza, nadhiri za kitawa, Madaraja matakatifu, n.k.; alieleza: “*Ili kuhuisha ndani yetu hisia ya roho na fadhila za neema tuliyopewa*”. Alipoweza, alipita siku katika mfungo. Kwa ukumbusho wa ubatizo, alisoma sala za ibada ya ubatizo na kurudia kuweka ahadi za Ubatizo.

Kwa namna ya pekee, upendo wa Mungu alioonyesha na kutekeleza kwa kulinganika kikamilifu na Mapenzi ya Mungu. Ni hapo kiini cha utakatifu, na imekuwa taa ya maisha yake. Kila hatua ilipigwa katika mwanga huo, kila tendo limeangazwa nao. Siku moja, akijibu heri zetu za kumbukumbu ya kuzaliwa, alituambia: "*Jambo moja linanifariji, ninapokumbuka kwamba niliitikia kidogo neema nyingi: kwamba nilifuata daima njia aliyonipangia Mungu toka umilele...*

*Ukurasa 146*

*mamlaka ngapi nilibeba! Lakini ndivyo Mungu alivyotaka, na neema yake ilikuwa pamoja nami. Ikiwa Bwana alibariki kazi nyingi nilizoanzisha, hata kushtusha watu mara nyingine, siri yangu ni kwamba nilijitahidi kufanya Mapenzi ya Mungu kabisa. Hiyo ndiyo faraja yangu na itakuwa amani yangu mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu*".

**Tamaa ya kimungu ya Ekaristi**

Juu ya ibada ya kipadre, kan. Allamano aliweka ibada kwa Yesu Ekaristi. Ulikuwa upendo wake mkuu. Tungetaka kusema, mintarafu mstari wa kiroho, tamaa yake tawala. Tamaa ambayo alijitahidi kwa kila njia na kwa uwezo wote kupitisha kwa mapadre vijana, na sisi: "*Ningetaka macho yenu yakazane, hadi kupenya, na kumwona daima Yesu katika sakramenti*".

*"Nataka wote mwe wenye ibada kabisa kwa Sakramenti Takatifu. Nataka iwe ibada yetu kuu. Lazima iwe ya wote, lakini hasa yetu kwa namna ya pekee".*

*"Nawataka wote kuwa Sakramentino, Wamisionari na Masista, hapa na Afrika".*

Furaha yake kuu ya moyo wake wa kipadre ilikuwa kuona zimeongezeka, kwa kuanzisha Shirika, idadi ya Tabernakulo Italia na Misionini. Alikuwa anasisitiza daima kuwa

*Ukurasa 147*

tuweze kuthamini neema ya kuwa na Yesu daima pamoja nasi; Tabernakulo iwe kiini cha kila nyumba, na tena cha kila moyo, ambamo yote humzunguka: "*Akili yetu na moyo wetu zingepaswa daima kuelekea Sakramenti Takatifu. Ni uzushi wa modernisti kusema kuwa siku zetu hizi zinadai kazi za nje, na sio sala nyingi, maisha ya amali, sio ya taamuli*".

Akisema juu ya Misa, roho yake ilishangilia: "*Eh, Misa ni jambo kubwa sana!... Ni ibada kuu kabisa ya ibada zote!... Hata tungepaswa kujitayarisha miaka kumi na tano au ishirini kwa kuadhimisha Misa moja tu, tuzo gani! Na kuzisali nyingi? Ah, heri ya padre!*". Katika miaka yake hamsini na mbili ya upadre hakuacha kamwe kuadhimisha Misa, isipokuwa kwa ugonjwa. Hata katika safari hakuacha kusali Misa, ijapo amechoka au saa imekwenda. Mara nyingine alifika Torino toka Roma karibu saa sita mchana, amechoka hata kumwonea huruma, lakini kila mara alisali Misa.

Siku yake ilikuwa ya ekaristi hasa, amegawa kati ya matayarisho na shukrani ya Misa. Jioni, katika maamkio ya Ekaristi, alianza kujitayarisha kwa mbali. Tena aligawa siku katika vipindi vingi

vya saa mbili mbili, na kurudia sala za kuabudu, shukrani, toleo, ombi na kumfariji Yesu. Lakini hata matayarisho na shukrani za karibu hakuziacha kamwe. Kabla ya Misa alijitahidi kulinda ukimya kuu. Alipomaliza sadaka takatifu,

*Ukurasa 148*

na hata baada ya shukrani, aliendelea kujikusanya, akiwashangaza wote.

Wote waliomwona altareni, kwa pamoja wanadokeza heshima yake, ibada na ari. Wanashuhudia: "hisia kali waliyopata"; wanasema: "kulelewa katika uroho wa kipadre hata kwa kutazama tu kuadhimisha Misa": "aliniongezea sifa niliposhiriki mara ya kwanza Misa yake".

Kwa kawaida alitumia dakika ishirini na tano hadi ishirini na nane, miaka ya mwisho alifikia nusu saa. Alikuwa na maneno ya kukemea wale, ambao, kisha kurudi toka altareni, walitazama zaa, wakijivunia kuharakisha: "*Aibu!... Aibu!.. Kupima muda kwa Bwana!... afadhali kutazama kama tumepuuza madhehebu, kuacha kitu, kwa sababu Bwana hawezi kuvumilia makasoro mengi katika kuadhimisha ya Sadaka Takatifu, na kurudi toka altareni tumebeba makosa kuliko mastahili*".

Toka kitabu cha Mt. Alfons "*La Messa strapazzata*" (Misa iliyochakazwa) alichukua sehemu kadhaa ambazo alizitengeneza kama taamuli fupi thelathini. Kila asubuhi alikuwa akiisoma moja, na alikiri kuwa alipata faida kubwa. Basi, imekuwa kwamba kwa nafasi ya Jubile yake ya kipadre, alipojibu heri zetu, aliweza kutamka maneno hayo kamili: "*Baada ya miaka hamsini ya Misa, sina majuto yo yote. Sisemi kwa kujivunia, ijapo imgekuwa kiburi takatifu.*

*Ukurasa 149*

*Nina makosa mengi, lakini Misa, nimejitahidi kuisali vema, nalo linanifariji sana kuliko yote*".

Mara ngapi tulimsikia kudhihirisha hamu yake ya kuweza kupokea sio siku zote tu, lakini hata zaidi ya mara moja kwa siku, ikiwezekana! Matokeo ya Komunyo aliyafupisha katika usemi mmoja wa pekee zake: "Kutoka kwa Komunyo tuliyopokea vema tunasimama tunamwaga neema, roho na mwili. Neema na yote neema". Alitaka pia ostia kuwa mpya na zima: "*Nataka Bwana Wetu aheshimiwe pia katika hayo*". Ni bure kuongeza kuwa kuhusu kupokea aliwaacha wanafunzi uhuru kamili; tena aliamuru kuwa kwa kwenda kupokea wasifuate orodha yo yote wala ya uzee au mbao au mengine yoyote. "*Napenda utaratibu, lakini kuhusu kupokea, na kwa ajili ya kupokea tu, ninaruhusu fujo*".

Akituelezea namba ya Katiba kuhusu Maamkio ya Ekaristi Takatifu alikuwa akisema: "*Sio kwamba bila kufikiri tuliweka Maamkio mara mbili kila siku, wala kwa nia ya kuziba wakati. Ni kwamba nataka mjifungie na Ekaristi takatifu kiasi cha kutoweza kuishi bila yeye. Afrika, hasa, nataka Yesu Ekaristi awe Mshauri wenu, Mwongozi wenu, wote kwenu*". Kwa waliosafiri aliwashauri wasikose Maamkio kwa Yesu Ekaristi melini, wakielekea nchi kavu walipodhani kuwemo kanisa. Onyo jingine:

*Ukurasa 150*

kwamba katika Maamkio kwa Yesu Ekaristi tuongee hasa moyo kwa moyo na Bwana: "*Huenda tukiongea na mtu tunamsomea tunachotaka kumwambia? Vitabu lazima viwe msaada tu. Kuchota wazo moja, halafu kuligeuza kuwa letu sisi, kulitafakari, kulionja na kumsifu nalo Bwana*".

Akidokeza jinsi alivyopanga dawati ofisini mwake, alisema: "*Kwenu naweza kuwafunulia sababu gani nilipenda mpango huo; ni kwa sababu nikiwa mezani, naelekea kikanisa cha Chuo, na altare ya Kanisa la Consolata. Natupia macho kwa pamoja Chuoni na kumwamkia Yesu, halafu ya pili na pale namsalimia Ekaristi*". Alikuwa akishika karibu naye orodha ya Vituo vya Misioni, na kufanya ziara kiroho, kila kimoja kwa zamu na kumwamkia Yesu Ekaristi.

Ekaristi Takatifu ilikuwa kweli uhai wa maisha yake ya kiroho. Kwa mgonjwa ambaye alisikitika kuwa, baada ya kufa, asingeweza kumbembeleza Yesu Ekaristi, alijibu: "*Nawe omba akujalie kupita muda wa mbinguni kandokando ya Tabernakulo, pamoja na Malaika wanaoabudu*". Basi, tunapenda kufikiri kuwa roho kuu ya Baba yetu apitie siku yake ya milele kati yetu, karibu na Tabernakulo aliyowekea kama kati na kama uhai wa shirika!

*Ukurasa 151*

**Mwelekeo wake hoihoi**

"*Nakiri mwelekeo wangu hoihoi, ijapo najivunia nao: ni upendeleo wa (madoido) madhehebu matakatifu ya ibada, na umuhimu wake nilikamatwa tangu seminarini*". Naam, upendo wa madhehebu matakatifu ulikuwa sifa yake moja muhimu ya roho ya kan. Allamano.

Aliuonyesha hasa kwa kuyatimiza kikamilifu, bila kutofautisha kati ya madhehebu na madhehebu, ya maana zaidi au pungufu; alikuwa akisema: "*Hakuna kitu kidogo katika utumishi wa Bwana, na kila madhehebu ina maana kubwa machoni pa Mungu*". Alitaka kufanya vizuri kuinama, akihakikisha kuwa kwa kila mwinamo barabara, huambatana baraka ya pekee ya Bwana. Hivyo kwa ishara ya msalaba, alisema: "*Jinsi inavyosikitisha kuona ishara za msalaba fulani!... Afadhali wasiifanye*". Ikiwa frateri au Padre hakuifanya itakavyo, alimwonya. "*Wengine watasema: kichwa maji!.. Ah, si kichwa maji Bikira Maria, aliyemfundisha Bernadeta kufanya ishara ya msalaba, na sidhani mimi nami kuwa vile alivyofanya Yeye. Jambo linaloheshimiwa sana mbinguni*".
Kupiga goti vibaya alisema kuwa "*kupiga goti kwa shetani*". Na kuongeza:

*Ukurasa 152*

“*Madhehebu nilijitahidi daima kufanya vizuri, nikikosa, mara natambua. Ijapo mzee, najitahidi ninapopiga goti kufika mpaka chini. Nahangaika mara ya kwanza, lakini baadaye ni rahisi zaidi*”.

Hayo yalijulikana sana, hata siku moja masista wamisionari walipotembelea Superga, walisikia kusema Rekta wa Kanisa: “Kweli ninyi mnaonekana kuwa mabinti wa kan. Allamano!” “Sababu gani?”.

“Kutokana na jinsi mnavyopiga goti na kufanya ishara ya msalaba”.

Ishara nyingine ya upendo wake wa madhehebu matakatifu: ari ya kuyafundisha. Akiwa Kiongozi wa roho seminarini, alipoanza darasa hilo, na pia mara nyingi katika mwaka, aliwapa mafrateri maonyo ya kuhamasisha. Alisema kati ya mengine: “*Natishwa na wazo la madaraka ambayo wadhifa hiyo inanilemea: madaraka nyeti sana, jinsi ilivyo umuhimu wa madhehebu matakatifu, hapo mnaweza kuelewa mradi wangu utakuwaje: nadai kufuata orodha ya wakati kuhusu muda na namna, na ibada ya nje na ya ndani*”. Haishangazi, basi, ikiwa wanafunzi wake wa zamani walikuwa umoja kuthibitisha jambo hilo, kwa kukiri kuwa: alithamini sana madhehebu matakatifu”; - kuwa “alidai ukamilifu kipeo”.

*Ukurasa 153*

*Picha*

*Ukurasa 154*

Tena kwa kiwango kikubwa zaidi alipenyeza ari hiyo kwa wanafunzi wa Shirika la Misioni. Haukupita mwaka asitumie mazungumzo ya pekee kuhusu umuhimu wa madhehebu matakatifu, kuhusu wajibu wa kutelekeza barabara. Kuhusu nia yake ya kufanya somo la dhati na la kudumu. “*Mhakikishe, wapenzi wangu, kuwa si wa kupoteza muda, tunaotumia kujifunza madhehebu matakatifu. Bwana atawapa neema ya kuweza kujifunza kwa jitihada zaidi na kuelewa kwa urahisi masomo mengine ya shuleni*”.

Alitaka kutuachia kwa maandishi maneno yafuatayo, yaliyo na umuhimu na utukufu wa wasia wa kibaba: “*Shirika letu leo linashika upendo kwa madhehebu matakatifu upendo waliokuwa nao Mashirika yote wa ari ya mwanzoni. Litadumisha upendo huo? Na tena Misionini, ambamo unapata vizuio vingi kwa kukosa makanisa ya fahari na mavazi ya thamani?... Ah, laiti maneno hayo yangechapwa kabisa akilini mwenu na moyoni mwenu! Laiti ningeweza daima kuona ndani yenu jitihada hiyo, hapa katika nyumba asili na Misionini! Laiti baadaye toka mbinguni ningeweza daima kuwatambua kama wana wangu wapenzi!... je, niwaambie?. Mimi, kwa ajili ya kujifunza na jitihada ya kufundisha madhehebu matakatifu, natarajia huruma katika hukumu ya Mungu, na mahali ambapo Bwana alipawekea kwa ajili ya wale wanaoshughulikia heshima ya B. W. Yesu Kristo*”.

*Ukurasa 155*

**Ustahi wa Makanisa**

Nalo limekuwa mwelekeo hoihoi wake mwingine wa Allamano, mtakatifu sawa na ule uliotangulia. *(Allamano anataja kama "mwelekeo hoihoi" mweleleko kwa mambo ya Liturjia, akitumia 'lugha ya kinyume')* Alikuwa na maoni ya kupaswa kuhifadhi katika makanisa utukufu wa hali ya juu, na aliwaambia wale waliodhania utajiri wa kupoteza ovyo wingi wa mali katika makanisa: "*Hawana roho ya Bwana wetu, bali ile ya Yuda*".

Alipoanza kurembesha Kanisa la Consolata, wengine walibishi:

"Upotevu gani! Kweli kuna lazima ya kutumia marimari, hali imetosha marimari bandia?"

Naye:

"Kwa ajili ya Bwana wetu na kwa ajili ya B. Maria haizidii mno, hakuna upotevu".

Wengine tena walimwambia:

"Ya nini kubadili sakafu na kuweka na pale marimari ya hali bora kabisa? Haikutosha ya jiwe?"

"Jiwe – alikuwa akijibu – linafaa nje mlangoni, lakini halifai ndani ya Kanisa; na mara itakapowezekana, tutaliondoa hata pale nje".

Alisisitiza hasa kuhusu usafi wa makanisa.

*"Usafi unawezekana popote, hauna gharama"*

*"Ukitaka kufahamu roho njema ya padre fulani, inatosha kutupia macho kanisani, jinsi linavyotunzwa".*

*Usafi na utaratibu kanisani si kazi ya mtumishi wa kanisa tu, bali hata ya padre; na lazima*

*Ukurasa 156*

*kuhesabu utukufu kufagia kanisani, hata kwa padre, paroko".*

*"Mambo makuu yanaoneka mara, na wote wanayaona: bali jitihada ndogo ya kila siku ya daima, hiyo inaonyesha utaratibu na upendo wa altare. Na ukutufu wa hekalu".*

*"Ningependa wengi wenu washike kazi ya sakristia, ili wote wapate roho hiyo".*

*"Seminarini niliwahi kuwa sakristiani kwa muda wa miaka mitatu, na najivunia kuliko mambo mengine yote".*

*"Misionini mtafanya kadiri mnavyoweza, Yesu alijifanya maskini kwa hiari, anaridhika na usafi na utaratibu. Lakini mlicho nacho kwa ajili ya vikanisa, mkitoe kwa ukarimu*".

Kila alasiri alikuwa akishuka kanisani na kupitia altare zote, akiwaambia wanaohusika maonyo yake. Safari moja alipoona vumbi kidogo katika altare moja, alianza kupangusa yeye mwenyewe. Bibi mmoja alipomwona, akamwambia:
"Lakini, Bwana Rekta, wewe unafanya hayo?"

"Ya nini? Naona fahari!".

Mara nyingine wakati wa usafi wa Kanisa zima, fulani akamwambia:

“Kwa nini unajali kiasi hicho? Unapoishi wewe Kanisa litakuwa zuri; atakayekuja baadaye, ataona”.

Naye Allamano akajibu:

*Ukurasa 157*

“Mimi nafanya kazi kwa ajili ya umilele”.

Alituhimiza kulipiza kwa njia ya ibada kubwa zaidi ya ndani na nje, kosa la uangalifu la makanisa mengi. Akidokeza tendo la Pius X kwamba alikuwa na taa nne katika kikanisa chake binafsi na kuwasha mwenyewe na kuzisafisha kwa mikono yake, alisema kwa mshangao:

“Hawa ni watakatifu!”.

Lakini, akisali Zaburi: “*Domine, dilexi decorem domus tuae et locun habitationis gloriae tuae*” kan. Allamano aliona kuwa wajibu wake kujitafiti kifupi dhamira, ili kuhakikisha kuwa yamekuwa ukweli. Na hali kandokando yake iling’aa marimari, na kuangaza dhahabu alizotumia kuangazisha Kanisa!

**Mwenye ibada kwa Bikiwa Maria**

Tumekwisha ona hatua muhimu zaidi za maisha yake ya kipadre ya Allamano, jinsi zote zina alama na jina la B. Maria. Katika sikukuu ya B. Maria, Mzazi wa Mungu Mtakatifu, alivaa sare ya frateri; - katika sikukuu ya B. Maria, B. Maria wa Karmeli, aliweka nadhiri ya usafi wa moyo; - katika sikukuu ya B. Maria, Kupaswa habari na Malaika, amejiweka wakfu kwake; - katika sikukuu ya B. Maria, Aliyepalizwa mbinguni, alihubiri mara ya kwanza akiwa Shemasi; - katika sikukuu ya B. Maria, wa Mateso, aliadhimisha Misa ya kwanza. Katika “Sheria ya maisha ya kipadre” aliahidi: kila siku, katika mwezi Mei,

*Ukurasa 158*

kutafakari fadhila za B. Maria; - kujitayarisha kwa njia ya novendi kwa sikukuu yake; - kusali kila siku, licha ya Rozari takatifu, sala nyingine za ibada; - kushika kiaminifu masharti ya vyama nilivyojiandikisha kwa heshima ya B. Maria.

Wakati alipokuwa na madaraka ya Kiongozi wa roho seminarini, upendo wake wa B. Maria uliweza kuenea na kushirikishwa. Mada inayopatikana mara nyingi zaidi katika mafundisho yake mafupi kwa mafrateri, kwa kweli ilikuwa ibada ya B. Maria. Na daima maneno yanabubujika ya kupendeza, ya kuvutia. Katika kukosa ibada hiyo au hata kwamba frateri, zinapokaribia sikukuu za B. Maria, haoni ari kabisa, anaona ishara ya kukosa wito au kutoitikia wito. Bali anataka, na anajitahidi kuwa kila frateri *“awe amejaza moyo na Maria!”*.

Basi, tunawezaje kushangaa, ikiwa, alipoteuliwa kuwa Rekta wa Kanisa la Consolata, Allamano aliweza kuwashia watu ari kuu ya ibada, na ya upendo wa B. Maria? Na, akiwa Rekta wa Chuo ya mapadre, aliweza kulea kizazi kizima cha mapadre katika fadhila zifaazo hali yao, chini ya

ulinzi wa Maria? Na, ikiwa kwa jina la Maria aliweza kuanzisha na kudumisha kazi nyingi na muhimu za kitume? Alikuwa wote wa Maria, na B. Maria alimtumia yeye kwa ajili ya mipango yake ya huruma.

Na upendo huu ulipoenea kupita mipaka ya Italia hadi kuwafikia watu wapagani,

*Ukurasa 159*

na Allamano alianzisha Mashirika mawili, kwa jina la Consolata Mtakatifu sana, tusemeje, kwa jinsi ya ari gani alijitahidi kupenyeza ndani yetu ibada ya B. Maria! Tulikuwa na hakika kuwa, kwa mfano wa Mt. Alfons aliweka ahadi ya kuongea kuhusu B. Maria katika kila hotuba yake.

Aidha sikukuu za B. Maria, alizotaka kusherehekea kwa ibada kubwa sana; - na ibada ya mwezi Mei, aliyohimiza kwa maneno motomoto; - na mafundisho yake ya Rozari takatifu; - na Sala ya Kanisa ya B. Maria Consolata, aliyotunga mwenyewe kwa ajili ya jumuia mbili za Mashirika, kwa kuwa: "*sala rasmi ya Shirika, ambayo kwa njia yake wangeweza daima kupata neema zote*"... hayo yote yanaweza kudhihirisha mazingira ambamo Allamano alitaka tuishi, yaani yamejaa ibada ya B. Maria.

Ili macho yetu yakazane kwa urahisi juu yake na kutaja daima jina lake, aliweka sanamu yake katika kila chumba cha nyumba asili, hata kiwanjani; halafu tena alitaka atawale toka juu katikati ya nyumba, kubainisha jinsi Consolata alivyotawala pekee juu ya Shirika, na pia awe moyo wa nyumba: moyo mkuu ambamo damu ya kuhuisha, ya neema, ikitoka katika kichwa Yesu, daima iwafikie kila mwanaushirika kwa ajili ya kupata matunda ya utakatifu na ya utume.

Na haikosi hata moja kati ya barua nyingi alizowaandikia wamisionari na masista

*Ukurasa 160*

wa Consolata, na pia kwa watu wenye ibada, kuwa pamoja na sahihi yake, kutaja jina la Consolata, akiombwa kubariki, au kwa faraja. Ilikuwa kawaida yake: kuingiza katika maandishi, kama vile katika mazungumzo, jina la B. Maria Consolata kama hali ya kiroho ya kupendeza. Roho yake ilipumua ibada hiyo. Hakuweza kutoka nyumbani bila kupita kumheshimu B. Maria Consolata, na vile aliporudi. Jumamosi ya Mateso, hakukosa kusalimia sanamu kabla ya kuifunika, wala kuwemo Jumamosi Kuu ilipofumbuliwa. Alitaka ibada hiyo aifanye Prefekt wa Sakristia, akivaa kota, akisema kuwa si jambo dogo. Na siri ngapi ingeweza kufunulia kijukwaa cha Kanisa, ambamo Allamano alizoea kwenda kusali na kubaki masaa na macho sanamu pendelevu ya Mama wa faraja.

Miezi michache kabla ya kufa, walipoomba kwake kwa ajili ya Novisiati sanamu ndogo ya Consolata – iliyowekwa miguuni pa kitanda chake wakati wa ugonjwa mkuu mwaka 1900 – Baba mwema hakuweza kukataa. Akaenda kuichukua, akaitazama kitambo kirefu na macho ya upendo, akaibusu kwa upendo mkuu halafu akaitoa. Ilikuwa kama kukabidhi mwenge: ule uliowaka moyoni mwake, na uliopaswa kukabidhiwa kwetu ili kuangaza na mwanga wake – kwa njia ya utume wetu – waliotembea gizani mwa upagani, na kwa moto wake kuhuisha waliokaa katika uvuli wa mauti!

*Ukurasa 161*

**Tajiri kwa maskini**

Tunachojua kuhusu ufadhili wa Allamano, ni kidogo sana kati ya mengi sana. Naam, alikuwa daima anajali usijue mkono wa kushoto analotenda wa kulia. Aliyotaka na hata kuamuru waliofadhiliwa ilikuwa ile moja: wasiseme neno. Na walio wengi hawakusema hadi kufa kwao.

Wa kwanza wa kufaidia fadhili yake – tulikwisha ona - walikuwa mapadre, ambao aliwaita "maskini wa kwanza". Naam, tunajua kuwa aliwatuma mapadre kwa mshonaji ama kwa ajili ya kanzu au kwa ajili ya koti kubwa, naye akawalipia. Mara nyingine akikutana na mmoja asiye na hali nzuri, alimwingiza chumbani mwake na kushurutisha kuvaa kanzu yake, mapya au karibu mpya. Kwa ajili ya wengine waliosali Misa katika Kanisa la Consolata, aliongezea, ya kwake, zaidi ya sadaka ya Misa. Na kwa mapadre wengi wa Chuo aliwalipia karo ya bweni, na kwa walio maskini zaidi hata fedha ya kulipia bakshishi ya watumishi. Nalo pia kwa mapadre na walei waliokwenda Mt. Ignas kwa mazoezi ya roho. Na tena, daima ilikuwa fadhili ya namna ya kikristo: asiwaibishe aliyefadhiliwa, kwa kisiri.

*Ukurasa 162*

Zinajulikana misaada ya ukarimu kwa familia maskini wasiothubutu kuomba. Na watu waliopata hasara ya mali, alikopesha kiasi kikubwa cha fedha, bila kudai baadaye. Hata wale wasioweza kurudisha kwa wakati waliopatana, Allamano hakuonyesha kuudhika kamwe, mbona aweze kufaidia roho zao. Aliwalipia kodi ya nyumba akina mama wazee, ili wamwombee. Wagonjwa maskini aliwashughulikia madawa, na hata ilichoweza kuwatuliza; bali wengine aliwalipia hata majuma mawili ya tiba baharini.

Kwa ajili ya fadhili nyingine alitumia mtumishi, ambaye alimpa bahasha zenye fedha ya kuwapelea wagonjwa hospitalini, au familia maskini katika dari ghorofani, akiwafundisha hususan namna ya kujimudu ili kutambua shida za maskini wale, na halafu kumtaarifu ili aweze kuwashughulikia.

Haishangazi, basi, kuwa walikuwa wengi maskini waliobisha mlango wa Consolata kila siku, wakiomba kan. Allamano, au kumwomba njiani, au kumpeleka maombi yao. Wote walijua kuwa kanoni mwema hawakumwendea bure. Wala haishangazi kuwa wanaomshangilia wawe na umoja kusema kuwa: "Allamano alitekeleza upendo katika upana wake wote kadiri ya sifa anazotaja Mt. Paulo.

*Ukurasa 163*

**Maskini kiwa ajili yake**

Tajiri kwa ajili ya maskini, kan Allamano alipenda na kutekeleza umaskini kwake mwenyewe. Hakuwahi kutafuta fedha kamwe, na alipinga tabia ya choyo. Alisema:"*Tabia ya uchoyo itatukosesha hususan ahadi tuliyoweka tulipopata daraja ndogo ya Kipara, ingetuzuilia kutekeleza wajibu zetu, na kutuingiza katika dhambi nyingi*". Aidha aliwaonya mapadre vijana:

ambao, watakapokuwa maparoko, wajihadhari kujazia nyumba na ndugu, au kukwama katika biashara yao, kontrakti, n. k.. Alisema: "*Ikiwa ndugu wanahitaji, afadhali kuwasaidia toka mbali. La sivyo ni kunyima wakati kwa roho, kuathiri maskini na Kanisa, kuharibu maisha yake mwenyewe, kubatilisha huduma yetu takatifu, na baada ya kufa.... ole wao mapadre matajiri!*".

Askofu Gastaldi alipodokeza ukarabati wa Kanisa la Consolata kwa Allamano, alimwambia: "Wewe una fedha, weka kwanza ya kwako, halafu Bwana atatekeleza yaliyobaki".

Allamano akafuata shauri na kutumia ya kwake, tangu karabati ya kwanza, sio pungufu ya lira arobaini elfu. Halafu katika kuanzisha Shirika amemaliza yote aliyokuwa nayo, akiuza haya manyumba, pamoja na nyumba ya shambani alipokwenda kila mwaka kupumzika kidogo.

*Ukurasa 164*

Orofa yake Consolata ilipangwa na machache, wala hakuwahi kuruhusu kuboresha kwa namna yoyote. Hivyo kwa mavazi yake: kupendeza, lakini sio anasa. Hakuwa na nyororo ya dhahabu ya saa, bali kamba nyeusi ya kawaida; hakutumia mifuko ya mikono. Safarini aliweka mfukoni nyuzi, sindano na vifungo, ikiwa inatokea shida, nalo kwa ajili ya roho ya umaskini. Hakutumia na kutupa kitu ovyo. Akipokea barua, alikata kurasa nyeupe au sehemu, ya kutuimia kwa ajili ya vyeti kwa watu marafiki. Kwa kusafiri sehemu mbalimbali ya mjini, asipokwenda kwa miguu, alitumia mabasi ya manispaa. Katika safari zake kwenda Roma, hata akiwa mzee na mdhaifu hakutumia behewa lenye vitanda, bali daraja ya pili.

Mikononi mwake zilipita mamilioni, lakini hata senti moja ilisimama. "*Sikuwahi kamwe kutafuta fedha* – alisema mwenyewe – *lakini fedha imenikimbilia mimi daima*". Ilikuwa onyo kwa maparoko wapya. Hata katika vipindi vya mahitaji makubwa zaidi, kwa ajili ya Kanisa wala kwa Misioni, hakuwahi kuombaomba. Alitumia Gazeti, lakini kila mara kwa utaratibu sana. Hakukubali kuomba kwa kuchokoza: "*Jumuia na watu fulani wanajivutia hasara kwa namna yao ya kuomba, kudai, kutaka. Watu wanawaona kama wachoyo wa fedha na hawavuti kwa wakarimu*". Hakukubali kubishana: "*Si heshima kwenu. Ikiwa ombi linazidi mno, kurasa 165 tuseme tu kwamba hatuwezi, lakini daima na adabu*".

Ijapo Shirika lilikuwa mboni wa jicho lake, na ijapo alihitaji zana fedha, Allamano hakujionyesha kuelekeza matumizi ya ufadhili kwa njia moja tu. Siku moja alikuja bwana fulani na Lira 500, akiomba sala. "Tutasali – akajibu Allamano – lakini hulazimishwi kutoa lira 500". "Lakini, Bwana Kanoni, mimi nataka kutoa".

"Kama ni hivyo, basi, amua unavyotaka itumike".

"Tazama, maskini wamekwisha kusaidiwa: basi utumie kwa ajili ya Misioni".

Yalikuwa mazungumzo ya kila siku. Mara nyingine sadaka ilikuwa kwa malengo mengine. Siku moja – baada ya kuanzisha Shirika - alipata ufadhili ya Lira 1.000 kwa kazi njema ya hiari. Wakati ule aliingia paroko mmoja akieleza shida yake ya mahitaji, kwa sababu alikuwa akijenga kanisa.

"Chukua – akamwambia Allamano – Bwana ameniletea sasa hivi"

Akampa yote kabisa.

Katika barua yake moja kwa Mkurugenzi wa Shule ya Kitume ya Mondovì, tunasoma: *"Ningalipendelea kuwa mwaka huu wanafunzi wangu watolee ufadhili yote kwa ajili ya Misioni*

*nyingine. Haifai kuwa wachoyo, nami nahisia mahitaji ya Wamisionari wa kila aina".*

*Ukurasa 166*

**Kama mwenge katika kivuli**

Upendo ni mwana wa unyenyekevu. Kujifanya kuwa wote kwa wote maana yake kujisahau binafsi. Basi, makusudi ya pekee ya Allamano, tangu seminarini na daima baadaye, yalielekea dhidi ya "kakiburi", na kupata kufanya kila tendo "bila alama ya kiburi". Yalikuwa mapambano matakatifu alimozoeza roho yake kwa maisha yake yote. Na akafaulu.

Alijihesabia kama chombo tu mikononi mwa Mungu katika kazi zake zote za jitihada; alikuwa Consolata kuangazisha uwezo wake kwa njia ya udogo wake. Kabla ya kuanzisha Ushirika alipatana na Bwana: "*azuie utekelezaji, akiona kwamba yeye angekubali hata wazo moja tu la kujipendelea*". Kila kazi aliyotekeleza alijihadhari kujihesabia kwake kitu, hata kuweza kusema: *"Sikuwahi kujipendelea kamwe".*

Akaongeza:

*"Kuliko kutenda dhambi ya kujivunia, naomba Bwana ateketeze kila kitu tulichonacho, hapa na Misionini"*

*"Katika mizani ya Haki ya Mungu ina uzito zaidi dhambi ndogo, kuliko mema yote tunayoweza kutenda duniani".*

*Ukurasa 167*

*"La, sivyo, mimi si mwanzilishi wa Shirika na sitaki kuitwa hivyo. Aliyeanzisha shirika ni B. Maria Consolata".*

*"Ninyi mnaniita Rekta, lakini Rekta wa kwanza na wa kweli ni yeye, Yesu:* Te Rector, Te Duce (wewe ukiwa Kiongozi, ukiwa Mpasua njia). *Mimi ni mjumbe wake*".

"*Nataka kuweza kufa bila kukubali hata wazo moja tu la kujivunia kibatili*".

Kumtolea sifa ilikuwa kumwudhi, na kwa majibu yake makavu na mafupi, alialika kubadili mazungumzo. Aliepa kupewa heshima, na alifundisha kuwa hasa mapadre wanapaswa kuepa. Hakukubali ukanoni, isipokuwa baada ya kusisitizwa sana na kama kwa amri ya Askofu mkuu.

Daima alikataa kuonekana. Akijificha kwanza kwa muda wa miaka 14 seminarini, halafu kwa muda wa miaka zaidi ya arobaini mahali pembeni katika Chuo, hakuwahi kujionyesha hadharani katika maonyesho ya hadhara, hakuonekana hata katika maandamano ya sherehe, alipopenda kuchanganyika na Wasakristiani, asitambulikane. Siku ya kumtangaza Cafasso Mwenye Heri, katika karamu kwa heshima ya Maaskofu na Wakuu wa Kanisa, yeye alishika mahali pa mwisho, karibu asionekane. Kwa kweli, kwa walio wengi wenye ibada ya Consolata hakujulikana, ila kwa sifa, lakini hawakujua ni nani, na wengi hawakujua hata jina lake.

Lakini alikuwa padre mwenye kuchochea kuliko wengi katika Jimbo kuu la wakati wake, yule aliyeacha nyuma yake kazi muhimu zaidi. "Ni kwamba – anavyoeleza vizuri

*Ukurasa 168*

mons. Pinardi – nuru ya roho inang'aa katika kivuli. Ni kama taa kubwa zinazoelekea kuangaza mbali mbinguni, na kana kwamba hazionyeshi asili zinamotoka. Kan. Allamano hakuwa mtu, wanavyosema, wa kutembea maringo. Kwa hadhara inayojali sifa ya majina, na kutazama sura ya nje, iliweza kukosa sura yake iliyofichika, na kama amechukia kujionyesha. Aliishi maisha yake katika nyumba ya ukimya ya konventi ya zamani, kwa kujikusanya katika chumba chake, akijitenga kama monaki hata kwa mapadre vijana waliolelewa na maongozi ya akili yake na moyo wake. Aliweza kusukiwa bila hata kuonekana, kujua yote karibu bila kuuliza".

**"Abnege!"**

(Jikatalie!). Maisha ya kan. Allamano yalikuwa hasa ya kujikatalia, kusilibiwa. Tusifikiri kuwa hayakuwa na gharama – yeye ambaye alikuwa mdhaifu wa afya hata kutapika damu – kiasi cha shughuli zake nyingi na mahangaiko, ambayo moja tu ingalitosha kumaliza utendaji, hata kuvunja nguvu ya mwili na ya roho ya mtu.

Kujifanya kuwa wote kwa wote, katika mahitaji yote ya kimwili na kiroho, bila kukataa hata mara moja, bila kujihurumia kamwe, na hivyo kila siku, na hivyo kwa miaka hamsini ya huduma ya kipadre.

Na ule utawala wa binafsi ya kushtusha, hata hakuonekana kuudhika wala kuchukia hata mara moja; - upole wake wa kiroho wa kawaida,

*Ukurasa 169*

*Picha*

*Ukurasa 170*

lisitoke hata mara moja kinywani mwake neno kali dhidi ya yeyote yule, wala gumu mno; - ule utulivu wa daima ya rohoni na usoni, hata asionekane na mtu amevurugika, amehangaika, hata katika nafasi ya pekee zaidi, lakini daima mtulivu na mwenye kutabasamu, sawa daima ndani yake.

Huenda alikuwa hakuguswa? La! Tena aliridhi tabia ya nguvu na ya kuwaka mara, na Mungu tu peke yake anajua jitihada aliyotumia, nguvu aliyojitendea ili kufaulu kupata utawala kamili juu yake mwenyewe: tabia, matendo na maneno. Basi hayo yote yanaumiza maumbile. Ni *juge martirium* (kuteswa kwa vikubwa) ya roho zinazotamani utakatifu; mateso kisiri mbele ya macho ya watu, lakini ya thamani kubwa mbele ya Mungu. Alisema siku moja: "*Nami niko vile, nasikia sana; mara nyingi ningalitamani kuwa na moyo mgumu kidogo. Lakini sivyo, afadhali ilivyo, na nafurahi kuwa ni hiyo...*". Ameridhika, kwa sababu amepambana na kuteswa, na pia kushinda na kustahili,

Msalaba wa mateso ya moyoni na rohoni, haukumkosea basi. Alimwandikia siku moja mtu

rafiki: "*Hakika, ningalikuwa na maelekeo kwa ugonjwa wa moyo, ningalikwisha kufa zamani. Kwa muda wa miaka arobaini, tangu nilipo Consolata, nimeona na kuteswa mengi!... na yanayonitesa zaidi ni makosa ya shukrani. Mara nyingine uchungu ulikuwa kiasi kwamba nilitoka damu kinywani. Ilikuwa ikidumu siku chache; hakika; lakini ni kama porojo. Na hakuna aliyejua kamwe.*

*Ukurasa 171*

*Baada ya kupokea nilikuwa nakaa pamoja na Yesu, miguuni mwa Consolata, na pale tulitengeneza yote*".

Na katika barua nyingine "*Mara ngapi katika maisha yangu nilijikuta peke yangu, bila kupata mtu wa kumshirikisha uchungu wa moyoni, nilimwendea Yesu! Naye alinituliza daima, akinipa hamu ya kuacha kutafuta matulizo kutoka kwa watu*". Sala yake, katika nafasi hizo ya mateso makali, ilikuwa kurudia kusema, akiinua macho mbunguni: "*Mungu pekee, Mungu pekee, Mungu pekee!*" na alikiri ya kupata matulizo mara na nguvu.

Lakini hata kujinyima, katika majikatalio ya milango ya ufahamu, alikupokea kikamilifu. Maisha ya jumuia kwake yalikuwa malipizi ya daima, kuanzia kuamka asubuhi mapema, hali tunajua alikuwa akikawia usiku dawatini, wala kuweza kupata usingizi ila baadaye sana. Alikubali mwenyewe kuwa akifanya kazi zaidi usiku kuliko mchana, ili mchana awe tayari kwa watu wanaomtafuta. Na pia kwamba ajiruhusu mapumziko ya muda zaidi, isipokuwa wakati wa ugonjwa. Aliamka saa kumi na moja asubuhi wakati wa baridi; na saa kumi na nusu wakati wa joto.

Ilikuwa hilo – katika kutekeleza jukumu yake - katalio la kwanza alilojiwekea, na kuwashauri wengine: "*Kufuata orodha ya wakati, bila kujali raha, kuvumilia wasumbufu kitubioni au katika sakristia, kujikusanya kidogo, kupunguza sauti, kuongeza saburi na wasaidizi; yote mambo yanayosulubu maumbile na kuvutia baraka za Mungu kwa kazi yetu ya kitume".*

*Ukurasa 172*

Halafu majikatalio ya nje, kadiri ya mafundisho ya Yesu, na mazoea ya Mtume: "*Castigo corpus meum* (Natesa mwili wangu)". Kuhusu jambo hilo Allamano alikuwa wazi. Alilalamikia kuwa siku zetu hizi, wasitake kusikia kusema kuhusu majikatalio ya nje ya mwili, kama mambo ya watawa wa ndani au yasiyofaa hali yetu ya mwili ulio mdhaifu leo hii. Alionya:

*"Ninyi, wapenzi wangu hamtafikiri hivyo. Naam, kwanza majikatalio la ndani, lakini baadaye hata majikatalio ya nje ya mwili".*

*"Mkiwa wamisionari, mnahitaji utakatifu mkubwa na pia neema zisizo za kawaida, ambazo mtapata kwa njia ya sadaka kubwa, hata za mwili".*

*"Mnisadiki: faraja za mmisionari hazipatikani isipokuwa na majikatalio mengi".*

*"Anakosa anayedhani kuwaongoa roho na hata kufanya miujiza bila majikatalio ya mwili: katika kulala, katika chakula, na mengine yote".*

*"Mmisionari asiye na roho ya majikatalio kimatendo, ni mmisionari batili".*

*"Lazima mpate tangu sasa mazoea ya majikatalio, ili kwa wakati wake mweze kufanya sadaka kubwa zaidi, hata kishujaa".*

Naye alitanguliza kwa mfano. Kuwemo kwake tu – jinsi alivyoketi bila kutegemea, heshima ya mwili wake mzima; macho daima yenye soni, kujinyima kila raha, hata kuweka kiti chini ya miguu

*Ukurasa 173*

wakati wa baridi sana – basi, yote katika mwenendo wake yalikuwa kwetu kielelezo cha majikatalio.

Mezani ilikuwa ya majikatalio daima. Masumbufu ya afya, angalihitaji chakula cha pekee, lakini hakutaka kabisa. Ila miaka ya mwisho wa maisha yake kwa kutii waganga. Chakula cha jioni kilikuwa mchuzi kidogo na nusu bilauri ya divai, na hivyo baada ya siku nzima ya uchovu. Ulikuwa mwujiza kweli kumwona kusimama ka kufanya kazi jinsi ile.

Aliumia maumivu makali ya kichwa (migraine) yaliyobadili hata sura ya uso wake. Basi, alijifunga chumbani, na kubaki peke yake, bila kula siku nzima, na hata siku mbili mfululizo. Alitoka akiwa amelemaa kabisa; lakini, bila kujiruhusu hata saa moja zaidi ya mapumziko, alirudi kwa maisha ya jumuia na shughuli za kawaida.

Tunadhani tunaweza kukiri kuwa alitumia hata malipizi za pekee. Hakika, aliyathamini sana. Alisema:
"*Hutakiwa busara, ndiyo, na ushauri kutoharibu afya, na hata kwa sababu wengine wana hisia za pekee kiroho; lakini kwa upande mwingine haifai kudhihaki malipizi makubwa: mshipi wa chuma, mijeledi, n.k. na kuzitaja kama mambo ya enzi ya kati. Hata kidogo, zinatumika hata leo*".

*"Katika jumuia haifai kuyatumia bila shauri la wakubwa; lakini tusipoweza hayo, walau kuyathamini ipasavyo".*

*Ukurasa 174*

*"Mazoezi ya mijeledi na mishipi yanasaidia kujirudi na kujikamilisha".*

*"Afadhali mijeledi inapowezekana, matumizi ya mishipi yawe ya saa kadhaa, mara moja au mbili kwa juma, na sio baada ya kula".*

*Siku moja baada ya kuonyesha kwetu minyororo aliyotumia Mt Cafasso, alitaka tuibusu, naye akaibusu kwa ibada kubwa ya imani, akisema: "Ah, kwa ajili ya kuwa watakatifu na kuokoa roho, lazima kufanya kitu!...* Sine sanguinis effusione non fit remissio!" (Bila kumwaga damu hakuna msamaha).

*Ukurasa 175*

# 4.
# Taji
# la utume

*Ukurasa 176*

“Tunakushukuru daima na popote, ee Bwana mwema, Mungu Mwenyezi wa milele, kwa njia ya Kristo Bwana wetu: sisi tumepata kwake tumaini la ufufuko. Tunasikitika kwa sababu tunajua kwamba lazima tutakufa, lakini tunatulizwa kwa kuwa ulituahidia uzima wa milele. Ee Bwana, uzima wa waamini wako hauondolewi, ila unageuzwa tu. Nayo makao ya hapa duniani yakisha bomolewa, tunapata makao ya milele mbinguni”

*(Mama Kanisa katika*

*Utangulizi wa Misa ya Wafu)*

“Baba Mtakatifu akisikitika kufa mkarimu kanoni Allamano, anamwombea pumziko milele roho teule na tulizo mbinguni Shirika Misioni Consolata”.

Kard. Pacelli

*Sevretary of State wa S.S.*

“Nyie vijana, mbusu kwa jina langu jeneza ile  na wekeni juu ya maiti barikiwa lily la usafi wa Kikristo. Kwa sababu Mtu aliyeondoka, alitunza weupe wa kitoto na kuonja furaha ya utoto safi usioweza kufa kamwe, kwa sababu huishi na kudumu katika Mungu, usafi usiopimika!”.

Kard. Carlo Salotti

*Ukurasa 177*

### Ukatili moyoni katika kishindo cha vita

Vita kuu ya kwanza (1914-1919), iliyokuwa kwa Shirika letu kipindi cha majaribio makali, kwa sababu hiyo ilikuwa pigo zito sana moyoni mwa kan. Allamano. Na kidonda hakikupona tena, wala hakurudishiwa afya tokana na tingiziko ya nguvu.

Kadiri wanafunzi walivyoandikishwa jeshini, walipoondoka (idadi yao polepole iliongezeka hadi kufikia yapata arobaini) imekuwa mzigo unaolemea mabega yake Rekta pamoja na jukumu ya kuongoza nyumba. Kuwatilia moyo wachache waliobaki na kulinda roho njema kwa kufuata

barabara nidhamu na maisha ya jumuia; kuwatayarisha wanaoondoka na maonyo ya kufaa; kutegemeza kiroho na kimwili waliokwisha kuondoka; yote sasa imekuwa kazi yake peke yake, na kazi ya kila siku.

Baba mwema aliteseka kikali; kila neno hususan vita lilifuta usoni tabasamu ya kawaida. Zaidi sana usiku mateso yalimzuilia mapumziko haba. Alisema wazi: "*Hakika nateseka, na nikifirikia usiku, nashindwa kupata usingizi hadi ninapokwenda kumwamkia Yesu katika Ekaristi. Hapo napata usingizi, kama Yohane kifuani mwa Yesu*". Hata sikukuu zilipoteza heri zake

*Ukurasa 178*

iliyokuwa furaha ya nje: "*Tu kama Waebrania Babeli; hatuwezi kucheza na kuimba nyimbo za furaha*". Na akijibu heri ya sikukuu: "*Nazipokea, naam, lakini kwa kweli huzuni niliyo nayo moyoni kwa sababu ya wapenzi wenzetu wengi walio mbali, inaongezewa*". Barua alizoandikia askari zinahesabika kwa mamia, na zilikuwa za baba mwema kuliko wote, na kuwapa mema yasiyopimika. Lakini aliwapa mahitaji ya kazima, na kadiri alivyoweza, hata raha zinazowezekana kwa maisha ya taabu ya kijeshi katika mazingira yale.

Mahangaiko mengine yalimjia kama Rekta wa Chuo na Kanisa la Consolata. Naam Chuo kilifungwa tangu mwaka 1916 kwa kukosa wanafunzi – na Allamano aliweka nyumba kwa ajili ya mapadre wanajeshi – na katika Kanisa la Consolata ibada zilifuatana kwa nyongeza ya pekee; hali kila siku ya mwaka na kila saa mahudhurio ya wenye ibada walikusanyika kusali miguuni pa Mama wa faraja. Na Allamano alijiunga na machozi yale kama ni yake, na kuyatilia thamani ya zake, sala zile zote. Alisema: "*Nikiwa Rekta nalemewa na majonzi hayo yote na zala hizo zote za wenye ibada kwa Consolata*". Wengi pia walimwendea, ama kwa ajili ya misaada ya mwili, ama kwa shauri na faraja, ama kwa kuomba sala zake na kupewa baraka yake.

*Ukurasa 179*

Kuwa kujaza kikombe cha uchungu ilikuja Februari 1917, jeshi kushika sehemu ya nyumba asili; halafu mwezi Juni kifo cha kwanza vitani, Frateri Eugen Baldi (alizaliwa Castigliole d'Asti 1895); halafu tena Januari 1918 kifo cha P. Umberto Costa Kiongozi wa nyumba asili (alizaliwa Cirié mwaka 1885. alikuwa mmoja wa mwanzoni. Kwa ajili ya akili yake ya ajabu na ibada thabiti, mwenye tabia ya maadili na asiyechoka kazini, alipewa madaraka daima muhimu hadi kuwekwa kuongoza jumuia kwa jina la Kiongozi).

Tukiongeza juu ya hayo yote mahangaiko kwa kuzidi namna ya kutisha mahitaji, hadi kukosekana mkate, tunaweza kufahamu ukali wa mateso moyoni, ya daima ya Baba; mateso yasiyopata tulizo isipokuwa na mwenendo mwema wa wanae jeshini, na zaidi ya kuishi katika mapenzi ya Mungu. Alisema: "*Ukweli mmoja unatawala daima rohoni mwangu, ni kulingana na mapenzi matakatifu wa Mungu. Na hilo sio kuhusu nafsi yangu, lakini hata kwa ajili ya Shirika. Nikifiri majaribio yanayotuponda leo hii, ningeshawishiwa kukata tamaa. La, sivyo, Shirika ni kazi ya Mungu na itapita katika majaribio hayo yote ili kuchanua upya kwa namna iliyo bora*".

"Nitakumbuka daima – anaandika P. Sandrone – tukio la majonzi, karibu na kitanda cha P. Costa. Alikuwa mahututi, na jumuia ya wanafunzi vijana pekee na mafrateri wachache,

*Ukurasa 180*

walisali kanisani sala za wanaokufa. Mimi nilimwangalia mgonjwa, na saa ile nilipaswa mimi nami kwenda jeshini. Rekta, akiwa na machozi na kwa sauti ya majonzi alikuwa anamwita mgonjwa. Nikipaswa kuondoka, nilimjongea na kubusu mkono. Kati ya mapadre watano waliobaki, alikuwa akiwapoteza wawili kwa mpigo mmoja: mmoja alimpoteza kabisa, na alikuwa yule ambaye juu yake aliweka matumaini yake kwa baadaye ya Shirika. Alinishika mkono kwa nguvu, na kwa kwikwi aliniambia:

“Nawe tena?!.. Nenda tu..., nenda na ukatimize wajibu wako!”

Alionekana sanamu ya uchungu. Lakini roho yake ilikuwa tayari, kwa sababu akiinua macho mbinguni, akaongeza:

“Mapenzi ya Mungu yatimizwe!”. Dakika chache baadaye roho ya mpenzi P. Costa ilikwenda kifuani mwa Mungu, kupokea tuzo la taabu na mateso yake.

**Faraja toka mbinguni**

B. Maria Consolata hakukosa kumpelekea faraja kidogo kwa fadhili za ajabu. Kwa ulinzi wake wa kimama alijionyesha kila wakati tangu kuondoka kwa wamisionari wanne wa kwanza kwenda Afrika. Kwa sababu ya uchelewaji usioeleweka, wa kupokea vyeti toka Roma, hawakuweza kupanda meli iliyolipiwa nauli:

*Ukurasa 181*

ambayo siku chache baadaye ilipigwa na kombora baharini, asiokoke hata msafiri mmoja. Na hivyo, karibu sawa na hiyo ilitokea baada ya muda kidogo, kwa mizigo ya thamani kubwa sana.

Pia hususan usalama wa uhai wa askari zetu, ulionekana ulinzi kama wa mwujiza wa B. Maria. Tazama, kwa mfano, yaliyomtokea P. Occelli. Alikuwa pamoja na askari wanne, na mmoja wao frateri, katika banda mojawapo wanayotengeza haraka huko na huko kufuata mahandaki. Hawakuwa na kinga sana, lakini walipaswa kubaki. Siku moja alipokuwa akimwandikia barua Mkubwa wake, ghafla ikalipuka gruneti. Banda ikaruka angani na wote kurushwa ovyo. Kwake P. Occelli barua ikachanwa vipande vipande, na karatasi nyingine, na kung’oa kofia ya chuma kichwani, lakini mengine.... hakuna kuguswa!. Akitishwa, katika moshi, akitiwa uziwi na mlipuko, anatafuta watu wake. Mmoja, aliyekuwa karibu naye, amechanwa vipande; wawili wengine walitoroka kwenye ulinzi; wanakutana yeye na frateri waliotafutana.

P. Sandrone, tuliyemtaja hapo juu, nchini Albania alipatwa na malaria na hali yake kuwa mbaya sana, alipanda meli kwenda Italia akitumaini kupata nafuu. Lakini alipofika Altamura, alipoteza nguvu zote; zaidi ya malaria ikaongezeka na nephritis (ugonjwa wa mafigo). Baada ya siku chache za

*Ukurasa 182*

kulazwa hospitalini, macho yalipofuka, na miguu ilianza kuwa baridi, na kukauka, hata Sista nesi akimwona na kijaribu kumtingisha mara kadhaa, alisema: “Amekufa!”; akafunika uso wake na suka. Kumbe yeye alikuwa akisia vizuri kabisa yaliyotokea kando yake, lakini hakuweza kutoa ishara yoyote ya uhai. Imekuwa baadaye, walipotaka kuhamisha katika mortuari, alifaulu kufanya tendo fulani. Mara wakamdunga sindano naye akaamka kama kutoka kwa usingizi mzito. Dakika ile aliona, kama katika maoni ghafla, altare ya Kanisa la Consolata na sanamu takatifu, iking’aa mwangaza. Toka dakika ile hali ya afya yale ikaboreka, na haraka katika siku kumi na tano aliweza kwenda Roma, kujinga ka kikosi chake cha afya, na kufanya kazi hospitalini Celio. Alipomsimulia tukio kan. Allamano, yeye alisikiliza akitabasamu, na kuongeza:

“Ah, hujui kuwa kila siku tulikuwa tunawaombea?”

Aidha, neema walizopata askari kutoka kwa B. Maria Consolata, zilikuwa nyingi sana. Kila siku ziliongezeka *ex voto* (moyo wa fedha au picha) za shukrani za wenye ibada; na hadi leo anayetaka kuziona, angeona jinsi zilivyo nyingi zinazodokeza matukio ya vita. Na si wachache kati ya waliojaliwa, baada ya kumshukuru B. Maria, walikuwa wakipita kumshukuru

*Kurasa 183*

kan. Allamano, ambaye lakini alikuwa akizihesabia “sala za Wamisionari”.

**Kifo cha Mwanzilishi Msaidizi**

Baada ya mauaji na uharibifu mwingi, mateso mengi na machozi mengi, hatimaye ilipambazuka siku ya burudisho kwa dunia, pambazuko ya amani.
Kisha kumaliza mapigano na wanajeshi kurudi nyumbani, iliwezekana kufungulia tena Chuo cha mapadre. Tena hata Shirika la Misioni ikachukua tena mwendo wake. Italia, miito ya kimmisionari iliongezeka ya kufariji sana, hata kuwa lazima kufungua nyumba nyingine. Afrika, baada ya Misioni mbili za Kenya na Kaffa, iliongezeka ya Iringa, iliyokuwa sehemu ya Vikarieti ya Kitume ya Daressalaam, katika Afrika Mashariki ya Ujerumani (sasa Nchi ya Tanganyika, walipofukuzwa wamisionari Wabenediktini, raia Wajerumani).

Motomoto huu wa kazi, ilikuwa faraja kubwa kwa Allamano, lakini pia uliongeza taabu zake, hali afya yake ilitikiswa na kazi nyingi mno na mateso makali ya rohoni ya vita. Na tena wakati huu kilitokea kifo cha msaidizi wake hodari, kan. Yakobo Camisassa (Alizaliwa Caramagna Piemonte tarehe 27 Septemba 1854, aliyetimiza naye masomo katika Oratorio ya wasalesiani wa Torino, na halafu kuingia seminarini ya Jimbo kuu. Alipata upadirisho

*Ukurasa 184*

tar. 15 Juni 1879 na Mons. Gastaldi. Akiwa na akili kali sana, mwaka 1889 alichaguliwa, kwa kupigwa makofi, Dakta Mshiriki wa Theologia na baadaye Dakta wa Jopo la Fani ya Sheria mbili. Mwaka 1892 aliteuliwa kuwa kanoni wa Kanisa Kuu. Baba Mt. Pius X akamtakia kwa kusisitiza sana Uaskofu, lakini katika unyenyekevu wake daima alikataa, kuendelea na kazi yake karibu na kan. Allamano. Kazi yote ngumu ya uhasibu na mipango – ya Kanisa la Consolata na ya shirika na ya Misioni – yote yalikuwa kazi yake pekee).

Pigo la kwanza la hatari la ugonjwa lilikuja mwisho wa Juni 1922. Alikwenda katika

nyumba ya Rivoli, lakini hakupata nafuu yo yote. Mara tena pigo jingine kali zaidi lilishurutisha kupumzika kabisa na asiondoke kitandani. Tunaweza kutambua fadhaa yetu sisi na ya wale wote waliompenda. Allamano aliteseka ajabu kama pigo katili. Tarehe 23 Julai baada ya kutujulisha hali mbaya ya ugonjwa na kutushauri kusali, aliongeza: "*Lakini ikiwa B. Maria hataki kutujali mwujiza... basi, tutapata mwombezi mbinguni, kwa sababu yeye amejaa mastahili. Lakini, mnaelewa kwangu mimi jinsi ilivyo... mimi ni mzee...*". Na hapo majonzi yakamshika kiasi kwamba alikabwa shingoni, asiweze tena kusema neno.

Naye kwake mgonjwa sikitiko kubwa lilikuwa wazo la kufikiri jinsi Allamano angeteseka kwa kutengana naye. Kila mara alipompa baraka, aliipokea kwa unyenyekevu, halafu alikuwa akishika mkono wake na kuubusu, kama kutaka kudhihirisha kwa njia ya busu ile upendo wake aliokuwa nao kwa muda wa miaka arobaini na miwili daima naye.

*Ukurasa 184*

*Picha*

*Ukurasa 185*

Katika sikukuu ya Kupalizwa B. Maria mbinguni, ameonekana amepona kama kwa mwujiza: alikuwa akiongea na kueleza mambo mkakamavu; hewa ya kiroho ilizunguka. Halafu ghafla aliwaambia masista waliosaidia:

"Siku tatu...na mtaona".

Siku tatu, Agosti 16, Ijumaa saa mbili jioni aliacha nchi ya ugenini kwa mbinguni.

Wale wanafunzi wachache wa nyumba asili (wengine walikuwa Mt. Ignas likizoni), walipoitwa kwa njia ya simu, walifika Consolata, Allamano alikuwa akitoka wakati ule chumbani mwa marehemu. Hatutasahau sura yake wakati ule, alionekana kama sanamu ya nta. Macho yake yalikuwa safi. Tukakusanyika kandokando yake kwa ishara ya upendo, kana kwamba tumetaka kutuliza uchungu wake. Alitaka kuongea na akasema:
"Mpendwa wetu Makamu...".

Lakini hakuweza kuendelea. Roho ilikuwa tayari, lakini mwili dhaifu. Aliashiria mbingu na kuinua macho ya machozi; na katika macho yake mapendo yote kwa marehemu, na majonzi ya moyo na mlingano kamilifu na mapenzi ya Mungu. Halafu alikwenda, akiinama kichwa, chumbani mwake. Tulitaka kumsindikiza:

"Bwana Rekta, uturuhusu kukaa pamoja nawe usiku huu".

"Hapana, wapenzi wangu, Mungu ananitosha".

Akajifunga chumbani mwake na upweke.

*Ukurasa 187*

**Mkutano mkuu wa kwanza**

Kifo cha kan. Yakobo Camisassa ilikuwa hasara kiasi kikubwa, hasa kwa sababu ilikuwa kabla ya Mkutano mkuu wa kwanza wa Shirika. Tulikwisha sema jinsi kan. Allamano alikwisha dhihirisha nia yake ya kujiudhuru kwa kuongoza Shirika, na kudokeza shauri Roma, akieleza kuwa shirika limeweza kujitegemea. Lakini daima alishauriwa asifanye. Imekuwa hasa baada ya vita, na hasa kwa sababu ya afya yake dhaifu kwamba aliweza kukubaliwa kuitisha Mkutano mkuu.

Mkutano ulikusanywa Novemba 1922. Ilipofika wakati wa kupiga kura kumchagua Mkuu, kan. Allamano hakuweza kukubali tena madaraka, akitoa sababu zote ambazo unyenyekevu wake ulimshauri. Kumbe amechaguliwa kwa kura ya wote pamoja, wasiweze kwa kupiga makofi walivyotaka.

Hapo, akasimama na akishirikisha na machozi, alirudia sababu alizofikri watakubali, na kuomba sana Mapadre wamchague mwingine. Lakini hata kura ya pili ilimwangukia kwa umoja, ijapo walikubali kurudia kwa heshima kwake. Matokeo, kama ile ya kwanza, wala isingalikuwa tofauti

*Ukurasa 189*

warudie mara ngapi.

Naye akaelewa, na akipanua mikono kama kwa kukumbatia msalaba, alisema: "Mapenzi ya Mungu yafanyike!".

**Jubile ya kipadre**

Jubile ya kipadre ya kan. Allamano ilitokea tarehe 20 Septemba 1923, naye akajitayarisha kwa kujikusanya na katika sala. Ilikuwa nia yake sherehe iwe na tabia ya kusanyiko ya kinyumbani ya sala, kama mkusanyiko wa waliobaki wenzi wa shule: kumi na mmoja jumla yao. Na Mons. Ressia aliyeshauri kukusanyika Mondovì, Allamano akajibu: "*Tu wazee na tumechakaa; Mondovì tungewashangaza watu. Kumbe Torino na hapa Consolata hatutaonekana. Mimi nitaadimisha Misa nawe utasema maneno machache, na kwa Baraka ya Ekaristi tutafunga sherehe yetu*".

Lakini sherehe – na isingeweza kuwa tofauti – imegeuka kuwa maonyesho makuu ya upendo na heshima toka kila tabaka ya watu. Gazeti la Misioni – ililochapwa kama toleo la pekee - liliweza kujipamba na barua ya mkono wake Baba Matkatifu Pius XI: ukurasa wa ajabu, ambao peke yake ungalitosha kuangaza kikamilifu sura ya kan. Allamano katika ukamilifu wa fadhila zake

*Ukurasa 189*

na ukuu wa kazi zake; na kwa kuwa neno la Wakili wa B. W. Yesu Kristo, limekuwa na mamlaka kupita sana na thamani ya kushinda tuliyoandika au kuweza kusema hususan Mwanzilishi wetu.

Pamoja na Maandiko ya Baba Mtakatifu, zilikuwa kama taji la heshima nyaraka kumi na tano za Waadhamu Makardinali wa Kanisa la Roma, kila moja umekuwa ishara mpya na tukufu ya sifa kuu kwa Allamano alivyoheshimiwa. Bahati mbaya, kati ya sauti nyingi, sauti moja ilikosekana, ile ya Mchungaji wa Jimbo kuu. Kard. Richelmy, aliyefariki mwezi mmoja kabla, tarehe 10 Agosti, alipojitayarisha kuandika kwa ajili ya gazeti ushirikiano wake wa kushangaza.

Kati ya ujumbe wa wengi uliomfikia aliyesherehekewa, hatuwezi kusahau ujumbe toka mbali Misioni za Afrika, bila shaka mmoja uliompendeza zaidi moyoni mwake wa kibaba. Katika kila Kituo cha Misioni walisherehekea  na ibada rasmi, Komunyo za hadhara, sala za hadhara, hotuba ya ukumbusho, na tena kwa siku ile Batizo na adhimisho za ndoa za Wakristo, ili kuzidisha hafla ya sherehe.

Akiguswa sana, kan. Allamano aliwaandikia Wamisionari na Masista Waraka kwa wote, kama inavyostahili Baba mwema sana,

*Ukurasa 190*

kustahili hasa mtu mtakatifu, na imekuwa kama wasia yake. Tunaleta sehemu kadha wa kadha:

*"Na moyo uliojaa faraja niliadhimisha miaka hamsini ya upadirisho wangu. Kwangu*

*ilikuwa neema ya pekee, nisiyoweza kutarajia, nisiyostahili, na wema wa Mungu pekee alitaka kunipa. Udhaifu wa kawaida wa afya yangu, na majukumu mengi katika nyakati mbalimbali ya maisha yangu zilipunguza mara nyingi nguvu yangu; lakini Bwana alinitunza hadi siku hiyo kwa kunipendelea kuliko wenzangu wengine wenye afya bora kuliko mimi.*

*Nilipojitayarisha kwa sherehe kwa njia ya mazoezi ya roho, niliweza kupitisha neema nyingi ambazo Mungu mwema alinijalia. Ya kwanza ya zote: kuweza kuadhimisha Misa takatifu karibu siku zote, na baraka zitokazo kwa ajili ya mwenye kuadhimisha. Halafu nyingine nyingi za kiroho na za kimwili nisizoweza kuhesabu:* Enumera stella si potes (Hesabu nyota ukiweza).

*Madaraka mangapi nilibeba kunilemea! Lakini Mungu ndiye aliyetaka, na neema yake ilikuwa pamoja nami:* Gratia Dei mecum (Neema ya Mungu pamoja nami). *Yeye alitaka niwe Kiongozi wa roho seminarini, halafu Rekta wa Chuo cha Kanisa na wa Kanisa la Consolata, na baadaye chombo cha utakatifu wenu, na kwa ajili ya wokovu uokovu wa roho nyingi za wapagani.*

*"Ikiwa mahali pangu angalikuwako aliye mtakatifu, kiasi gani cha mema angalitenda na kustahili zaidi! Lakini nafarijiwa na wazo kuwa nimejitahidi daima*

*Ukurasa 191*

*kutekeleza Mapenzi ya Mungu niliyotambua kwa njia ya Wakubwa. Ikiwa Bwana amebariki kazi nyingi nilizoanzisha, hata ya kushangaza, siri yangu ilikuwa kumtafuta Mungu pekee na Mapenzi yake tu, yaliyoonyeshwa na Wakubwa wangu.*

*Hiyo ndiyo faraja yangu maishani, na mbele ya hukumu ya Mungu. Sidhani kuwa ni kiburi kuwa kielelezo na mfano kwenu katika fadhila ya utii. Mnisadikini:* Vir oboediens loquetur visctorias! (Mtu mtiifu ataimba ushindi)".

**"Nunc Dimittis!"**

Wimbo wa shangwe wa kan. Allamano kwa kuadhimisha Jubile ya kipadre, uliandamana na tamaa yake ya mbinguni. Alihisi kuwa utume wake hapa duniani ulitimika na kwamba kazi zake alizoanzisha, zote na mafanikio, aliweza kuzisaidia zaidi toka mbinguni kuliko hapa duniani.

Toka mwaka 1922 alipokwenda Mt. Ignas kwa ajili ya mazoezi ya roho, alitarajia kuwa ilikuwa mara yake ya mwisho kuona kanisa lile alilopenda, lililoshuhudia zaidi ya miaka hamsini ya ibada yake na ari yake. Kabla ya kuliacha, alitaka kukawia kirefu na peke yake kusali kwa kila altare. Alishinda hasa kwenye altare ya Mt. Ignas, ili kumkabidhi mwanzilishi huyo mkuu roho ya kitume ya wanae na mabinti yake wamisionari.

*Ukurasa 192*

Mwaka 1923, matembezi yake Shirikani, tena kwa sababu ya afya yalipungua, na amesikitika. Miezi ya mwisho wa mwana 1924, kwa shauri ka waganga – waliotaka kumwezesha kwenda Roma katika msimu wa joyo unaofuata, kwa ajili ya kumtangaza Mwenye Heri Cafasso – hakuondoka tena chumbani. Msimu ule wa baridi (1923-1924) kwake ulikuwa wa maumivu ya pekee, na alipaswa kulala kitandani mara kwa mara. Kwa mara ya kwanza tangu kuanzisha Shirika

hakuwamo kati yetu katika sikukuu ya Mt. Yosef. Hata katika Kanisa kuu jimboni alikuwa haendi tena. “*Sasa niko kama kioo* – alisema – *na siwezi kutojali magonjwa kama zamani*”.

Zilifika sherehe za kutangaza Mwenye Heri Mjomba, Roma na Torino, na kwa afya yake zilikuwa kama pigo la mwisho. Hakuinuka tena. Tulitambua sisi na wote waliomkaribia. Walifaulu kumshauri kwenda nyumbani Rivoli kwa pumziko kamili. Alikubali shingo upande. Alisema: “*Niko hapo kupumzika, lakini najisikia ugenini. Mbali na Consolata siwezi kuishi*”. Akarudi Torino bila kupata nafuu. Lakini hakuwa na ugonjwa halisi: waganga hawakuuona na walikuwa wakimshauri mapumziko. Alikuwa amechakaa. Ulikuwa mwali unaozimika.

Wala hatuwezi kunyamazisha kuwa licha ya maumivu hayo ya mwili, yaliomgezeka nyakati za mwisho maumivu makali ya kiroho. Mungu aliruhusu hivyo ili kumtakasa zaidi mtumishi wake mwaminifu, ili kuongezea mwangaza

*Ukurasa 193*

wa taji lake la haki, kuvutia baraka maridhawa juu ya kazi alizoanzisha. Hatutafunulia siri nyeti za moyo wa Baba; tutasema tu kuwa naye alikunywa kikombe cha uchungu cha Jetsemani, na kupanda Kalvari, hadi kutamka katika saa ya upweke mkali sana: “*Tazama, imekuwa kwamba zaidi ya taji la mabikira na waungama dini, Bwana Mungu ataongezea la mashahidi!*”.

Ndivyo mambo yalivyokwenda katika msimu wa baridi wa 1925-1926, kati ya mateso mengi kwake, katika sala kwa upande wetu na kwa matumaini kuwa aweze kupata afueni. Kwa kweli, hakuna aliyefikiri kuwa mwisho wake ulikuwa karibu sana.

## Ugonjwa wa mauti

Ghafla mambo yalizidiwa. Ilikuwa tarehe 1 Februari. Asubuhi ile, saa kumi na moja, kan. Allamano alimwita Makamu wa Kanisa la Consolata, kan. Cappella, ili kumwambia kuwa asingeweza kusali Misa: asali yeye katika chumba jirani na kumpokeza Komunyo. Asiweze kusali Misa, imekuwa hadi kufa uchungu wake mkali zaidi. Tangu siku iliyotangulia akijisikia mdhaifu sana, aliomba sista aliyemsaidia amwombee ili kupata neema ya kuweza kusali Misa hadi mwisho; na akamwambia, kwa kuwa alipokea tu Komunyo:

*Ukurasa 194*

“Ah, kan Cappella leo asubuhi alikula karamu na kushiba, nami akanipa futuru tu!”.

Prof. Battistini Profesa maarufu, mganga, alikuja asubuhi na kuona hali kwa jumla kuwa si mbaya, alimshauri akae kitandani. Na mgonjwa akajibu: “*Sive vivimus, sive morimur Domini sumus!*” (Tukiishi, au tukifa, tu wa Bwana). Siku mbili baadaye, Februari 4, akiona nafuu, alitaka kuamka kusali Misa; kwa aliyemkemea kwa sababu ya jaribio hilo, iliyokuwa zaidi ya utashi kuliko nafuu kweli, alimjibu:

“Ni siku tatu sisali Misa!... wao, waganga, hawajui maana yake nini kuacha Misa. Napokea, ndiyo, lakini Misa!...”.

Siku ile Misa hakuweza kuisali, na hakuisali tena.

Tarehe 5 Februari, mganga, akiona hakuna kitu cha pekee kibaya, alimruhusu kuamka kidogo alasiri. Alijaribu, lakini hakuwa na nguvu. Usiku ule, wa mwisho bila msaada, amehangaika sana. Akitaka kutelemka kitandani, ameshindwa. Alipata nafasi ya kupiga kengele ya mtumishi, naye mara akakimbia na kumwona chini ametetemeka kwa baridi.

Februari 7, waganga walikutana kushauriana. Wakaamua kuwa mgonjwa mpendwa angeweza, isipokuwa kupona, walau kupata afueni kidogo.

*Ukurasa 195*

Kanisani Consolata walizidisha sala. Mgonjwa kwa upande wake alibaki tulivu; uchungu pekee: Misa!

Alisema: “Naam, naam, ni kitu muhimu kupata Misa na kupokea, lakini hakuna kifani na kuweza kuadhimisha Misa”.

Tena Februari 8, sista usiku akitaka kumpa dawa ya kutuliza, alimwuliza:

“Lakini, kweli kuna ruhusa ya kuvunja mfungo?... Sijafanya sadaka kubwa kiasi hicho: nisiweze kusali Misa na kupokea bila kufunga! Lakini bado kidogo tutasali Misa ya milele...”.

Pamoja na wazo la Misa lilimsindikiza lile la Misioni.

“Nawaombea, – aliwaambia mapadre na Masista – kwa ajili yenu ka kwa ajili ya wale walio Afrika. Ndiyo jukumu yangu ya daima... siwezi mengine”.

Na kwa Wakubwa wa Shirika waliomwahidia sala:

“Ndiyo, mniombeeni. Mnaona maisha haya machache yaliyonibaki ni kwa ajili yenu... Nimewapa yote!”.

Na ili sadaka ya kuteketeza impendeze zaidi Mungu, aliboresha na utii kamilifu wa mapenzi ya Mungu. Hakuna lalamiko lilitoka kinywani mwake, hata kudhani kuwa hakuteswa. Lakini aliteswa, na kwa sista, ambaye usiku alitaka kumtolea kinywaji, alikata tulizo akisema: “Acha, ngoja hadi baada ya mwamko wa saa kumi na moja.

*Ukurasa 195*

Wangapi wanateswa mateso hayo hayo ninayoteseka mimi. Ah, simo peke yangu kuteswa!”.

Sala yake fupi ya kawadia pamoja na maombi ya Maria Consolata, ilikuwa:

“Mapenzi yako, ee Mungu wangu, yatimizwe!”.

Kwao waliouliza habari za afya, alikuwa akijibu tu: “Mapenzi ya Mungu, mapenzi ya Mungu tu!”.

Wakimwambia kuwa wengi wanamwombea afya:

“La, sivyo, msiombe hilo, sitaki hilo, lakini kutekeleza mapenzi ya Mungu tu!”.

Ijumaa Februari 12, amezidiwa. Waganga walijadiliana. Wakaamua hali yake kuwa mbaya lakini sio bila matumaini. Kwa sababu madawa yalifanya kazi, na hakuna tatizo la pumzi au mapafu. Yote yamekuwa sababu ya umri wake kizee na mwili wake dhaifu. Mons. Gamba, askofu mkuu wa Torino, aliyekwisha kumtembelea, alianzisha maombi ya siku tatu kanisani Consolata. Naye pia Mons. Pinardi alifika mara nyingi kwake, na maaskofu wote wa Pidmont walimpelekea heri zao za dhati ya kupona haraka. Baraka ya pekee ya Baba Mtakatifu ilipokelewa na mgonjwa na ishara za furaha wazi, na kumtuliza sana.

Asubuhi ya Februari 13, mara alipoamka aliomba Mons. Perrachon aliyefika toka Kenya jana yake jioni

*Ukurasa 107*

na alionyesha hamu ya kumwona. Akampokea kwa furaha, na kuzungumza naye muda na kumbariki kwa moyo.

Tarehe 14 alipata saa kadhaa ya utulivu asubuhi, lakini alasiri alizidiwa tena. Makamasi mengi yaliziba koo, akipumua kwa taabu na kukoroma. Sista aliyemwambia kuhusu mwezi wa Mt. Yosef na sala zitakazofanyika, alijibu akiinua macho mbinguni:
“Mapenzi ya Mungu... mapenzi ya Mungu...”.

Siku ya 15, saa tisa asubuhi alitaka wamwite kan. Cappella ili aone pamoja naye kama yote ni sawa Kanisani; halafu karibu na pambazuko aliomba wasali Misa. Ilipoanza, alitaka kupiga ishara ya msalaba, asiweze kupeleka mkono panda la uso. Kwa Injili alitaka tena ishara tatu za msalaba, akitaka kutekeleza hadi mwisho madhehebu hayo madogo. Kabla ya kupokea masista walitaka kulowesha kidogo midomo kabla ya kupokea, lakini alikataa, akisema kwa sauti ndogo: “Naweza bado kumeza”.

Halafu alitaka kuwapokea mapadre wa Chuo, ambao aliwaambia maneno ya kuagana na kuwabariki.

Walipomwambia kwamba alionekana kama bwana arusi, kwa sababu ya nguo nyeupe aliovaa, akajibu:

“Naam, nakwenda arusini ya milele!”.

Na karamu ya milele ilikuwa karibu sana.

*Ukurasa 198*

**Kukumbatiwa na Mungu**

Na tazama, alasiri ya 15 ghafla amekuwa mahututi. Kan. Cappella alionea vema kumpa mafuta matakatifu, ambayo mgonjwa alifuata kwa uangalifu na ibada, maadamu walitayarisha kwa Komunyo pamba. Wakati huu askofu mkuu mons. Gamba, mons. Filipo Perlo, mons. Perrachon pamoja na wakubwa wa Shirika walikimbilia chumbani mwake. Komunyo pamba ililetwa na kan. Cappella akisindikizwa kwa heshima kuu na mapadre wa Chuo, na wanafunzi wa Shirika la kimmisionari, masista wamisionari na wengi watu wenye ibada. Ilikuwa saa kumi na moja jioni.

Wakati wa kupokea kwa mara ya mwisho Yesu mpenzi Ekaristi, mgonjwa alijaribu kuinua mkono. Sista akielewa nia yake, alimwondoa kofia, naye akafurahi. Kwa sala fupi walizomsalisha aliashiria na kichwa, akijitahidi kufahamisha kuwa alipendezwa.

*Ukurasa 199*

Mons. Perlo, ambaye hata siku zilizotangulia alikuwa anamjia mara nyingi sana, tangu sasa hatamwacha tena, akaomba baraka ya mwisho kwa Shirika na Misioni. Aliashiria na ishara nyepesi ya kichwa, hali kwa jitihada yote alitaka kuinua mkono, ulioanguka mara usio na nguvu. Hapo mons. Perlo, kwa niaba ya mgonjwa alihakikisha baraka hiyo ya mwisho juu ya wote waliopiga magoti, halafu mmoja mmoja mapadre wa Chuo, wanafunzi wa Shirika na masista wamisionari walipita kubusu mkono wake mara ya mwisho.

Imekuwa jioni na usiku umefika na kuwashwa na nyota tele zilizoangaza Kanisa la Consolata, lililofungwa katika uchungu. Nje duniani kanival ilikuwa inavuma kelele na nderemo; kifo kile kilichokaribia polepole na ya kuchosha kilionekana kama Njia ya Msalaba, toleo la mwenyewe kwa malipizi ya wengi wanaosahau.

Utungu wa mauti wa Baba ulikuwa utungu wa wana, na kila kwikwi ya anayekufa ilikuwa ikigonga moyoni mwetu. Kwa muda wa saa kumi na mbili, kando kando ya Dhabihu, ilikuwa sala tu. Waliokuwa karibu zaidi waliweza kupokea maneno kama silabi hafifu kama pumzi. Walisikia wazi kusema "*Amen*" kwa kujibu sala fupi; halafu dhahiri maneno: "*Ave Maria*". Ilikuwa salamu ya mwisho ambayo mwana mpenzi alimtolea toka duniani kwa "Mama yake Mpenzi sana",

*Ukurasa 200*

ambaye toka mbinguni alimfungulia mikono. Halafu tena ishara ya kupendelea, baada ya sala walipoanza Rozari kwa sauti.

Kidogo baada ya saa tisa asubuhi alipoonekana kupata nguvu, alifungua macho, kwa namna iliyotupendeza sana, na akazungusha akiwa na ufahamu; halafu akawa mahututi kabisa. Macho yalikuwa yakipofuka dakika kwa dakika. Waongeza sala. Mgonjwa alihisi msalaba midomoni mwake, akajaribu kuubusu. Halafu basi. Uso ulikunjika kidogo... kivuli kizito kilizima nuru hafifu ya macho... na mauti. Ilikuwa saa 4 na dakika 10 ya tarehe 16 Februari, siku ya kuamkia Jumatano ya Majivu, na kwetu sisi, wanae, siku ya kwanza ya Kwaresima itakayorefuka kwa maisha yote, hadi tutakapojaliwa kumwona tena mbinguni.

Wakasali sala za marehemu, kan. Cappella alisali Misa katika chumba cha marehemu, halafu maiti, ikivishwa na mavazi ya kikuhani alipelekwa katika kikanisa cha ndani cha Chuo, na kuwa chumba cha maiti. Saa ile ile iligonga kengele ya *Malaika wa Bwana*, na milango ya Kanisa la Consolata kufunguliwa kwa waamini wa kwanza waliopanda juu kusali *Raha ya Milele.*

*Ukurasa 201*

*Picha*

*Ukurasa 202*

**Ombolezo la moyoni**

Mara kisha kutangaza Torino habari ya kifo cha kan. Allamano, iliwaletea wote mshangao na uchungu, kwa sababu walizoea kumwona, licha ya mtu wa pekee, kama muundo, programu, senta ya amali ya kiroho, asiyeweza kuondoka kamwe.

Chumba cha maiti kilikuwa mara shabaha ya hija endelevu. Maelfu ya watu walipiga magoti kandokando ya maiti ile na kuonja mtazamao wa kifo cha Kikristo, kisicho na uchungu na kitisho, bali kimeonekana kama usingizi wa amani.

Baba Mwema aliyevaa roketi (*kama kanzu fupi ya kikanoni*) na sitola zambarau, mwenye msalaba mkononi, alipumzika. Maiti, kati ya mishumaa mirefu manne ilielekea altare, ambamo juu yake ilikuwako sanamu ya Cafasso akionyesha sanamu ya B. Maria Consolata kwa waamini. Hapo imeonekana kana kwamba Mwenye Heri atabasamu kwa maiti ya mpwa, akisema na tendo lake: "Amekuja kumjongea B. Maria aliyemheshimu". Pia katika utulivu wa mauti kan. Allamano alionyesha kufanana kwake wazi na sura ya Mjomba. Pale, katika kikanisa kidogo, mambo hayo yalitambulikana wazi mara, hadi kuingiwa na hofu ya kusumbua

*Ukurasa 203*

utulivu wa ndugu wa kifamilia wanaokutana: Mjomba na Mpwa walikutana katika utukufu wa Maria Consolata, B. Maria mpendwa waliomtumikia hapa duniani na furaha ya imani.

Mafuriko ya watu walipita kuonja kidogo mazungumzo hayo ya lugha ya mbinguni na amani hiyo; hakuna aliyeondoka bila kugusa kitu, bila kugusa mikono yake na kitu che kuweza kusema baadaye : imeguswa na mikono yake, ni kama zawadi yake kwangu. Mapadre wawili walishughulika kuridhisha matakwa ya waamini, ambao kwa imani yao walitambua kuwa mauti ile haikuleta hasara, bali walimpata mtakatifu.

"Mama – alisikika mtoto kuuliza – kwa nini wote wanamgusa na kitu?".

"Kwa sababu alikuwa mtakatifu".

"Na kwa sababu gani alikuwa mtakatifu?".

"Kwa sababu... kwa sababu hakutenda mabaya yo yote, bali daima alitenda mema mengi!",

Wanawake wawili, wanapoondoka na kuashiria sanamu ya M. H. Cafasso juu ya altare, walishirikishana kifupi:

"Siku moja tutamwomba naye, pale altareni".

"Sio sisi, tu wazee mno".

"Eh, tutamwona bado... wasipomtangaza mtakatifu yeye!".

Mwanamke mwingine anakaribia sista mmisionari:

"Uniambie, sista, mauti inawaachia watu watulivu hivi?"

*Ukurasa 203*

“Ndiyo, wale wanaokwenda mbinguni”.

Na katika majibu hayo yote ilikuwako hakika kamili na thabiti.

Haiwezekani kuorodhesha rambirambi zote zilizofikia Kanisa la Consolata na Shirika la Wamisionari. Toka kwa Baba Matakatifu, hadi mapadre wa kawaida. Toka Wanamfalme wa Ukoo wa Savoia hadi watu wa kawaida wanaojulikana na wasiojulikana, toka kila sehemu ya Pidmont, na mikoa iliyo mbali ya Italia, telegramu, barua na vyeti vya kitambulisho zimefika lundo nzima. Gazeti Katoliki la kila siku la Torino ilikuwa na mistari meusi ya msiba katika kurasa la habari ya mjini, hali *Gazzetta del Popolo* na *La Stampa* yalisifu fadhila na mastahili yake.

**Utukufu**

Heshima ya mazishi, kwa matakwa ya makleri na ya watu imechukua ishara kuu ya utukufu. Naam yalikuwa maonyesho taratibu na ya kushangaza ya maombolezo, ishara isiyosahaulika ya Mtume mnyenyekevu wa ukweli na upendo.

Usiku wa mwisho wa kushinda kwa maiti iliyoheshimiwa katika nyumba iliyokuwa uwanda wa kazi yake ya ajabu, ulikuwa kesha ya ari ya kidini. Wanachuo na Wamisionari wa Consolata walipishana daima bila kuchoka kusali karibu na maiti.

Saa moja asubuhi, kabla ya sherehe ya mazishi, mapadre wahudumu wa Kanisa la Consolata walitaka, na wazo la kitauwa,

*Ukurasa 205*

kutoa heshima ya ibada yao kwa Rekta mpendwa na ibada nyepesi na ya kuvutia. Likibebwa na Wanachuo, na kutangulizwa na wanafunzi Wamisionari na masista wamisionari, jeneza la kan. Allamano, limefunikwa na kitambaa cheusi cha mahameli, lilichukuliwa kutoka kwa chumba lilimokuwa, na kwa maandamano, yakipita katika kiwanja cha nje, kuingizwa katika Kanisa mbele ya altare kuu. B. Maria Consolata, toka juu ya kiti chake cha enzi, alionekana kutabasamu kwa upendo mkuu umati wa waamini, waliosali kwa ibada kwa ajili ya Mtume wao mkuu. Padre Gallea alisali Misa, akisindikizwa na wimbo wa wanafunzi wa Shirika.

Kwa saa iliyopangwa, walianza maandamano ya kushangaza, ambayo daima ikipita kati ya umati wa watu waliosimama pembeni, yamepita barabarani mjini hadi Kanisa kuu la Kiaskofu. Kwa mara ya mwisho kan. Allamano aliingizwa katika Kanisa ambalo kwa miaka mingi lilishuhudia ari yake ya daima na ibada ya kuvutia. Kan. Giuganino, mkurugenzi wa Kazi za Misioni, aliimba Misa, na baadaye kubariki jeneza. Kisha ibada katika Kathedral, mwandamano ulielekea Shamba la Mungu la mjini, ambamo alizikwa karibu na asiyesahaulika kan. Camisassa, mwanzilishi msaidizi wa Shirika.

*Ukurasa 206*

*Tupu*

*Ukurasa 207*

# 5.
# Kungoja
# sauti ya Kanisa

*Ukurasa 208*

**Sauti ya Baba Mtakatifu**

Tunaleta kwa kirefu barua ya mkono wake Baba Mtakatifu Pius XI aliyompelekea kan. Allamano kwa nafasi ya Jubile ya kipadre, na ambayo tumekwisha kutoa sehemu sehemu:

KWA MWANA MPENDWA

PADRE YOSEF ALLAMANO

PIUS PAPA XI

*Mwana Mpendwa, salamu na baraka ya kitume.*

*Ikiwa, tarehe 20 ya mwezi ujao itakumbukwa miaka Hamsini wa upadirisho wako, tunatumia nafasi hii ya pekee na nzuri sana kwa kushuhudia hadharani shukrani yetu kwako, ambaye tunaona unastahili, kwa namna ya pekee, kwa sababu ya mengi mastahili, ambayo wakati wa huduma yako ndefu ya kipadre, ulijipatia mintarafu Kanisa la Mungu, na pia katika mambo ya kibinadamu na kijamii.*

*"Naam, kwako uliyeteuliwa tangu miaka 43 kuwa Rekta wa Kanisa la Consolata, na unandelea kushika wadhifa hiyo hadi leo, na ibada yenye ari kwa Bikira Maria, wakaaji wa Torino wanakutilia stahili ya licha ya kukarabati na kupanua karibu toka msingi jengo hili, sembuse kujitahidi kwa taratibu kulipamba na kazi za sanii na kulifunika na marumaru ya thamani.*

*Ukurasa 209*

*"Sifa hiyo yako, ijapo kubwa, inapaswa kuwekwa nyuma, ikilinganishwa na kazi ya kudumu na ya jitihada uliyofanya kwa muda mrefu: kuhusu kutakatifuza roho za watu, na tena kwa kuhifadhi malezi na utakatifu wa mapadre.*

*"Naam, kwako ambaye umeonekana Mjomba wako stahiki Yosef Cafasso, amekurithia roho*

*yake, mara ulipoanza kazi ya huduma takatifu, Mafrateri wa seminari ya Torino walipata mwalimu wa ibada mwenye hekima; na halafu tangu ulipoanza kuwa Rekta wa Basilika la Consolata ulichukua mwongozo wa Chuo cha Mapadre kilicho jirani, hustaajabisha jinsi ulivyoshughulikia kwa ajili ya kuwapa taaluma na pia fadhila mapadre uliowalea. Na hivyo wamehesabiwa mamia na mamia mapadre – na kati yao wengi maaskofu na maaskofu wakuu – ambao  wanajivunia kuweza kulelewa nawe kwa maisha yanayostahili watu wa Kanisa.*

*Hayo yote lakini tuliyosema kwa sifa, hayakutoshea upendo mkuu ambayo nayo wewe unawaka kwa ajili ya roho za watu: na tazama, katika mwaka 1901 ulianzisha Shirika la Wamisionari, na mwaka 1910 la Masista Wamisionari, yote mawili kwa jina la "Consolata" kwa ajili ya Misioni za Nje. Na kiasi cha Wamisionari na Masista waliokwenda katika nchi za wapagani, ni kikubwa, na wanatekeleza wajibu mgumu wa utume kwa ari, na ijapo walifika wa mwisho shambani, hawaonekani kuwa nyuma ya mashirika mengine yaliotangulia zamani.*

*Ukurasa 210*

*Basi, tukipima mastahili hayo yote, ni haki kutambua jinsi tukio hilo liwaletee furaha moyoni mwa wanamji wa Torino, na pia kwa wanafunzi wako wa zamani na wapya. Kwa heri na pongezi zao tunashirikisha heri na pongezi zetu, pamoja na kukutakia kuwa yanayobaki ya maisha yako yatumike kupatia Kanisa mafanikio makubwa, kwa njia ya ari uliyo nayo iliyo ya pekee kwako. Na sasa, kama dhamana ya neema za mbinguni, na ishara ya upendo wetu kwako, Mwana Mpendwa, kwa Chuo na Mashirika ambayo wewe ni Mkuu wao, tunakupa baraka ya kitume kwa moyo mkunjufu.*

*Imetolewa Roma karibu na Mt. Petro, tarehe 5 Agosti ya mwaka 1923, wa pili wa Utume wetu wa Kipapa*

PIUS PAPA XI

**Sauti ya Makardinali**

Jinsi alivyoheshimiwa Kan. Allamano na Makardinali wa Kanisa la Roma, anatuambia P. Ferrero, ambaye aliwahi kuwa Mjumbe mkuu na Shirika kule Roma: "Nilimsindikiza siku zote Padre wetu kwa waheshimiwa wakuu wa Kanisa, ambamo alipaswa kuwaendea ili kuwaheshimu au kwa mashauri. Wote walimpokea na maonyesho ya pekee ya heshima. Hivyo nakumbuka Kard. Vico ambaye amekuja binafsi kumpokea

*Ukurasa 211*

katika sebule na kukumbatia kwa upendo wa pekee, na kumwambia:

"Ah, kanuni Allamano! Nimemjua kwa sifa, lakini sana nina heri ya kumfahamu mwenyewe binafsi!"

Akamsindikiza ofisini, akishinda naye muda mrefu. Kard. Van Rossum, Prefekt wa

*Propaganda Fide*, alipomwaga, baada ya mazungumzo ya kirafiki, akamwambia:

"Nakushukuru kwa niaba ya Kanisa kwa yote uliyofanya na kufanya ka ajili ya Misioni. Hukupaswa kufanya yote hivyo!".

Katika nafasi nyingine Kard. Bisleti, Mwongozi wa Mchakato ya kumtangaza M. H. Cafasso, alimchukua kwa mazungumzo zaidi ya saa moja na nusu.

Tumekwisha leta katika utangulizi, na sehemu nyingine ya kitabu, maneno ya upendeleo na heshima ya Makardinali wengi wa Kanisa. Tutaongeza tu chache za barua zilizomfikia kan. Allamano katika sikukuu tuliyosema.

Kard. Vinsent Vannutelli, Dekani wa jopo la Makardinali na Datarius (*anayegawia wadhifa*) wa Kiti Kitakatifu, baada ya kukumbuka miaka mia nane ya Consolata, alipopata bahati ya kumtia Taji Sanamu takatifu, aliongeza: "*Ukumbusho huo hautengani na ule wa mpendwa sana Kan. Yosef Allamano, ambaye amejipatia sifa kubwa kwa ajili ya Kanisa hilo, ambalo ni kama amelijenga upya toka msingi, na ambaye daima alihifadhi sana ibada*

*Ukurasa 212*

*ya B. Maria ambayo watu wa Torino huipenda sana. Nilijua, lakini safari ile nilifahamu zaidi, mheshimiwa Bwana Kanoni, ijapo kwa unyenyekevu wako ulijaribu kufunika stahili lako, kazi yako ya hekima na bila kuchoka, sio tu kwa ajili ya kuhuisha ibada hiyo, lakini zaidi pamoja nayo kuhifadhi malezi ya makleri, na kutengeneza Shirika la Wamisionari wa Consolata, ambao matunda ya uokovu katika utume mgumu, wanawaletea furaha safi sana Baba Mtakatifu na idara ya Propaganda Fide. Mafanikio ya kazi hizo zako za kipadre yanaamsha heshima ya kirafiki ya zamani, nisiyoacha kukutolea*".

Kard. Camillus Laurenti, Prefekt ya Idara ya Watawa, alimwandikia: "*Miaka hamsini ya upadirisho wako yananipa fursa ya kukutolea kwako, Mheshimiwa sana, ambaye inaniungana nawe toka muda mrefu hisia ya kiupendo, nakutakia heri nyingi kwa dhati. Mrithi wa roho ya mtakatifu Mjomba wako, ulifanya kazi kubwa sana katika ukimya wa unyenyekevu. Lakini unaweza hakika kufurahi katika Bwana ya kuzidisha kwa uwingi hazina zake ulizopata kwa kuwekewa mikono na Askofu. Mlezi wa vijana wengi kwa kazi ngumu ya upadre, ukawapa nguvu zile hai zinazobubujika moyoni mwako. Mwenye ibada kubwa kwa B. Maria,*

*Ukurasa 213*

*hukutafuta kwa ajili yako peke yako tabasamu na faraja yenye nguvu ya Mama huyo Mpenzi sana, lakini umehimiza ibada yake katika Kanisa linalong'aa ajabu, na kupeleka roho nyingi za wenye huzuni kwenye kiti cha enzi cha Mfariji mwenye huruma. Lakini Mama mpenzi kutoka kiti chake cha enzi anatupia mbali zaidi macho yake yenye huruma, na hakika amekuwa yeye kukupuliza kuwapeleka Wamisionari wa Consolata kwa uokovu wa ulimwengu wa wapagani... Na leo kwa shangwe wa watu wa Torino wako na Italia wanajiunga na sauti yao ndugu wa Afrika mbali...".*

Kard. Alois Sincero: "*Fadhila zinazong'aa, ari ya kitume ya sura hiyo mpendelevu na kuu ya padre zinajulikana popote na kusifiwa, hata Jubile yako huvuka mipaka ya sikukuu ya kifamilia na kuwa sikukuu ya Kanisa Katoliki. Nilipata bahati ya kukutana nawe mara nyingi katika Kanisa*

*la Consolata, miguuni pa B. Maria, ambaye ibada yake imekuwa hamu yako kuu, na daima nilihamasishwa sana...*".

**Sauti ya Maaskofu**

Tumepata nafasi mara kwa mara kuangaza sifa kubwa kwa kan. Allamano kutoka kwa Maaskofu wakuu wa Torino. Mons. Laurenti Gastaldi, Kard. Gaetan Alimonda, Mons. Daudi Riccardi, kard. Augustino Richelmy, kard. Yosef Gamba,

*Ukurasa 214*

bila kusahau mwanafunzi mpenzi wake Mons. Pinardi, na Maaskofu wengine wa Pidmont. Tunajiruhusu kuongeza ushuhuda nyingine za thamani:

Mons. Mathayo Filippello, Askofu wa Ivrea: "*Kan. Allamano nilimwona, na kumthamini, na kuomba kwake ushauri, na majukumu ya wakati ule, seminarini, na baadaye katika ziara za kiuchungaji, yalinizuilia kumtembelea nilivyotamani*".

Mons. Yosef Castelli, Askofu wa Novara: "*Katika kukutana na Allamano daima nilipata hisia ya mtu mwenye hekima, busara, amejaa roho ya Mungu, anayefahamu kikamilifu watu na vitu, akiepa daima kelele na kupatiwa sifa. Kwa hiyo kila mara nilipohitaji huduma ya kipadre au kupata matatizo ya kutatua, hukimbilia kwake na imani, na baada ya neno lake wazi hushika njia aliyoonyesha*".

Mons. Albino Pella, Askofu wa Casale: "*Kan. Allamano nilimwona mara ya kwanza mwezi Septemba 1916, niliposhiriki baraza la Maaskofu wa Pidmont wa Torino na Vercelli. Tangu mkutano ule wa kwanza nilipata hisia ya kuwa mbele ya mtu wa kupita wengine, padre aliye wote wa Mungu. Aidha niliweza kuangalia jinsi alivyomheshimu Askofu Mkuu kard. Richelmy, na pia mwenye kumstahi Mons. Ressia*,

*Ukurasa 215*

*mwenzake wa masomo, Mons. Spandre askofu wa Asti na wengine waliomfahamu kwa muda mrefu*".

Mons. Umberto Rossi, aliyewahi kuwa askofu wa Susa na halafu wa Asti, ambaye kwa upande wake anamtangaza: "*Utukufu wa Kleri wa Torino na wa Pidmont*".

Mwenye Heri Patriarka wa Yerusalemu mons. Alois Barlassina, ambaye kwa muda wa miaka thelathini na tano alihusiana na Allamano kirafiki sana, anakiri kuwa: "*ari isiyochoka, ibada ya kuwaka, busara ya shauri, upendo ambao daima Allamano alioonyesha kwa mapadre wote waliomwendea, ilimstahilia imani na heshima ya wote*".

Mons. Yosef Debernardi, askofu wa Pistoia: "*Kwa upande wangu naweza kusema kuwa kila mara nilipohitaji ushauri wa kuangaza na wa busara, sikumwendea bure kan. Allamano. Alikuwa mmoja wa wale watu ambao zaidi wanajulikana na zaidi wanaheshimiwa*".

**Sauti ya wanafunzi**

Tungetaka kukusanya sauti ya wote ambao kan. Allamano alikuwa Mwalimu wao au Mshauri na Kiongozi wa kiroho, tungepaswa kuongeza maradufu saizi ya kitabu – na hatutilii chumvi. Hatutafanya hivyo, tunawashauri wasomaji kutumia maandiko muhimu ya Maisha kamilifu, yaliyoandikwa kutegemea ushahidi wa makleri wengi wastahiki sana. Hukumu ya jumla tutaleta

*Ukurasa 216*

aliyoandika padre mchaji na mwenye mstahifu Fransisko Tiboni wa Shule za kidini:

"Hisia niliyopata tangu mara ya kwanza na kan. Allamano (1880), kwamba hakuwa mtu kama wengine, bali juu sana ya mstari wa wengine, hata walio wema. Ilinigusa hasa roho yake ya ibada na sala. Bada ya zaidi ya nusu karne, bado inanigonga sikioni mtindo wa tamko la sauti aliyotumia katika sala za kawaida. Hasa, aliposali: "*Benedikta tu in mulieribus*" (umebarikiwa kuliko wanawake wote), hutambulika heshima, ibada na imani, upendo wa kimwana kwa B. Maria. Imenikuzia roho namna ile ya ibada, ustahi, na utaratibu mkamilifu sana wa kuadhimisha Misa takatifu, iliyodhihirisha imani yake hai na kuabudu kwa unyenyekevu. Tena ibada yake iling'aa katika mwenendo wake mzima.

Nilipata nafasi ya kushangazwa na wema wake, latifu na upole kwa majirani na kwa walio chini yake, hata alipopaswa kukemea na kuadhibu; busara aliyojenga katika uhusiano na watu. Kweli alijifunza kutoka kwa usemi wa Bwana wetu: *Discite a me quia mitis sum et humilis corde* (mjifunze kwangu, kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo).

Alikuwa daima sawa na mwenyewe, daima katika amani; na kandokando yake daima alitawalisha amani na nidhamu ya kupendeza.

Katika mwenendo wake alikuwa na usafi wa kimalaika, na katika maneno yake akiitumia daima mzunguko wa maneno ya utaratibu sana akipaswa kugusa hoja nyeti.

Alishangaza na uthabiti wake wa kuzuilia maovu ya kimaadili, hata kitu kidogo, lakini daima

*Ukurasa 217*

*Picha*

*Ukurasa 218*

pamoja na upendo na uangalifu, na karibu ningesema, kwa heshima ya watu; akiwa na sura tulivu daima, na tabasamu kidogo daima.

Na haikuwa pungufu subira yake katika kusikiliza watu, hata wasumbufu, wachokozi na wasio na akili; - alivyoshughulikia manufaa ya watu waliomo nyumbani; - ukamilifu na uaminifu

wake katika mambo ya uhasibu, hasa kuhusu sadaka za Misa; ari yake kuhusu urembo wa nyumba ya Mungu, na hasa ya mwangaza ya ibada takatifu; na hasa roho yake iliyoangazwa, upendo wake mpole sana, hekima yake katika kitubio, zilizomfanya kweli mtu wa Mungu.

Inawezekana kusema kuwa hayo yote, zaidi au pungufu, hupatikana katika kila mtu wa Kanisa aliye kamili. Lakini katika mambo hayo ya kawaida Allamano alitilia kilichokuwa cha kushangaza, yake pekee. Nilifahamu na kuhusiana na mapadre wengine wengi wanaostahili sana, lakini sikumpata mtu wa kulingana naye; tena asiyebaki mbali sana naye. Machoni pangu alikuwa padre mkamilifu kwa kila upande".

**Mweka hazina wa Consolata**

Kwenye kaburi la Allamano haukushuka mtandao wa ukimya, wala uvuli wa kusahauliwa. Licha ya alivyokuwa kwa asasi alizoanzisha – yaani uhai wa maisha yao na dhamana ya kuchanua – walikuwa watu kugeuza kiroho kaburi lake kuwa altare:

*Ukurasa 219*

kuchanua maua mapya ya bustani, yasiyokosekana kamwe, na hasa yale ya kiroho ya maombi, bado akiwa hai, yaliyomfikia kutoka kila upande na daima, kana kwamba ni "mweka hazina wa B. Maria Consolata".

Jina hilo la sifa walilompa watu, kubainisha utume aliotimiza na anaoendelea kutimiza toka mbinguni.

Hakuna mshangao basi, ikiwa baada ya kifo chake waliendelea kuongezeka: kwa upande mmoja maombi ya sanamu zake na za ukumbusho wa Allamano; upande mwingine ishara za shukrani kwa ajili ya neema ambazo walisema walipewa kwa maombezi yake.

Tena hayo, baada ya kutangaza kitabu cha "Maisha" yake – iliyopata idhini ya kila tabaka ya watu: toka Baba Mtakatifu Mkuu wa Kanisa hadi waamini wa kawaida – ishara zilizo za kiasi kwamba ilikuwa kwaya ya sauti za kuomba au za shukrani, hadi kutambua kama uthibiti toka mbinguni wa hisia ya kiimani ya wote waliomwona kan. Allamano kama mgawaji wa pekee wa fadhili za B. Maria Consolata.

Tunasema hayo tukijali inavyotakiwa, kukubali hati na maamuzi atakavyoamua Mama Kanisa, pekee Mwalimu wa Utakatifu anayezalisha daima watakatifu, ambaye ni kwake peke yake kila hukumu ihusu. (Ni mwaka 1938, kabla ya kutangazwa Mwenye Heri)

(Neema zilizopewa na kumhesabia kan. Yosef Allamano, zinatangazwa katika gazeti (MISIONI CONSOLATA))

*Ukurasa 220*

**Uhamisho wa maiti**

Maiti ya Allamano iliposhuka katika kaburi ya Shamba la Mungu la mji wa Torino, hisia ya wote ilikuwa: sio makao yake ya mwisho. Hakuna aliyekuwa na mashaka, hata dakika, kwamba Baba atarudi kati ya wanae: furaha yake hapa duniani na taji lake mbinguni; katika Nyumba ile iliyo

kiini hai na msukumo wa asasi zake muhimu ya kuangazia nuru na imani na maendeleo katika Afrika.

Mashauri yaliyotakiwa yalifanyika mapema, na yalipata matokeo mema, hata kwa sababu ya kibali ya shangwe ya Wakubwa wa Kanisa na wa Serikali. Walingoja tu kwanza, kuweza kutayarisha kilichotamaniwa, kujenga kanisa kwa ajili ya watu, lililounganika na nyumba asili ya Shirika, ambamo kingepata nafasi ya kufaa chumba cha ukumbusho kwa ajili ya kaburi ya Mwanzilishi mpendwa.

Lakini kwa matukio yaliyoingilia kati, na hata kwa sababu ya nyakati ngumu, ikiwa matumaini ya kuharakisha mradi, na, kwa upande mwingine wasiweze kupeleka mbali mno matakwa yaliyokuwa ya wengi sana, iliamuliwa kutengeneza ukumbusho katika kikanisa, kisicho kanisa kamili, lakini kilichojulikana na kutumiwa na watu wa Torino,

*Ukurasa 221*

hasa wa mtaani.

(Kikanisa hicho kina mlango katika Avenue Ferrucci, ambamo kuna makao ya Shirika na kilicho wazi siku nzima)

Jengo limefaulu barabara kiasi kwamba kwa jumla na kwa vigezo vidogo linatekeleza kikamilifu malengo yake.

Basi, mwili wa kan. Allamano unapumzika katika kivuli cha kiroho kama pa mahali patakatifu, ukitunzwa na kuheshimiwa na uchaji na wanae, ukihuishwa na roho na katika roho ya muundo mkuu alioanzisha yeye, na ataendelea kutenda mema. Na sio kwa wanae wamisionari tu, walio karibu na walio mbali, atakuwa mwanga na nguvu ya kufuata mifano yake ya utakatifu, na pamoja dhamana ya utume wenye kuzaa matunda; lakini pia kwa wote watakaokuja kumwaminisha uchungu wao, na kumtolea kwa niaba yake, B. Maria wa Faraja zote, ombi la dhati na lenye matumaini.

Na wote wakiungana – wana na wanafunzi, wafadhili na wapenzi – bado tutaomba ili igeuke kutekelezwa matumaini hai yaliyo leo moyoni mwetu: kumtukuza hapa duniani yule ambaye tuna hakika amekwishatukuzwa mbinguni!

(Matumaini hayo yalitimika tarehe 9 Oktoba 1991 alipotajwa Mwenye Heri, na Baba Mtakatifu Yohane Paulo II katika Kiwanja cha Kanisa la Mt. Petro, Roma – *n. ya edt.*).

*Ukurasa 222*

## YALIYOMO

Kwako Msomaji..........................................................uk. 7

**1. Padre na mtume** ........................................ 9

Baraka ya Mtakatifu - Mwalimu na mtume - Shuleni mwa Mtakatifu mwingine - Saa ya Mungu - Mpenzi wa Yesu - Kilele kuu - Msimamizi wa parokia - Kiongozi wa roho - Dakta Mshiriki - Mtengenezaji (Ukarabati) na Rekta wa Chuo cha Mapadre - Rekta wa Kanisa la Consolata - “La,

Sivyo" ya mtu mtakatifu - Nguvu ya baraka ya Allamano - Kupunga pepo aliyepagawa - Mkubwa wa Monasteri - Mwungamishi mtakatifu - Paradisini kwa utii - Talanta iliyofanyiwa biashara - Kutazama mbele ya baadaye - Kazi zote za mema - Uchapaji na Aksyo Katoliki - Amali ya kijamii - Mazoezi ya roho ya makleri na walei - Kumtangaza Mwenye Heri Mjomba Don Yosef Cafasso

## 2. Mtume wa mitume..................................... 79

Mwali unaolipuka - Baada ya kushindwa ushindi maarufu - Mifumo na vizuizi - Njia za Mungu - Mkutano mwingine wa baraka ya Mungu - Kuponya kwa mwujiza - "Kwa jina lako nitatupa nyavu" – Uanzilishi - Tukio, huenda pekee... - ... na majikatalio nadra sana - Unabii wa kard. Cagliero - Masista Wamisonari wa Consolata - Kutanguliza nyakati - Mkuu wa Shirika - Wandugu wa wamisionari - Kichwa maji wa namna yake - Mwongozo wa utume

## 3. **Roho ya mtume** ............................................ 119

Mtu mkamilifu - Padre asiye na dosari - Siri kuu - "Laus perennis" ya Kanisa - Mwana wa Kanisa - Katika nyayo za Mjomba - Miali ya upendo wa Mungu - Tamaa ya kimungu ya Ekaristi - Mwelekeo wake hoihoi - Ustahi wa Makanisa - Mwenye ibada kwa Bikiwa Maria - Tajiri kwa maskini - Maskini kiwa ajili yake - Kama mwenge katika kivuli - "Abnege!"

## 4. Taji la utume ........................................... 175

Ukatili moyoni katika kelele la vita - Faraja toka mbinguni - - Mkutano mkuu wa kwanza - Kifo cha Mwanzilishi Msaidizi - Jubile ya kipadre - "Nunc Dimittis!" - Ugonjwa wa mauti - Kukumbatiwa na Mungu - Ombolezo la moyoni – Utukufu

## 5. Kungoja sauti ya Kanisa ............................ 207

Sauti ya Baba Mtakatifu - Sauti ya Makardinali - Sauti ya Maaskofu - Sauti ya wanafunzi - Mweka hazina wa Consolata - Uhamisho wa maiti

**END - MWISHO**